# KUCHUNGUZA USIHIRI KATIKA NGANO ZA ZANZIBAR

**JUMA HAMAD ABDULLA**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YAKUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

# ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo: ***Kuchunguza Usihiri katika Ngano za Zanzibar*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**....................................................**

**Prpf. Emmanuel Mbogo**

**(Msimamizi)**

**Tarehe:.............................................**

## IKIRARI

**Mimi JUMA HAMAD ABDULLA** nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na halisi, na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya Uzamili au shahada nyingine yoyote.

**Saini ………………………………..**

**Tarehe ………………………….**

## HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile Tasnifu hii kwa ajili yoyote kama vile Kieletroniki, Kurudufu Nakala Kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya Mwandishi au Chuo Kikuu Huria Kwa Niaba.

## TABARUKU

Kazi hii natabaruku kwa baba yangu mpenzi Bw. Hamad Abdulla Hamad wa Sizini Micheweni Pemba. Baba nashkuru sana kwa kunikuza kitaaluma hadi leo nimefika ngazi hii Pia kwa mama yangu mpendwa Bi. Asha Kombo Bakar wa Sizini Micheweni Pemba mama hongera sana kwa ushirikiano wenu na Baba kwa kunilea na kunipa ushauri faafu hadi leo kufikia hatua hii. Namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie afya njema na awape maisha marefu muzidi kuwalea vijana kwa ushirikiano wenu. Amiin.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa, natoa shukrani zangu zisizo na ukomo kwa ALLAH SUBHANAHU WATAALAH kwa sababu yeyé ndiye Mkuu na anayepaswa kushukuriwa kwa hatua yoyote ya maisha ya mwanadamu. Ninamshukuru kwa kunijaalia afya njema kipindi chote cha masomo yangu, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifa katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Nasema kwa unyenyekevu, Alhamdulillah Rabbil –alamin.

Pili, napenda kumshukuru kwa dhati Msimamizi wangu Prof. Emmanuel Mbogo kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Sina neno linalofaa kutoa shukrani zangu kwake bali namuombea afya njema na maisha marefu Pamoja na familia yake ili apate utulivu na aendelee kutoa msaada wa kitaaluma kwa wanafunzi wanaohitaji maarifa zaidi.

Tatu, nawashukuru sana wazazi wangu kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunifunza kuhusu ulimwengu. Vile vile, shukrani za pekee ni kwa mke wangu kipenzi kwa uvumilivu wake, huruma na kunitia moyo pale nilipokata tamaa.

Nne, napenda kuwashukuru wale wote walioshiriki katika utafiti huu kwa njia moja ama nyengine pamoja na ushirikiano walionipa kipindi chote cha kufanya utafiti huu. Nitakuwa mchache wa fadhila nisipotoa shukrani zangu kwa walimu wote walionifunza Kiswahili katika viwango tofauti akiwemo Bi. Ulfat Abul-Aziz.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza usihiri katika ngano za Zanzibar. Utafiti ulijikita kuchunguza namna vipengele vya usihiri vinavyojidhihirisha katika ngano za Zanzibar na namna vipengele vya usihiri vilivyotumika kuibua dhamira katika ngano teuele. Mtafiti alichagua mada hii kwasababu matumizi ya usihiri alibaini hayajachunguzwa katika ngano za Zanzibar.

Utafiti huu ulifanyika  uwandani katika ukusanyaji wa data. Maeneo yaliyotumika kukusanya data ni Sizini, Micheweni, na Wingwi. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya madhumuni maalum. Aidha, data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya maelezo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu.

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa ngano za Zanzibar zinatumia usihiri katika vipengele vya ujenzi wa wahusika, ujenzi wa mandhari, motifu za safari, ndoto, vyakula,wahusika, matukio mbali mbali Pia utafiti umegundua kuwa vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar vimetumika kuibua dhamira za ujasiri, malezi, ushujaa, uongozi mbaya, utu, uchoyo, kiburi, uvivu, ukarimu, ujanja, nafasi ya mwanamke, uhalifu, ukoloni na umaskini.

## YALIYOMO

ITHIBATI ........................................................................................................ ii
IKIRARI ........................................................................................................ iii
HAKI MILIKI ........................................................................................................ iv
TABARUKU ........................................................................................................ v
SHUKRANI ........................................................................................................ vi
IKISIRI…….. ........................................................................................................ vii
YALIYOMO ........................................................................................................ viii
ORODHA YA MAJADUELI ........................................................................................................ xiii
ORODHA YA VIAMBATANISHO ........................................................................................................ xiv
ORODHA YA VIFUPISHO ........................................................................................................ xv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ........................................ 1**
1.0 Utangulizi ........................................................................................................ 1
1.1 Usuli wa Mada ........................................................................................................ 1
1.2 Tatizo la Utafiti ........................................................................................................ 6
1.3 Malengo ya Utafiti ........................................................................................................ 7
1.3.1 Lengo Kuu ........................................................................................................ 7
1.3.2 Malengo Mahsusi ........................................................................................................ 8
1.4 Maswali ya Utafiti ........................................................................................................ 8
1.5 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................................ 8
1.6 Mipaka ya Utafiti ........................................................................................................ 10
1.7 Muundo wa Tasnifu ........................................................................................................ 10

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ........ 12**
2.0 Utangulizi ........ 12
2.1 Ufafanuzi wa dhana muhimu ........ 12
2.2 Aina za Ngano ........ 14
2.3 Dhana ya Usihiri ........ 16
2.4 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Ngano ........ 17
2.4.1 Tafiti kuhusu Ngano ........ 17
2.5 Dhana ya Dhamira ........ 23
2.6 Pengo la Utafiti ........ 25
2.7 Mkabala wa Kinadharia ........ 25
2.7.1 Nadharia ya Uhalisiajabu ........ 26
2.7.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisiajabu ........ 27
2.8 Hitimisho ........ 30

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 31**
3.0 Utanguliz ........ 31
3.1 Maana ya Mbinu za Utafiti ........ 31
3.2 Mpango wa Utafiti ........ 32
3.3 Eneo la Utafiti ........ 32
3.4 Uteuzi wa Watafitiwa ........ 33
3.4.1 Sampuli na Mbinu za Usampulishaji ........ 33
3.4.1.1 Usampulishaji ........ 34
3.4.1.1.1 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalum ........ 34

3.4.1.2 Sampuli ..... 36
3.5 Ukusanyaji wa Data ..... 37
3.6 Aina data za Data ..... 37
3.3.1 Data za Awali (Msingi) ..... 37
3.3.2 Data za Upili (Fuatizi) ..... 38
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ..... 38
3.6.1 Usomaji wa Nyaraka mbali mbali ..... 38
3.6.2 Mijadala ya Vikundi ..... 39
3.6.3 Usomaji Makini Maktabani ..... 40
3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data ..... 41
3.8 Vifaa vya Utafiti ..... 42
3.8.1 Shajara ..... 42
3.8.2 Kompyuta ..... 42
3.9 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti ..... 42
3.9.1 Usahihi wa Data ..... 42
3.9.2 Kuaminika kwa Data ..... 43
3.9.3 Maadili ya Utafiti ..... 43
3.10 Hitimisho ..... 44

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ..... 45**

4.0 Utangulizi ..... 45
4.1 Ngano Teule ..... 45
4.2 Vipengele vya Usihiri katika Ngano za Zanzibar ..... 45

4.2.1 Matumizi ya Wahusika wa Kisihiri ........................................................ 46
4.2.1.1 Wahusika wanyama ................................................................................ 46
4.2.2 Kubadilika Kutoka Umbile Moja kwenda Jingine.................................. 49
4.2.3 Matukio ya Kihalisiajabu.......................................................................... 52
4.2.4 Manuizo ya Kisihiri ................................................................................... 57
4.2.5 Ndoto za Kisihiri........................................................................................ 59
4.2.6 Vyakula vya Kisihiri .................................................................................. 61
4.2.7 Mawasiliano ya Kisihiri............................................................................. 61
4.2.8 Safari za Kisihiri ........................................................................................ 62
4.2.9 Mandhari ya Kisihri .................................................................................. 62
4.3 Dhamira za Usihiri Zinazobainishwa katika Ngano za Zanzibar .............. 65
4.3.1 Ujasiri........................................................................................................ 65
4.3.2 Malezi ....................................................................................................... 67
4.3.3 Ushujaa ..................................................................................................... 69
4.3.4 Uongozi Mbaya......................................................................................... 71
4.3.5 Utu............................................................................................................. 72
4.3.6 Uchoyo ...................................................................................................... 74
4.3.7 Kiburi ........................................................................................................ 75
4.3.8 Uvivu......................................................................................................... 78
4.3.9 Ukarimu .................................................................................................... 79
4.3.10 Nafasi ya Mwanamke ............................................................................... 80
4.3.11 Uhalifu ...................................................................................................... 82
4.3.12 Ukoloni ..................................................................................................... 84
4.3.13 Umasikini.................................................................................................. 87

4.3.14 Uchawi na Ushirikina ........................................................................ 90

4.4 Hitimisho........................................................................................ 92

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.......... 93**

5.0 Utangulizi........................................................................................ 93

5.1 Muhtasari wa Tasnifu ........................................................................ 93

5.2 Matokeo ya Utafiti ............................................................................ 95

5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza........................................................... 96

5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili ................................................................... 96

5.3 Hitimisho........................................................................................ 97

5.4 Mapendekezo .................................................................................. 98

5.4.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine.............................................. 98

5.4.2 Mapendekezo kwa Watunga Sera ................................................... 98

5.4.3 Mapendekezo kwa Taifa ................................................................ 98

**MAREJELEO ........................................................................................ 100**

**VIAMBATANISHO ................................................................................ 106**

## ORODHA YA MAJADUELI

Jadueli na .3.1  Idadi ya Washiriki wa Utafiti.......................................................... 35

Jadwali Na. 1 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Ujasiri............................................ 65

Jadwali Na. 2 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Malezi............................................ 67

Jadwali Na. 3 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Ushujaa.......................................... 69

Jadwali Na. 4 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uongozi Mbaya.............................. 71

Jadwali Na. 5 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Utu.................................................. 72

Jadwali Na. 6 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uchoyo .......................................... 74

Jadwali Na. 7 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Kiburi............................................. 75

Jadueli NA.4. 1 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uvivu........................................... 78

Jadueli NA.4. 2Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Ukarimu....................................... 79

Jedwali NA.4. 4 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Nafasi ya Mwanamke................. 80

Jadueli NA.4.5 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uhalifu.......................................... 82

Jedwali NA.4.6 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Ukoloni....................................... 84

Jedwali NA.4.7 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Umaskini .................................... 87

Jadueli NA.4.8 Hadithi nambari15: Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uchawi na Ushirikiana ........................................................................ 90

## ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho na. 1 Hadithi ya Zimwi na Mkia ..................................................... 106

Kiambatanisho na. 2 Hadithi ya Zena ................................................................ 108

Kiambatanisho na. 3 Hadithi ya Raajabu ............................................................ 109

*Kiambatanisho* na. 4 Hadithi ya Kijoka ............................................................. 112

Kiambatanisho na. 5 Hadithi ya Abanawasi na Sufuria ....................................... 114

Kiambatanisho na. 6 Hadithi ya Mbwa Mahoka ................................................. 115

Kiambatanisho na. 7 Hadithi ya Tatu na Saida .................................................... 117

Kiambatanisho na. 8 Hadithi ya Mazimwi Wala Watu ....................................... 120

Kiambatanisho na. 9 Hadithi ya Yamuimui ......................................................... 121

Kiambatanisho na. 10 Hadithi ya Babu Dii ......................................................... 123

Kiambatanisho na. 11 Hadithi ya Tango ............................................................. 124

KIambatanisho na. 12 Hadithi ya Jini Kisiki ...................................................... 125

Kiambatanisho na. 13 Hadithi ya Kilichomponza Nyoka Akakosa Maguu ....... 126

Kiambatanisho Na. 14 mwongozo wa maswali ya mijadala ya vikundi kwa ajili ya walimu wa fasihi wa shule za sekondari ................ 128

Kiambatanisho Na. 15 Picha ya Mtafiti Akiwa na Mtafitiwa ............................... 129

Kiambatanisho Na. 16 Picha ya mtafiti akitambiwa Ngano .................................. 130

Kiambatanisho Na. 17 Mtafiti akishiriki katika mijadala ya vikundi ya ................ 131

Kiambatanisho Na. 18 Mtafiti akishiriki katika mijadala ya vikundi ya walimu waskuli ya Chwaka Tumbe Sekondri kuhusu ngano.......... 131

Kiambatanisho Na. 19 Mtafiti Akitambiwa Ngano na Mtafitiwa........................... 132

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili la Zanziubar |
| KTJ | Ameshatajwa |
| K v | Kama vile |
| Prof | Profesa |
| (a.s) | Alaihi Salamu |
| Bw | Bwana |
| Bi | Bibi |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi inayobainisha vipengele vyote vya kiutangulizi katika utafiti huu. Vipengele vilivyobainishwa ni pamoja na, tatizo la utafiti, mada, usuli wa utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti ambayo utafiti huu umekusudia kuyajibu na umuhimu wa utafiti. Mipaka ya utafiti, Mpango/ muundo wa tasnifu na Hitimisho pia ni miongoni mwa vipengele vilivyobainishwa hapa.

Utafiti huu umehusu mada isemayo: Kuchunguza usihiri katika ngano za Zanzibar, kiukweli lengo la mtafiti ni kutaka kubaini namna ngano za Zanzibar zinavyotumia usihiri, hii ni kutokana na kwamba vipengele hivyo vya usihiri vinaibua dhamira zinazojitokeza katika maisha ya kila siku ndani ya jamii zetu.

## 1.1 Usuli wa Mada

Mada ya utafiti huu ni ‘’Kuchunguza Usihiri katika Ngano za Zanzibar’’. Al-Farsy (1993) anaeleza kuwa sihiri au uchawi ni aina ya athari ya nafsi na akili ambayo huanza fikirani na yaweza kuathiri mwili kwa njia ile ile kama athari au ushawishi wa kimwili iwezavyo kuathiri akili na fikra. Anasema kuwa ukweli hauwezi kubadilika kwa uchawi lakini mawazo ya mtu yakishabadilika na uchawi huanza kuhisi kuwa ukweli umebadilika. Anatolea mfano wa kamba na fimbo zilizotupwa na Firauni kwa Musa (a. s), kuwa hakika haikubadilika lakini watu na hata Nabii Musa (a. s) aliona kuwa zimebadilika. Hali lilisababisha Mwenyezi Mungu kumteremshia ufunuo Musa kuwa katu asiogope kwa vile ni yakini kwamba yeye atashinda na kwamba atupe chini fimbo yake. Tunaelezwa katika Qur-ani takatifu kama ifuatavyo:

> “Tahamaki, kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake (Musa) kwa uchawi wao, zinakwenda mbiombio.Basi Musa akaona hofu katika nafsi yake. Tukasema: Usiogope! Hakika wewe ndiye utakayekuwa mwenyekushinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kiume: kitavimeza walivyovitengeneza. Hakika wao wametengeneza hila za mchawi tu, wala mchawi hafaulu popote afikapo” (20:66-69)

Kwa ujumla, mtafiti ameona neno sihiri linafanyakazi pale ambapo, imani ya mtu inaanza kubadilika juu ya kuamini jambo fulani na matokeyo yake sihiri hufanya kazi kwa mnasaba wa imani ya mtu juu ya jambo hilo. Kwa hivyo, mawazo yaliyotangulia yamemsaidia mtafiti katika kuvibaini vipengele vya usihiri katika ngano na pia mtafiti amepata uwelewa ya kwamba mchawi hana mwisho mwema.

Mutiso (2012) anasema kuwa hakuna jamii yoyote ulimwenguni, iwe ni yenye imani za kidini au la, ambayo haina dhana ya nguvu za kulinda, kuleta baraka na kutibu. Nguvu hizi huwa ni za hirinzi ambapo neno hilo visawe vyake ni kago, kinga, zindiko, pagao, sihiri, uchawi, uganga, ndumba, mburuga, urogaji, ulozi, uchomozi, dawa, uwanga, uramli.

Hart na Ouyang, (2015), wanamnukuu Wamitila (2013), akielezea dhana ya mazingaombwe au maajabu neno ambalo katika kazi hii linachukuliwa sawa na usihiri kuwa lina ugumu katika kulielezea kwani ni neno ambalo hukiuka mipaka ya uhalisi kwa kuhusisha hali, matendo, mielekeo au matukio ambayo yanavuka mipaka ya “ukawaida” wa uhalisi. Maajabu au mazingaombwe ni dhana inayoweza kutumiwa kueleza chochote kinachokiuka ujarabati zikiwemo imani za kidini, ushirikina, migani, visasili na kadhalika.

Katika ufafanuzi wa aya zilizotangulia zinatoa muelekeo mzuri wa matumizi ya usihiri katika shughuli mbalimbali za jamii, na mtafiti ameona kuwa usihiri ni jambo maarufu katika jamii nyingi za Kiafrika ikiwemo Zanzibar ispokuwa kila jamii imeupa jina lake kutokana na mahitaji pamoja na matumizi yaliyokusudiwa.

Wamitila (2013) anafafanua kuwa kuna ugumu wa kuieleza dhana ya uhalisiajabu kutokana na sifa ambazo zinahusishwa na mikondo au matapo mengine ya fasihi kama uhalisiafifi, ulimbwende, usasa na usasaleo/usasabaadaye nakadhalika. Wamitila (ameshatajwa) anataja kazi ambazo ni za kiuhalisiafifi lakini zina sifa zinazohusishwa na uhalisiajabu. Wamitila anamnukuu Zamora na Faris (1995), wakieleza:

> Katika matini za kihalisiajabu matendo yasiyokuwa ya kawaida si jambo rahisi na dhahiri bali ni tukio la kila siku linalotokea, kukubalika, na kuwa sehemu ya urazini na matukio ya uhalisia wa kifasihi. Maajabu au mazingaombwe si matukio ya kiwazimu bali ya kikaida. Uk 35

Zamora na Faris (ameshatajwa), wanaendelea kueleza kuwa uhalisiajabu unaweza kuangaliwa kama mwendeleo wa uhalisia hasa kwa kuwa kimsingi unajihusisha na suala la hali ya uhalisi pamoja na uwasilishaji. Hata hivyo, unatofautiana na uhalisia wa kijadi kwa kuwa haudhibitiwi na misingi ya urazini unaohusishwa na kipindi cha baada ya utaalimifu wa kimagharibi. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, uhalisiajabu unavunja mipaka ya hali ya kawaida ya kuwako kwa kazi za fasihi kwa kuivuka mipaka ya hali ya kawaida ya kuwako kwa kazi za fasihi.

Maelezo hayo ni muhimu kwa mtafiti kwa sababu yamelenga kutoa ufafanuzi wa uhalisia ajabu, ambao pia ni mwendelezo wa uhalisia kwa vile unajihusisha na swala la uhalisia pamoja na utekelezaji wake.

Wamitila (2013) anawanukuu Herman na wenzake (2005), ambapo wanauona uhalisiajabu kama ni utanzu. Mkabala huu wa kuangalia uhalisiajabu kama ni utanzu pia unaungwa mkono na Zamora na Faris (1995). Wamitila anasema kuwa, mawazo haya yanaenda kinyume na mawazo ya Waliaula (2010), ambapo anauona mkabala wa uhalisiajabu kama nadharia.

Miongoni mwa vipengele vinavyohusishwa na uhalisiajabu katika fasihi kama vinavyojadilliwa na Wamitila (2013), ni pamoja na mbinu za kisimulizi za matukio yasiyokuwa ya kawaida, njozi au fantasia, michezo na utatizaji wa dhana ya wakati ambapo kwa kiasi kikubwa hutumia wakati wa kivisasili, matumizi ya mitindo ya udenguzi na uumbuzi. Pia, kazi za kiuhalisiajabu huwa na sifa ya umahuluti wa kitamaduni, kitanzu na mwingilianomatini, wahusika huwa ni wa kinjozi, visasili au fantasia na matendo yao hayadhibitiwi kamwe na kanuni wala sheria za maisha ya kawaida. Vilevile, kunakuwa na ishara na usitiari na mfumo mzima wa uashiriaji ambazo zinatatiza suala la ubainishaji wa maana ya kifasihi ya kazi inayohusika. Aidha, kazi za kiuhalisiajabu huwa na sifa ya kiontolijia, yaani ni mkondo unaoruhusu ukiukaji wa kazi wa kaida au mipaka ya kitanzu, kisiasa, kijiografia, kihistoria, au hata kiontolojia yaani hali ya kuwako kwa kazi inayohusika.

Chaligha (2013) katika makala yake alipokuwa anajadili vigezo vya Ruth Finnegan katika Utendi wa Lianja anagusia suala la usihiri alilonalo mhusika Lianja. Anaeleza mazingira ya kisihiri kwa kusema kuwa, Lianja baada ya kuwaua watu katika vita kati ya Wasau-sau na Wamongo aliwapuliza dawa wote wakafufuka na kuwa wazima. Pia, alikuwa na kengele yake ya kisihiri ambayo alipoipiga na kusema maneno wakati anaipiga yale maneno yanatimia kama alivyosema. Usihiri huo pia ni

pamoja na nguvu za kiume kama alivoonekana Ilele, (baba wa shujaa alimuoa Mbombe) na kuzaa watoto wengi kwa mimba yake moja.

Mchango huo wa Wataalamu umemsaidia mtafiti kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza utafiti wake kwani vimetajwa baadhi ya vipengele ambavyo vinahusishwa na uhalisiajabu katika fasihi kama vile mbinu za kisimulizi za matukio yasiyokuwa ya kawaida, njozi, na hata matumizi ya mitindo ya udenguzi na uumbuzi. Kwa hiyo imemsaidia mtafiti katika kuziendea kazi za fasihi ikiwemo ngano za Zanzibar na kuona jinsi usihiri unavyojitokeza na kutumika.

Wamitila (2013) anaeleza kuwa katika fasihi ya Kiswahilia baadhi ya kazi zinazohusishwa na uhalisiajabu ni: Nagona na Mzingile (zote za Kezilahabi), Babu Alipofufuka, Dunia Yao, na kwa kiasi fualani Nyuso za Mwanamke (zote za S. A. Mohamed), Bina- Adamu! na Musaleo! na labda kwa kiasi fulani Dharau ya Ini za (K. W. Wamitila), Ziraili na Zirani (ya William Mkufya) na Shimo la Maangamizi (ya H. P. Simai). Wamitila anaendelea kusema kuwa,kazi za fasihi za hivi karibuni zina sifa ya uhalisiajabu. Hata hivyo anaamini kuwa, kazi za mwanzo za fasihi andishi ya Kiswahili zina sifa za uhalisiajabu. Anataja riwaya ya Kusadikika, Kufikirika na Adili na Nduguze za Shaaban Robert kuwa ni mifano ya kazi zenye mitindo ya kiuhalisiajabu.

Mapitio yetu yanaonesha kuwa tafiti nyingi zimefanyika kwa nia ya kuchunguza usihiri katika fasihi andishi ya Kiswahili, hata hivyo, ngano za Uswahilini hazijatafitiwa kwa mawanda mapana ili kuchunguza matumizi ya usihiri. Hivyo basi, katika utafiti huu tumedhamiria kuchunguza matumizi ya usihiri katika ngano za

Zanzibar. Hali hiyo, inatupasa kujiuliza ngano ni nini? Swali hili linaweza kujibika kwa kifupi tunapomrejelea Wamitila (2003), akieleza kuwa ngano ni hadithi za kimapokeo ambazo huwatumia wahusika kama vile wanyama, miti, watu nakadhalika  kusimulia tukio au kisa fulani chenye mafunzo. Aina za ngano anazozibainisha Wamitila (ameshatajwa) ni kama vile ngano za mazimwi, ngano za usuli, ngano za kishujaa, ngano za hekaya, ngano za hurafa au wanyama, ngano za mtanziko, ngano za kimafumbo (k.v. ngano za istiara, mbazi/vigano, mcahapo/ kidahizo), ngano za kichimba kazi/ kudhubahi na soga.

Kwa uzoefu wetu tumebaini kuwa pamoja na watafiti wengi kuzungumzia uchawi katika fasihi andishi, hata hivyo tunaamini zipo ngano za Zanzibar ambazo zina akisiko la matukio ya usihiri katika vipengele mbalimabali.Ngano hizo hufumwa kwa mitindo ambayo inakiuka matukio ya uhalisia wa kijamii. Mathalani, ngano ambazo binadamu huweza kuruka angani kama vile ndege kwa kutumia nguvu za kisihiri ni miongoni mwa ngano zilizo na sifa  za usihiri.

Kwa minajili hiyo, baada ya kupitia maandishi kadhaa ambayo yanahusu tafiti za hadithi simulizi hatukuona utafiti uliojikita kwa kina kutafiti kipengele cha usihiri katika hadithi hizo. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu ulidhamiria kufanya uchunguzi katika ngano za Zanzibar ili kugundua namna hadithi hizo zilivyotumia usihiri katika kuibua dhamira kwa jamii. Hata hivyo, tumeona ipo nafasi ya kufanya utafiti huu.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Ngano ni utanzu wa fasihi simulizi ambao ulipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi chengine kwa njia ya masimulizi ya mdomo Senkoro, 2011. Breket Tafiti nyingi

ziliwahi kufanyika kuhusiana na ngano. Mathalani, watafiti kama vile Sengo (1985), Senkoro (1997), Haji (2013), Hamad (2013), Mzee (2015), Ali (2015), wamewahi kufanya uchunguzi kuhusiana na ngano katika vipengele vya fani na maudhui. Kwa mfano, Omar (2013), alifanya utafiti uliojikita katika kuchunguza dhima za hadithi simulizi katika kukuza maadili ya wanafunzi wa shule za Sekondari za Zanzibar. Katika utafiti huo aligundua kwamba, hadithi simulizi zimekuwa zikitunza maadili ya vijana wa Zanzibar katika nyanja mbalimbali. Hamad (2013) alichunguza mhusika Abanawasi katika ngano za Zanzibar na kugundua kwamba muhusika huyo anawakilisha watu wajanja,wenye kutumia akili kuwalaghai wengine, wasiopenda kushirikiana na wengine na kadhalika. Pamoja na mapitio hayo, mtafiti hakuona kazi iliyowahi kufanywa kwa nia ya kuchunguza usihiri katika ngano za Zanzibar. Hivyo basi, swali linalotatiza utafiti huu ni Je, kuna vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar? Je, matumizi ya usihiri hubeba dhamira gani katika ngano za Zanzibar? Kutokana na maswali hayo, tatizo la utafiti huu ni kutaka kuchunguza usihiri katika ngano za Zanzibar, ili kubaini jinsi usihiri unavyotumiwa na watunzi kama msingi wa utunzi wa ngano za Zanzibar na namna usihiri unavyoibua dhamira katika ngano husika.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo la jumla na malengo mahsusi kama yanavyojionyesha katika sehemu ifuatayo:

### 1.3.1 Lengo Kuu

Kuchunguza usihiri katika ngano za Zanzibar, ili kuona ni jinsi gani ngano hizo zinavyotumia vipengele vya usihiri katika kuibua dhamira.

### 1.3.2 Malengo Mahsusi

Utafiti huu, una malengo mahsusi mawili.

1) Kubainisha vipengele vya usihiri vinavyojitokeza katika ngano za Zanzibar.
2) Kubainisha dhamira zinazoibuliwa na vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

1) Ni vipengele vipi, vya usihiri vimejitokeza katika ngano za Zanzibar?
2) Ni dhamira zipi zinazoebuliwa na vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu zifuatazo:

Kitaaluma**:** Utafiti huu umetoa mchango katika taaluma ya fasihi kinadharia na vitendo. Kwa kueleza na kuchambua usihiri unavyojidhihirisha katika ngano za Zanzibar. Tumeweza kubaini ni jinsi gani ngano za Zanzibar zinavyotumia mbinu za kisihiri katika kuibua dhamira zake. Aidha, utafiti huu utaweza kutumika katika taaluma ya fasihi simulizi, hivyo utatumika kama marejeleo kuhusu hadithi simulizi za Zanzibar.

Kinadharia**:** Mtafiti kupitia utafiti huu, ameongeza maarifa kupitia weledi alioupata katika matumizi ya nadharia na mbinu za uhakiki wa hadithi simulizi za Kiswahili. Kwa vile alipata muongozo wa uchanganuzi wa data na kufanya mijadala ambayo imesaidia kujibu maswali ya utafiti hatimae kutoa matokeo ya utafit.

Kwa watafiti wengine, utafiti huu utakuwa ni kichocheyo kwa watafiti wengine kutupia jicho fasihi simulizi ya Kiswahili. Hivyo basi, utafiti wetu utawashajiisha watafiti wapya waweze kuchunguza na kuchambua tanzu kadhaa za fasihi simulizi ili kuona jinsi gani dhamira za usihiri zinavyojitokezana kuakisi mazingira halisi ya jamii.

Kwa jamii, utafiti huu umetarajiwa utasaidia sana kudhihirisha nafasi ya usihiri na mchango wake katika maisha ya kila siku.

Kwa taifa,Taifa lolote lile linahitaji wasomi walio andika ili kumbukumbu zao zitumike katika harakati mbalimbali za kitaifa kama vile uchumi, siasa na hata kijamii, utafiti huu ni miongoni mwa kumbukumbu zitakazotoa msukumo kwa taifa na kutumiwa na viongozi mbalimbali wa vyama na serikali ili kuchunguza na kuthibitisha kile wanachotafuta.

Kwa mtafiti, Mbali na hayo utafiti huu umempa mwanga mtafiti katika kukuza upeo wake wa taaluma kwa kuzamia kwa kina maandiko mbali mbali kama vile, tasnifu, majarida, vitabu mbali na kubaini kwamba ngano za Zanzibar zimesheheni matukio kadhaa ya kisiasa kiuchumi na hata ya kijamii pia kupitia ngano hizo zinaelimsha zinaadilisha na hata kuionya jamii pale ambapo ita kwenda kinyume na maadili ya jamii lengwa. Hivyo basi, kupitia umuhimu huo uliopatikana katika utafiti huu pia umemsaidia mtafiti kujibu maswali yake ya utafiti.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Pamoja na kuwepo kwa matapo mengi ya hadithi simulizi, kama vile uhalisiafifi, ulimbwende, usasa na usasaleo au usasabaadae, tumeona haitokuwa rahisi kutafiti matapo yote hayo. Hivyo basi, utafiti huu umejikita kuchunguza na kuchambua ngano za Zanzibar ambazo zimetumia vipengele vya usihiri, kwa vile mtafiti amebaini zitakidhi haja ya kulijibu swala la kwanza na la pili la utafiti wetu.Sababu ya kuchagua ngano ni kwa vile hadithi hizi zina athari kubwa katika fasihi ya Kiswahili. Pia, kutokana na umaarufu wa hadithi simulizi katika jamii za Uswahilini na nje ya eneo la uswahilini tumeona kuwa bado hakuna utafiti wa kina uliowahi kufanywa kwa nia ya kuchunguza usihiri katika hadithi hizo.

## 1.7 Muundo wa Tasnifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Kila sura imegaiwa katika sehemu ndogo ndogo kama ifuatavyo:

**Sura ya Kwanza -** imehusu vipengele muhimu vifutavyo:

Sura Utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, mpango au muundo wa tasnifu na hitimisho

**Sura ya Pili- Mapitio ya kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia:** Sura hii imesheheni vipengele vifuatavyo: Utangulizi, ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia: Nadharia ya uhalisia ajabu na hitimisho.

**Sura ya Tatu- Mbinu za Utafiti**: Sura hii imehusu uchambuzi wa vipengele vifuatavyo: Utangulizi, maana ya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji.

**Sura ya Nne- Uwasilishaji, Uchambuzi na mjadala wa data za utafiti:** Sura hii imejadili vipengele vifuatavyo: Utangulizi, ngano teule, uchanganuzi wa vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar, dhamira zinazo wasilishwa na vipengele vya usihiri katika hadithi simulizi za Zanzibar na hitimisho.

**Sura ya Tano- Muhtasari,hitimisho na mapendekezo**: Sura hii imejitokeza utangulizi, muhtasari wa tasnifu,, matokeo ya utafiti, mapendekezo, hitimisho, marejeleo, viambatanisho pamoja na orodha ya majaduweli.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kina wa maandishi ya watafiti watangulizi, unaofanywa na mtafiti kwa ajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi lazima yaonyeshe uhusiano wa maandishi hayo na mada ya utafiti. Katika mapitio ya kazi tangulizi huoneshwa pia nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data. Aidha, mapitio ya kazi tangulizi ni maarifa yanayopatikana kwa usomaji wa kina maandishi hayo ya huko nyuma ambayo hufananishwa na taarifa hai zilizopatikana ndani ya utafiti wa sasa (Enon, 1998).

Hivyo basi, sehemu hii inahusu mapitio ya kazi tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti. Sehemu hii imegawika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni mapitio ya maandiko kuhusu ngano na sehemu ya pili inaelezea mkabala wa nadharia.

Kwa misingi hiyo sura hii imeimarisha utafiti hususan kwa kurejelea kazi mbalimbali tangulizi zenye uhusiano na mada ya tafiti. Ili kujenga ithibati na umakini wa kutimiza haja ya malengo na maswali ya utafiti.

## 2.1 Ufafanuzi wa dhana muhimu

Katika sehemu hii tumefanya ufafanuzi wa dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu. Hivyo basi, dhana hizi zimefanyiwa ufafanuzi huku zikirejelewa kwa kutumia mawazo ya waandishi kadhaa watangulizi kadri ilivyoonekana inafaa. Ufafanuzi wa dhana hizo ulifanyika kama ifuatavyo:

Senkoro (1997) anafafanua utanzu wa ngano kwa kuwatazama wasimuliaji wa ngano; yaani hadhira. Anaona kuwa bibi ama babu wasimuliapo watoto hadithi fulani katika jamii, watoto huielewa ngano hiyo na wasimulianapo wao kwa wao huchukua nafasi ya kuwa watunzi.

Nao Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa ngano ni hadithi zinazotoa mifano kadhaa wa kadhaa ya maisha ya binadamu na matatizo anayokumbana nayo ulimwenguni. Dhamira kuu ya ngano nyingi ni kuonesha jinsi binadamu anavyotumia akili yake na anavyoweza kuyamudu matatizo yanayomkabili na hivyo kuweza kuishi maisha ya raha mustarehe. Kwa upande mwingine, ngano huonesha kuwa watu wasiotumia akili katika matatizo yaliyowakabili huangukia katika maangamizi . Wakati mwengine binadamu huweza kufunzwa na ulimwengu, hapa ulimwengu huweza kuchukuliwa kuwa ni viumbe wengine kama majini mazimwi na wanyama.

kimapokeo ambazo hutumia wahusika kama vile wanyama, miti au watu kusimulia tukio au kisa fulani chenye mafunzo. Anaendelea kueleza kuwa neno ‘ngano’ hutumiwa katika jamii kwa maana pana sana kiasi kwamba aina nyingine ya simulizi au hadithi zinaweza kuingia kwenye kundi la ngano.

Omar (2013), anamnukuu M’Ngaruthi (2008), akieleza kuwa hadithi ni kisa au matukio halisi au yaliyobuniwa. Hadithi hizi za kimapokeo hujulikana kama ngano. Anaendelea kueleza kuwa, hata hivyo baadhi ya ngano zimebadilika kiasi kwamba zinaposimuliwa na wasimulizi tofauti husikika kama ngano tofauti. Hali hii hujitokeza kutokana na baadhi ya wasimulizi kuondoa au kuongeza mambo fulani

katika hadithi wasimuliapo ama kwa kutaka kuongeza chumvi au kutokana na usahaulifu wa baadhi ya sehemu za hadithi asilia.

Baada ya kupitia fasili kadhaa zinazohusu ngano tunaweza kusema kuwa, ngano ni hadithi za kimapokeo ambazo husimuliwa kwa njia ya mdomo na kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Hadithi hizo huweza kuwa na wahusika wanyama, wadudu, majini, Mungu, malaika, mazimwi, binadamu nakadhalika ambao hutumika ili kuakisi tabia za watu waliomo katika jamii husika. Hii ni kusema kuwa hata wanyama wanapotumika katika ngano huwa wanabeba ujumbe unaowahusu wanadamu.

## 2.2 Aina za Ngano

Suala la ugawaji wa ngano limekuwa ni changamano. Hii ni kutokana na kwamba, uainishaji wa vipera vya ngano umekuwa ukitofautiana kati ya mtaalamu mmoja na mwingine Mathalani, Ndumbaro (2013), anawanukuu Khamisi na Madumulla (1989), wakibainisha vipera vya ngano kama ifutavyo:

Isitiara- Ni hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine iliyofichikana yaani, hadithi nzima ni kama sitiari.

Mbazi- Ni hadithi fupi yenye mafunzo itolewayo kama kielelezo wakati wa maongezi au wa kumkanya mtu.

Kisa- Ni hadithi fupi ya kufurahisha kuhusu tukio la kweli.

Kwa upande mwengine Kubo na wenzake (2011), wananukuliwa na Maeda (2016), ambapo wanabainisha ngano katika vipera vifuatavyo:

Visasili- Ni hadithi zinazoelezea kwa nini viumbe tofauti huwa na tabia, maumbile au uhusiano fualani. Kwa mfano, sababu ya mbuni kuwa na shingo ndefu.

Hekaya- Ni ngano fupi zinazohadithia matukio yanayoonesha hila, ujanja na kustaajabisha mara kwa mara. Kwa mfano, hadithi ya Abunuwasi na sufuria.

Hurafa- Ni masimulizi ambayo hutumia wanyama kama wahusika katika kutoa ujumbe wake. Hutumia mbinu ya kuvipa uhai vitu na sifa za kibinadamu vitu ambavyo kwa kawaida havina uhai. Wanyama ambao hutumiwa sana katika hurafa ni kaka sungura, fisi, mzee kobe, chura, ndege na nyoka.

Istiara- Ni hadithi ya kimafumbo ambayo maana yake haijitokezi moja kwa moja. Maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine isiyokuwa ya wazi. Kwa mfano, ngano ya *Msafiri na Ngamia.*

Ngano za Kijanja- Ni masimulizi kuhusu wanyama wadogo wanaotumia ujanja wahali ya juu ili kujinasua na hali ngumu au mtego waliotegewa.

Mbazi- Ni hadithi isiyokuwa ndefu inayotolewa katika maongezi ili kutoa mafunzo yenye uadilifu.

Ngano za mazimwi- Ni masimulizi yanayohusu majitu ya ajabu ambayo hudhuru na kumuangamiza binadamu.

Ngano ya mtanziko- Haya ni masimulizi ambayo mhusika mkuu anajikuta katika hali ngumu na anashindwa kutoa uamuzi wowote kwakuwa kila aina ya uamuzi ungemletea athari mbaya.

## 2.3 Dhana ya Usihiri

Usihiri ni dhana tata ambayo hubeba maana changamano miongoni mwa wanajamii. Dhana hii imekuwa ikipewa visawe kama vile uchawi, mazingaombwe, ndumba n.k. Katika taaluma ya fasihi usihiri umekuwa ukihusishwa na dhana ya uhalisiajabu. Mathalani, Roh (1925) alitumia neno uhalisiajabu katika muktadha wa ulimwengu wa sanaa kueleza aina fulani maalum ya kudhihirisha usiri ulioko kwenye maisha ya kila siku bila kuupigia maswali yoyote uhalisia huo. Pamoja na hayo uhalisiajabu katika kazi ya sanaa hushughulika na kazi zinazoambatana na zisizoambatana na ujumi wa uhalisia.

Chanady (1985), katika Rio (1999), anasema kwamba uhalisiajabu unahusu matukio yasiyo ya kawaida, ya kimiujiza au chochote kilicho kinyume cha uhalisia wa kawaida. Suala muhimu zaidi ni kwamba matukio yanayotendeka katika uhalisiajabu hayawezi kujitenga na uhalisia. Matukio yasiyo ya kawaida, ya kimiujiza na ni kinyume cha uhalisia wa kawaida.

Namkate (hainamwaka) akieleza dhana ya usihiri anasema kwamba ni ile hali ya kuonekana kitu athari yake au manufaa yake bila ya chenyewe kuonekana. Mawazo haya ya namkate yanatudokeza kwamba usihiri kwa kawaida huwa ni suala lililofichika. Kwa hivyo tutayatumia mawazo haya ili kuona namna usihiri unavyojidhihirisha katika ngano za Zanzibar.

Njogu na Chimera (1999) wanasema uchawi kama imani ya jadi hutumika katika kazi za fasihi ili kuhifadhi utamaduni wa mababu ambao unatupiliwa mbali na kizazi cha sasa cha Afrika. Pia, hutumika ili kuweka daraja kati ya tamaduni za kale na za

sasa ambazo zina athari ya Kimagharibi. Hivyo, imani hizi hutumika ili kuonesha migongano iliopo kati ya tamaduni hizi mbili. Wanatolea mfano wa uchawi katika tamthilia za Afrika kwamba uchawi umetumika kama jazanda inayosimamia uongozi au uwezo kati ya kundi moja na jingine. Mfano mzuri wa uchawi hutumika kijazanda na urogi kuwa ni pale mwandishi anapotuonesha taswira ya uongozi mbovu uliomo katika tamthilia ya Ngoma yaNg`wanamalundi. Kwa hakika uchawi ndio mihimili mikuu ya tamthilia hii.

Maelezo haya ni muhimu katika kufikia malengo ya utafiti huu kutokana na kutuonesha namna usihiri unavyoweza kuibua dhamira za fasihi. Hivyo, tutayachukua mawazo haya kama msingi wa kufikia malengo yetu tutapochunguza usihiri katika ngano za Zanzibar. Aidha, mawazo hayo yamekuwa ni muhimili imara wa utafiti huu katika kulifikia hitimisho kwa kina na kwa haraka, jambo ambalo limeibua hisia kubwa kwa wasomaji wa kazi za fasihi kwa kila mmoja kuwa na hamu ya kutaka kujisomea kwa lengo la kupata maarifa zaidi.

Pamoja na maelezo haya kuhusiana na dhana ya usihiri ambapo huangaliwa kama ni mifano ya uhalisiajabu. Katika utafiti huu tuliona kuwa uhalisiajabu ni dhana pana ambayo usihiri ni dhana finyu inayopatikana ndani yake. Kwa mantiki hiyo kazi hii haikuchukulia kila kipengele cha uhalisiajabu kuwa ni sawa na usihiri.

## 2.4 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Ngano

### 2.4.1 Tafiti kuhusu Ngano

Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kina wa maandishi ya watafiti watangulizi, unaofanywa na mtafiti kwa ajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi lazima yaonyeshe uhusiano wa maandishi hayo na mada ya utafiti.

Vilevile katika mapitio ya kazi tangulizi huoneshwa nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data (Enon, 1998).

Sababu kuu ya kuyapitia maandiko yaliyotangulia kuhusu somo la utafiti ni kuhakikisha kuwa swali lililotafitiwa awali halirejewi tena kwa kutoelewa. Kwa mnasaba huo, sehemu hii imemsaidia mtafiti kuwa kazi yake ikikamilika itatoa mchango mpya katika eneo la taaluma anayoishughulikia (Buliba na wenzake, 2014).

Tafiti mbali mbali zimewahi kufanywaa kuhusu ngano. Hapa tumewachunguza watafiti kama vile Mghanga (1984), Njue (1989), Senkoro (1997), Njogu na Chimera (1999), Omar (2013), Hamad (2013), Haji (2013), Oyoyo (2013), Ali (2015), Mzee (2015), na Nyemsenda (2015), wamewahi kufanya tafiti kuhusu ngano katika vipengele vya fani na maudhui. Mathalani, Mghanga (1984), alichunguza ngano tano za Kidawida zilizoandikwa na Mbele. Katika ngano hizi, Mghanga alishughulikia maudhui kwa kutumia nadharia ya Kimarx. Anasema kuwa fasihi haiwezi kuwa fasihi bila ya mwandishi, msimulizi au msanii kutumia lugha kwa njia ambayo itamwezesha kuwasiliana na wasomaji ama wasikilizaji wake kwa njia ya kuwavutia na ambayo itawafanya wasome ama wasikilize ujumbe wake. Kazi hii ilitupa msukumo kufikia malengo ya utafiti wetu kutokana na kutuonesha namna data zinazohusu ngano zinavyoweza kufanyiwa uchambuzi. Tofauti ya kazi yake na utafiti huu ni kwamba sisi tunajikita kuchunguza usihiri katika ngano za Zanzibar wakati yeye alishughulikia ngano tano za Kidawida katika vipengele vya fani na maudhui.

Aidha, Njue (1989) alichambua ngano za Waswahili huku akishughulikia ujumbe pamoja na mafunzo kwa jamii iliyozizusha. Pia, amezungumzia wahusika, ploti ya ngano na umuhimu wa fasihi kwa jumla. Uhakiki wake ulihusisha baadhi ya vipengele vya fani kama vile wahusika na ploti umetufaa. Hata hivyo, bado katika kazi hiyo kunaonekana kuna pengo kwani Njue hakushughulikia usihiri kama tunavyofanya katika utafiti huu. Kwa mnasaba huo ni dhahiri kwamba, utafiti wetu utaziba pengo lililoachwa na mwandishi huyo kwa lengo la kuifanya jamii ya waswahili hususani wale wapenzi wa fasihi kuondokana na kadhia mbalimbali katika uga wa fasihi simulizi.

Kadhalika, Senkoro (1997) alichunguza motifu za safari katika ngano za Zanzibar. Katika utafiti huo anaeleza kuwa shujaa katika ngano za Zanzibar lazima asafiri kutoka nyumbani iwe kwa kufahamu au kutofahamu. Pia, shujaa hupambana mwenyewe na mara nyengine hupata msaada kutoka kwa dege, mtu, au kitu chochote. Vile vile shuja wa ngano za Zanzibar huwa na busara na hekima. Utafiti huu pia ni muhimu katika kufikia lengo la utafiti wetu. Hii ni kwa sababu tunapozitafiti ngano teule tumeona shujaa na tumemchunguza kwa undani na tumebaini shujaa huyo anatumia usihiri au katika kuiendeleza kazi yake. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mara nyingi mashujaa katika ngano nyingi za Waswahili hupewa uwezo mkubwa kuliko ilivyozoeleka kwa binadamu wa kawaida, jambo ambalo sisi tunalichukulia kama ndio usihiri wenyewe.

Pia, Njogu na Chimera (1999) walifanya uchambuzi wa ngano na namna ya kufundisha ngano darasani. Katika uchambuzi wao wametumia mfano wa ngano ya *“Mvulana na Jusi Kuuu”* kuhakiki baadhi ya vipengele vya fani ambavyo huwa

vinajidhihirisha katika ngano. Hata hivyo, kazi hiyo pia haikugusia kwa aina yoyote suala la usihiri ambalo ni hoja muhimu katika utafiti huu. Uchambuzi wa Njogu na Chimera (wameshatajwa) ulikuwa na manufaa kwa mtafiti kutokana na kuonesha namna ya uchambuzi wa ngano unavyofanyika. Hali hii ndiyo iliyotushawishi na kuweza kuyachukua mawazo hayo na kuyafanya kama mwega wa kusogeza mbele zaidi katika kuiendea mada yetu.

Vilevile, Hamad (2013), alichunguza mhusika Abanawasi katika ngano za Zanzibar. Katika utafiti huo amegundua kuwa Abanawasi ni mhusika anayetumia ujanja, akili, ulaghai pamoja na akili za hali ya juu katika kupambana na masaibu yaliyomkabili. Utafiti huu pia ni chanzo cha utafiti wetu kwani tumejifunza namna dhamira zinavyoweza kujitokeza katika ngano za Zanzibar. Kwa mantiki hiyo, tutachukua mawazo ya Hamadi katika kushadadia utafiti wetu. Kwani mara kadhaa wahusika wa aina hiyo hutumia nguvu za kiza na kufanya jambo ambalo ni vigumu kufanyika katika hali ya kawaida, na hii kwetu sisi tunaichukuwa kama ndio dhana nzima ya usihiri.

Pamoja na hao, Haji (2013) alifanya uchunguzi kwa nia ya kuchunguza dhima za ngano katika kukuza maadili mema ya wanafunzi wa shule za sekondari, visiwani Zanzibar. Utafiti huu utakuwa na manufaa sana katika kufikia lengo la utafiti huu. Hii ni kwasababu hadithi zilizotafitiwa na Omar zinatarajiwa baadhi kuingia katika mkabala wetu. Tofauti ya utafiti wa Omar na utafiti wetu ni kwamba sisi tumechunguza usihiri kwa mkabala wa Nadharia ya Uhalisiajabu lakini yeye hakufanya hiivyo. Jambo ambalo lilitupa ari kubwa ya kutaka kuziba pengo lililoachwa na watafiti tangulizi, Omar akiwa ni miongoni mwao.

Kwa kuongezea, Oyoyo (2013), hakuachwa nyuma kwani alifanya uchunguzi katika ngano tano za Kiswahili. Katika utafiti huo Oyoyo alichunguza vipengele vya fani na baadae kulinganisha miundo ya ngano alizoziteua. Utafiti huo uligundua kuwa misuko na masimulizi pamoja na uumbaji wa wahusika vimeingiliana vizuri na kushikamana kiasi kwamba huwezi kuondoa moja kisha muundo wa ngano ile ikabakia na uwezo wa kuwa na umbo lililokusudiwa. Ama kuhusu matumizi ya lugha, utafiti huo ulihitimisha kuwa, msimulizi ameweza kuwasilisha maana ya sifa katika ngano hizi. Tamathali za usemi zimetoa taswira na sifa mbalimbali za wahusika.

Wahusika wanyama, katika ngano hizi wametumiwa kisitiari kuwakilisha tabia za binadamu halisi katika jamii. Wahusika hawa ni wa viwango viwili tu, aidha wabaya au wazuri. Mhusika mwenye tabia mbaya hastahili kuigwa. Watunzi wa ngano hizi wamewaumba wahusika wao vizuri. Pia, wametumia misuko sahili ambayo inasaidia kueleweka kwa ngano hizi kwa njia rahisi. Fani katika ngano hizo imeingiliana vizuri na vipengele vyake haviwezi kutenganishwa. Ingawa lengo la Oyoyo lilikuwa ni tofauti na lengo la utafiti wetu, hata hivyo tutapata uwelewa wa namna ya kubaini vipengele mbalimbali vya fani na maudhui kuhusu ngano za Uswahilini. Pia mchango wake utasaidia kujibu lengo la kwanza na la pili la utafiti wetu.

Fauka ya hayo, Ali (2015) alifanya uchunguzi wa namna hadithi simulizi za jamii ya Wapemba zinavyomchora mwanamke. Katika utafiti huo aligundua kuwa hadithi simulizi za jamii ya Pemba zimemchora mwanamke akiwa na dhima kadhaa. Baadhi ya dhima hizo ni kama vile; mwanamke ni mlezi, mwanamke ni mwenye majungu, mwanamke ni mshauri, mwanamke ni msaliti na kadhalika. Utafiti huu unamanufaa

na umuhimu mkubwa katika kufikia malengo yetu, Hii ni kwa sababu Ali (ameshatajwa), alichambua dhima za mwanamke katika hadithi hizo za jamii ya Pemba jambo ambalo limetupa utambuzi wa namna ya kuziibua dhamira katika ngano tulizozitafiti ili hatimae kutuwezesha kujibu swali letu linalohusiana na dhamira katika ngano zenyekutumia usihiri.

Hata hivyo, Mzee (2015) alifanya uchunguzi juu ya maudhui yanayopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, Nadharia ya Sosholojia na Nadharia ya Simiotiki. Katika utafiti huo Mzee aligundua kuwa hadithi za watoto za jamii ya Wapemba zina dhamira za ugumu wa upatikanaji wa elimu, umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii, mapenzi na ndoa, kuonya, nafasi ya mwanamke, ukarimu, uzembe na uvunjifu wa kanuni. Pia, alichunguza vipengele vya fani vinavyosaidia kuibua dhamira katika hadithi za watoto na kugundua kuwa vipengele hivyo ni wahusika, matumizi ya lugha, muundo mtindo na mandhari. Aidha, aligundua kuwa hadithi za watoto zina ujumbe kama vile wazee kuwaasa watoto juu ya kufuata ushauri wa wazazi wao kwa kila wanalotaka kulifanya, kujitenga na mambo ambayo yanaweza kuwaletea matatizo, wanataluma wawe na uvumilivu; wasiwe na ufedhuli na lugha chafu kwa wanafunzi nakadhalika. Katika utafiti wa Mzee (ameshatajwa), tumejifunza mengi kuhusu ngano za Uswahilini. Kwanza tumejifunza namna dhamira zinavyoweza kuibuliwa, pili tumeona namna vipengele vya fani vinavyoibua dhamira katika ngano. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu umekuwa ni chanzo kikubwa katika kufikia malengo ya utafiti huu. Hata hivyo, Mzee alichunguza hadithi simulizi akiongozwa na nadharia ya sosholojia na mwitiko wa

msomaji tofauti na sisi tumechunguza ngano ambazo zina usihiri tukiongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu.

Kwa kumalizia, Nyemsenda (2015) alichunguza ushujaa wa shujaa wa motifu za safari na msako katika ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari. Utafiti huo uliongozwa na nadharia ya Vikale, Umuundo, Saikolojiachanganuzi na Nadharia ya Sosholojia. Pamoja na mambo mengine, utafiti huo uligundua kuwa jamii hizo zinatofauti za kiutamaduni, kijamii, kihistoria, kijiografia, kifalsafa na tofauti ya kaida mbalimbali za kijamii. Hivyo tofauti hizo ndizo sababu za kuwepo kwa tafauti kati ya ushujaa wa shujaa wa motifu za safari na msako katika ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari. Aidha, utafiti wa Nyemsenda (ameshatajwa), ulibaini kuwa motifu za safari na msako wa shujaa katika ngano za jamii teuele zinalingana, kuingiliana na kuathiriana kama zilivyo pande mbili za sarafu moja. Utafiti huu kama zilivyo tafiti nyengine zilizotangulia utakuwa na manufaa katika kufikia lengo la utafiti wetu. Hasa ikizingatiwa kwamba utafiti huu umeshughulikia ngano za Zanzibar kama tutakavyofanya katika utafiti wetu. Tofauti kati ya utafiti wa Nyemsenda na utafiti wetu ni kwamba yeye alichunguza ushujaa wa shujaa wa motifu za safari na msako katika ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari, lakini sisi tumechunguza ngano za Zanzibar tu tukiwa na nia ya kuchunguza usihiri na namna unavyoibua dhamira katika ngano teule. Pia, utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhalisiajabu.

## 2.5 Dhana ya Dhamira

Ndungo na Wafula (1993) wanasema dhamira ni sehemu moja tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Hivyo dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi (msanii)

katika kazi ya fasihi. Waandishi hawa wamezigawa dhamira katika makundi mawili, nayo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Kwa mfano, unaweza kuwa na dhamira ya vita vya ukombozi, dhamira ya ujenzi wa jamii, dhamira ya utu bora, uvivu na ulanguzi.

Mawazo ya Ndungo na Wafula yametusaidia katika utafiti huu kubaini dhamira katika kazi zilizotafitiwa. Hii ni kutokana na kwamba, waandishi hao wametoa mifano ya dhamira zinazojitokeza katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mtafiti amechukua maelezo hayo kama ni msingi wa kutafiti dhamira katika ngano teule.

Naye Sengo (1999) anaelezea kuwa dhamira ni sehemu ya maudhui, na maudhui ni yale yasemwayo na maandishi ya kazi za fasihi. Dhamira ya mtunzi ya asili yaweza kuwa ni mgogoro wa ndoa, maandishi yakatoa dhamira kadhaa juu ya kugongana wenyewe kwa wenyewe viongozi wa juu wa serikali.

Sengo (ameshatajwa) anakubaliana na mawazo ya Ndungo na Wafula (ameshatajwa) kuhusiana na dhamira. Utafiti huu unakubaliana na mawazo hayo. Ingawa tukiri kwamba, ufafanuzi wa Sengo tumeona umeingia ndani zaidi kuhusiana na suala la dhamira, ukilinganisha na ule wa Ndungo na Wafula kwasababu Sengo anafafanua zaidi kwamba mgogoro ndio unaoibua dhamira katika kazi za fasihi. Kauli hii ya Sengo itasaidia utafiti huu kuchunguza migogoro iliyo na muelekeo wa kihalisiajabu iliyojitokeza katika kazi teule ili kubainisha dhamira zilizomo. Jambo hili limesaidia kukamilisha lengo na madhumuni ya utafiti huu.

Hivyo basi, suala la dhamira katika utafiti huu limekusudiwa kufafanuliwa kama msingi imara wa kazi ya fasihi ikiwemo ngano. Ili kuona jamii za Kizanzibar

inavyotumia dhamira zinazojitokeza katika ngano na mchango wake kwa jamii kisiasa kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni.

## 2.6 Pengo la Utafiti

Baada ya kupitia machapisho, majarida na tafiti mbalimbali zilizotangulia kuhusu mada ya utafiti huu, tumebaini kuwa kazi nyingi zilizofanywa zimeegemea katika vipengele vya fani na maudhui. Mapitio ya maandiko hayo yalidhihirisha kuwa, hakuna utafiti ambao umekwishafanyika kuhusu kuchunguza usihiri katika ngano za Zanzibar. Kwa kulibaini hilo, tumeona kuwa ipo haja ya kufanya utafiti wa kina ili kuchunguza usihiri na namna unavyotumika kuibua dhamira katika ngano za Zanzibar kwa kutumia Nadharia ya Uhalisiajabu (magic realism), Ili kuziba ombwe au mwanya ulioachwa na watafiti wengine.

## 2.7 Mkabala wa Kinadharia

Wafula na Njogu (2007) wanasema, nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum.

Nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo, yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani (Msokile,1993).

Kwa kuhitimisha tunaweza kusema kuwa, Nadharia ni jumla ya maelezo, taratibu, kanuni, misingi, mfumo uliorasmi, mwongozo na mpango unaotumiwa na mhakiki au mtafiti ili kumsaidia kuifanikisha kazi yake ya fasihi kwa cha kitaaluma.

Hivyo basi, Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu katika uchambuzi wa data. Nadharia hiyo imechaguliwa ili kuongoza utafiti huu tukiamini kwamba

imetuwezesha kufikia malengo ya utafiti huu. Nadharia hii imefanyiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:

### 2.7.1 Nadharia ya Uhalisiajabu

Vutagwa (2013) anasema kuwa Nadharia ya Uhalisiajabu ambayo pia hujulikana kama nadharia ya uhalisia mazingaombwe ni mojawapo ya nadharia za usasa leo ambazo hushikilia kwamba kazi ya fasihi hujengwa kutokana na mchangamano wa tajriba au uzoevu. Kulingana na Zamora na Faris (1995), kama anavyonukuliwa na Njogu na Wafula (2007), nadharia ya uhalisiajabu iliasisiwa mwaka wa 1925 na Mjerumani Franz Roh aliyekuwa mhakiki wa sanaa. Franz ndiye aliyetumia istilahi ya uhalisiajabu katika muktadha wa sanaa kuelekeza na kuonyesha jinsi ya kusawiri aina fulani ya uajabu kwa maana ya mazingaombwe yaliyomo kwenye uhalisi uliozoeleka na unaotokana na ujaribati.

Mbatiah (2002) anaeleza kuwa istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Akieleza kuhusu mazingaombwe hayo Cooper (1998) anadai kuwa hali za kushangaza na kuogofya, huwasilishwa kana kwamba ni hali za kawaida.

Wamitila (2004) anasema kuwa uhalisiajabu huhusishwa na Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa ulimwengu wa tatu. Sifa yake kuu ni kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabu ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa maana

inayoyafanya yaonekane ya kawaida. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii.

Wamitila (2008) anasema kuwa katika kazi za kiuhalisiajabu huwepo matukio ambayo ni vigumu kuyaelezea katika msingi wa uhalisi wa kawaida katika jamii. Njogu na Wafula (2007), wanasema kuwa Roh (1925), alitumia neno uhalisiajabu katika muktadha wa ulimwengu wa sanaa kueleza aina fulani maalum ya kudhihirisha usiri ulioko kwenye maisha ya kila siku bila kuupigia maswali yoyote uhalisia huo. Pamoja na hayo uhalisiajabu katika kazi ya sanaa hushughulika na kazi zinazoambatana na zisizoambatana na ujumi wa uhalisia.

Vutagwa (2013) anamnukuu Chanady (1985), katika Rio (1999), akisema kwamba uhalisiajabu unahusu matukio yasiyo ya kawaida, ya kimiujiza au chochote kilicho kinyume cha uhalisia wa kawaida. La muhimu zaidi ni kwamba matukio yanayotendeka katika uhalisiajabu hayawezi kujitenga na uhalisia. Matukio yasiyo ya kawaida, ya kimiujiza ni kinyume cha uhalisia wa kawaida.

Strecher (1999) anafafanua uhalisiajabu kama ‘kile kinachotendeka wakati ambapo ukweli wa ndani wa mandhari ya juu unapoingiliwa na kitu ambacho ni cha kiajabu sana kuaminika’. Mtazamo huu wa uhalisiajabu unatokana na usomi wa watu wa nchi za Magharibi kutohusishwa na imani ambayo ni mzizi wa uhalisiajabu ambao ni rahisi sana kueleweka na tamaduni za watu wasio wa Magharibi.

#### 2.7.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisiajabu

Wanjiru (2013), anawanukuu Danow (1995), Cooper (1998), Zamora (1995), (1993) na kubainisha mihimili ya uhalisiajabu kama ifuatayo**:**

i) Matokeo ya kiajabuajabu yanayoonekana ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya.

ii) Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.

iii) Mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa, maanake ni kuwa wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja.

iv) Wakati na mahali zina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Inamaanisha kwamba jambo linaweza kujirudia kwa sura nyingine mahali pengine.

v) Uhalisiajabu umefungamana na sanaajadi kama vile visasili. Visasili ni hadithi zinazoeleza asili ya watu na matukio fulani.

vi) Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Mtindo wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hutumika. Jambo hili hufanywa kwa kumpeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili.

vii) Mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa.

viii) Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu.

ix) Uhalisiajabu unapinga uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali mbalimbali kama vile uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na utamaduni huonekana zikiingiliana. Ni muhimu kutaja kwamba, katika utafiti wetu, si mihimili yote ambayo itatumika. Itakayotumika ni ile tu, itakayofaa zaidi kufafanua ngano tulizozichunguza ili kuweza kuangaza dhana ya uhalisiajabu. Miongoni mwa mihimili tuliyotumia ni wa kwanza, wapili, watano, wa saba, wa nane na watisa kama inavyojitokeza hapo juu.

Waliaula (2010) anasema kwamba wapinzani wa nadharia hii wanaikosoa kama uhalisia mazingaombwe unawezesha kutoa nuru au kusambaza kiza zaidi kwenye hali halisi ya maeneo ilikojikita fasihi ya aina hiyo. Wapo wanaotaja sana dosari ya mtindo huu wenye kuhusisha akili za wahusika wakuu walio na akili zisizokuwa timamu, mwingiliano matini uliopindukia na utambulisho wenye kuteteresha. Walibora 2012 anamuelezea Scott akipinga kwamba uhalisiajabu unafaulu pale ambapo uhalisia unapofeli, akisisitiza kwamba uhalisiamazingaombwe sambamba na uhalisia, umefungwa kwa minyororo ya lugha, na hivyo basi hauwezi kuondoa udhaifu wa lugha katika kuwakilisha hali halisi kikamilifu.

Pamoja na udhaifu uliotajwa hapo juu bado tumeona ipo haja ya kuichagua nadharia hii ili kukamilisha malengo ya utafiti huu. Hivyo basi, Nadharia ya Uhalisiajabu hutumika katika kuchunguza matukio yasiyoyakawaida kama vile uchawi na usihiri. Kwa mantiki hiyo tumeichagua Nadharia ya Uhalisiajabu ili kutuongoza katika

kuchunguza vipengele vya usihiri na namna vinavyoebua dhamira katika ngano za Zanzibar zilizokusanywa katika utafiti huu tuliamini kuwa imetuwezesha kufikia lengo la utafiti huu.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imekuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu kama sura nyenginezo. Kwa ufupi sura hii imejikita kujadili kwa kina vipengele muhimu ambavyo ni uti wa mgongo wa utafiti huu. Miongoni mwa yaliyojadiliwa ni pamoja na ufafanuzi wa istilahi mbalimbali. Sura hii imeelezea mapitio mbalimbali ya machapisho yaliyohusu dhana ya ngano, aina za ngano, usihiri na vipengele vyake pamoja na kazi ambazo ziliwahi kuchunguza ngano. Pia, sehemu hii imefafanua Nadharia ya Uhalisiajabu ambayo itaongoza utafiti huu na kujibu maswala yote la kwanza na la pili. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utanguliz

Sura hii inaelezea maana ya mbinu mbalimbali za utafiti ambazo zitasaidi kupatikana kwa data za msingi na data za upili ambazo zitachambuliwa katika sura ya nne. Miongoni mwa mambo yanayowasilishwa katika sura hii ni pamoja na mpango wa utafiti, eneo la utafiti, aina ya data zitakazokusanywa, mbinu za kukusanyia data, mbinu za uchambuzi wa data na zana za utafiti. Pia, sehemu hii inaeleza usahihi wa data, kuaminika kwa data na maadili ya utafiti.

## 3.1 Maana ya Mbinu za Utafiti

Kothari (2004) anaeleza mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu / taratibu zote stahiki zinazotumika wakati wa kufanya utafiti. Enon (1998) anafafanua mbinu za utafiti ni njia na taratibu zote zinazopaswa kufuatwa wakati wa ukusanyaji wa data (taarifa) kulingana na aina ya utafiti.

Mbinu za utafiti ni utaratibu maalum wa kufuatwa au kuchunguza kitu kwa kuzingatia hali ya umakini, malengo na mantiki nzuri kwa lengo la kufanikisha kazi husika vizuri ( University of Abuja (1992).

Kwa kumalizia tunaweza kusema kuwa, mbinu za utafiti ni jumla ya mpango na utaratibu maalum ambazo atazifuata mtafiti wakati anapofanya mchakato wa ukusanyaji wa data kulingana na mada husika ya utafiti wake.

### 3.2 Mpango wa Utafiti

Mpango wa utafiti hutoa picha kamili inayoonesha namna utafiti utakavyofanyika tangu kuanza mpaka unamalizika (Kothari, 2008). Mpango wa utafiti ndio unaoonesha kuwa utafiti husika utakuwa ni wa namna gani na data zilikusanywa vipi. Zipo aina nyingi za mpango wa utafiti lakini mtafiti alitumia uchunguzi kifani katika utafiti huu. Robson (2007) anaeleza kuwa uchunguzi kifani ni mbinu ya mpango wa utafiti ambao hutumika kwa mtafiti kuteua eneo au jambo maalumu ambalo yeye atalishughulikia katika utafiti wake. Katika utafiti huu tumeteua hadithi za ngano za Zanzibar ambazo, ndizo tulizozishughulikia. Yin (1994) anaeleza kuwa uchunguzi kifani ni mbinu ya utafiti ambayo humwezesha mtafiti kutumia muda mfupi na kisha kukusanya data nyingi za kutosha kukamilisha utafiti wake. Hii inatokana na ukweli kuwa mtafiti anakuwa na muda wa kutosha kulichunguza jambo moja na hivyo, kuwepo uwezekano wa kupata data za kutosha kukamilishia utafiti.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unafanyika kulingana na vile mtafiti anavyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali yake ya utafiti (Creswell, 2009).

Enon (1998) anaeleza, eneo la utafiti la kijografia ni pahala mahsusi ambapo mtafiti amekwenda au amekutumia katika kukusanya data za utafitiwake.

Kwa kuhitimsha, eneo la utafiti ni sehemu maalum ambayo mtafiti huiteua kwa ajili ya kufanya utafiti wake, pia eneo hilo ni lazima liweze kutoa data sahihi za kukamilisha malengo mahsusi ya utafiti na kujibu maswali ya utafiti.

Kwa mujibu wa mada ya utafiti, *Kuchunguza usihiri katika Ngano za Zanzibar,* mtafiti alikusanya data kupitia uwandani katika Mkoa wa Kaskazini Pemba Wilaya ya Micheweni ikiwemo Skuli ya Wingwi Sekondari, Micheweni Sekondari, Chwaka Tumbe Sekondari.na kijiji cha sizini.

Mtafiti amechaguwa eneo hili kwa sababu ni sehemu ambazo kwa kiasi kikubwa, kipera cha hadithi za ngano zilikuwa zikisimuliwa kwa njia ya ana kwa ana kati ya mtambaji na wasikilizaji nyakati za usiku. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa sababu mtafiti anaamini kuwa atapata ngano zinazohusu usihiri katika ngano za Zanzibar. Pia, atapata wanafunzi na walimu wa somo la fasihi ambao watashiriki katika mijadala ya vikundi kikamilifu. Hata hivyo data za utafiti wetu zimekusanywa uwandani ambako mtafiti aliamini atapata data za kutosha ambazo hatimae zilimuwezesha kujibu swali la kwanza na la pili la utafiti huu.

## 3.4 Uteuzi wa Watafitiwa

Watafitiwa ni jumla ya watu wote/vitu vyote ambao/ambavyo mtafiti amewakusudia kuwafanyia utafiti (Kombo na Tromp 2006; Enon 1998). Kwa hiyo, walengwa wa utafiti huu ni ngano za Zanzibar. Mtafiti alikusudia kuchunguza ngano hizo kwa sababu ameona kuwa bado hazijachunguzwa kwa kina katika kipengele cha usihiri. Pia, anaamini kuwa katika ngano za Zanzibar kuna mitindo ya usihiri hivyo ameona ipo haja ya kuchunguza hali hiyo kwa kina ili kuwekwa wazi tatizo hili kwa misingi ya kisayansi.

### 3.4.1 Sampuli na Mbinu za Usampulishaji

Sapata (2003) anaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu kutoka kundi lengwa ili litumike katika utafiti kama kiwakilishi cha

kundi lote linalotafitiwa. Zipo mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini sampuli ya utafifi huu itatumia mbinu mbili ambazo ni mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum na mbinu ya uteuzi rahisi.

#### 3.4.1.1 Usampulishaji

##### 3.4.1.1.1 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalum

Uteuzi wa sampuli kwa kutumia kigezo cha madhumuni maalumu ni uteuzi wa sampuli kwa kuzingatia sababu mahususi. Katika mbinu hii ya uteuzi wenye madhumuni maalum, sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo maalum ambavyo vitakuwa na uhusiano na maswali ya utafiti ili yaweze kujibiwa kwa urahisi na ukamilifu (Powell na Conway, 2004). Kombo na Tromp (2006) wanasema ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni raslimali anayoitegemea katika utafiti wake. Mbinu hii imempa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli itakayowezesha kujibu maswali ya utafiti. Mbinu ya uteuzi wenye madhumuni maalumu ilitumika kuteua ngano zenye mielekeo ya matumizi ya usihiri miongoni mwa ngano nyingi za Zanzibar. Ngano hizo ziliteuliwa kutokana na uelewa wa awali wa mtafiti kwamba, zipo ngano ambazo zina matukio ya usihiri.

Pia, mbinu hii ilitumika kuwateua watafitiwa wa utafiti huu, ambao wanazitambua ngano za Zanzibar. Lengo likiwa ni kupata watu ambao walizitamba ngano ambazo baadae zilitoa data za utafiti zilizojibu maswali ya utafiti huu.

**Mbinu ya Uteuzi Rahisi**

Kothari (2013) anaelezea mbinu ya uteuzi rahisi kuwa, ni mbinu inayotumika kuteua sampuli ya wahojiwa miongoni mwa kundi kubwa la wahojiwa wenye sifa sawa.

Sampuli katika mbinu hii huteuliwa kuwakilisha kundi kubwa bila kujali sifa ya mteuliwa kwani kila mmoja katika kundi hilo huwa na sifa sawa na mwingine. Katika utafiti huu mijadala ya vikundi ilifanywa kati ya walimu wa fasihi ya Kiswahili kutoka Kisiwa cha Pemba katika shule teule. Mtafiti aliamua kuteua sampuli kwa kuchukua orodha ya majina ya walimu na wanafunzi. Kwa kutumia orodha hiyo, mtafiti aliteua sampuli yake kwa kutumia nafasi kila baada ya mtu wa pili, mtafiti aliteua jina la mtu ambaye alilengwa kushiriki kama sampuli yake. Alifanya hivi kwa majina ya kike na ya kiume na hivyo kuwa na idadi ya walimu washiriki kumi, watano wanawake na watano wanaume. Pia alifanya hivyo kwa wanafunzi wa shule zilizo teuliwa kupata wanafunzi arobaini. Uteuzi wa makundi haya ulizingatia jinsia kwa sababu utafiti huu unaamini kuwa watu wa jinsi tofauti wanaweza kutoa maoni na mitazamo tofauti. Mtafiti aliwagawanya watu aliowateua katika makundi mawili. Kwa upande wa walimu kila kundi lilikuwa na watu watano. Kundi la kwanza lilifanya mjadala wa vikundi siku ya kwanza na kundi la pili litafanya mjadala wa vikundi siku ya pili. Kila kundi lilitumia saa moja na dakika thelathini.

**Jadueli na .3. 1Idadi ya Washiriki wa Utafiti**

| Na. | AINA | JINSIA | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | | KE | ME | |
| 1 | Walimu wa Shule za Sekondari | 5 | 5 | 10 |
| 2 | Wanafunzi wa Shule za Sekondari | 20 | 20 | 40 |
| 3 | Wazee wa kijiji cha Sizini | 02 | 02 | 04 |
| | JUMLA | | | 54 |

#### 3.4.1.2 Sampuli

Kwa mujibu wa Ponera, (2010) Sampuli ni sehemu ndogo ya jamii ya watafitiwa ambayo huteuliwa na mtafiti kwa kukusanya data. Kiwango cha ukubwa wa sampuli huamuliwa na mtafiti mwenyewe kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu hizo ni aina ya utafiti, asili ya mada ya utafiti pamoja na kiasi cha rasilimali alizonazo mtafiti ikiwa ni pamoja na muda na fedha za kuendeshea utafiti wake.

Hivyo basi, katika utafiti wetu sampuli iliteuliwa kwa kuchagua:

a) Walimu watano wanawake na watano wanaume, wanaofundisha somo la Fasihi ya Kiswahili katika skuli za Micheweni Sekondari, Wingwi Sekondari na Chwaka Tumbe Sekondari.
b) Wanafunzi ishirini Wanaume na ishirini wanawake kutoka skuli za Micheweni Sekondari, Wingwi Sekondari na Chwaka Tumbe Sekondari wakiendelea na mchakato wa kutambiwa na kutambiana ngano.
c) Wazee wanne wawili wanaume na wawili wanawake kutoka kijiji cha Sizini, Michweweni na Wingwi.

Kothari (2004:174) anaona kuwa ugawaji wa sampuli utaamuliwa na mtafiti kwa kuangalia mgawanyo wa makundi anayotegemea kuyatafiti, aina ya utafiti, aina ya sampuli na mengineyo. Sampuli hii imechaguliwa kulingana na aina ya utafiti ambao hasa umejikita kwa wale ambao wanaonekana kuwa na mwamko kuhusiana na ngano. Kwa hivyo kupitia sampuli lengwa hizo, data zilizopatikana kutoka kila kundi ziliongeza upeo wa kuelewa usihiri katika ngano za Zanzibar, na namna zinavyoebua dhamira.

## 3.5 Ukusanyaji wa Data

Enon (1998) anaeleza ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti, zoezi ambalo, humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika lengo lake la utafiti. Kothari (2004) anafafanua ukusanyaji data kuwa ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika malengo yake ya utafiti. Aidha, hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua ya ukusanayaji wa data. Kiudhati, katika utafiti wowote hususan utafiti wa kitaaluma ukusanyaji wa data huwa unajitokeza katika aina kuu mbili: Data za Awali (Msingi) na Data za Upili (Fuatizi)

## 3.6 Aina data za Data

### 3.3.1 Data za Awali (Msingi)

Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi (Kothari, 2004). Data hizi za msingi huwa hazijapata kukusanywa na mtafiti mwingine kwa lengo la utafiti kama huu ambao unakusudiwa kufanywa kwa mara ya kwanza. Data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kupitia uwandani ambako mtafiti aliamini atapata data za kutosha zilizoweza kulijibu swali la kwanza na kutoa msukumo wa swali la pili la utafiti huu. Miongoni mwa data awali ni vyakula vya kisihiri, wahusika wa kisihiri, ndoto za kisihiri, nuizo la kisihiri, mawasiliano ya kisihiri na mandhari ya kisihiri.

Kwa ujumla data za awali ni aina ya data halisi na thabiti ambazo mtafiti huzikusanya kwa mara ya kwanza kutoka katika eneo halisi alilolichagua kwa mujibu wa mada yake ya utafiti.

### 3.3.2 Data za Upili (Fuatizi)

Data za upili ni zile ambazo zimekwishakusanywa na watafiti wengine na kuchapishwa ama kuandikwa (Kothari, 2004). Katika utafiti huu mtafiti, alikusanya data za upili kutoka katika machapisho mbalimbali ya waandishi watangulizi kama vile; vitabu, majarida, tasnifu, na mtandao wa intaneti. Data hizi zimesaidia kuthibitisha data za msingi na kuandika sehemu ya pili ya utafiti huu ambayo inahusiana na kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, jambo ambalo limepelekea kufikia lengo la utafiti huu. Hivyo, ili kuzipata data hizi mtafiti alisoma machapisho mbalimbali katika maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA) na Maktaba kuu ya Zanzibar katika matawi yake ya Pemba ambapo mtafiti ndio rahisi kwake kwa vile ndio sehemu anayoishi.

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji wa data, ni njia anazochagua mtafiti kuzitumia kukusanya data kwa ajali ya utafiti wake (Kothari, 1990). Kitaaluma utafiti wowote ule, hauwezi kufanyika bila ya kuwepo mbinu maalum zitakazotumika kukusanya data. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi wa maandiko maktabani, mijadala ya vikundi na usomaji wa kina wa ngano teule.

### 3.6.1 Usomaji wa Nyaraka mbali mbali

Mbinu hii ilimuwezesha mtafiti kupata data za upili. Maktaba ni chanzo kizuri kwa ajili ya tafiti za kimaelezo kwa sababu mtafiti hufanya uchunguzi wa kina katika muktadha wa tatizo linalohusika. Kothari (2013) anaeleza kuwa katika maktaba mtafiti huweza kupata data nyingi, kwa urahisi bila ya gharama. Hivyo, mtafiti alitembelea sehemu mbalimbali zinazohifadhi kumbukumbu na nyaraka mbalimbali

kama vile Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, maktaba ya ,Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar na maktaba kuu ya Taifa. Katika matawi ya Pemba (yameshatajwa) mtafiti alisoma machapisho na maandiko mbalimbali, kama vile vitabu, makala, magazeti, tasnifu na tahakiki kwa ajili ya kupata taarifa kuhusu mada ya utafiti. Kwa kutumia mbinu hii, mtafiti alikusanya data za upili ambazo zilimuwezesha kuandika sura ya pili ya utafiti huu pamoja na kushadadia data za msingi katika sura ya nne ya utafiti huu.

### 3.6.2 Mijadala ya Vikundi

Mbinu hii ni mbinu ambayo mwongozo wa majadiliano yanafanywa baina ya kundi la watu kati ya sita hadi kumi ambao huwa na sifa na uzoefu unaofanana (Girbich, 1999). Jilala (2008) anasema kuwa majadiliano ya vikundi chini ya msimamizi mmoja yanaongozwa kiasi kwamba ingawa washiriki wanahamasishwa kuwa huru katika majadiliano lakini lazima kuwepo na mambo ya msingi yanayojadiliwa. Kwa hiyo, msimamizi wa majadiliano hujikita katika mambo mahususi. Mbinu hii ni bora kwa sababu inampa mtafiti taarifa nyingi, haraka na kwa muda mfupi. Vile vile ni mbinu muafaka katika kuibua imani, mawazo, maoni na mtazamo ndani ya jamii. Aidha, kwa kutumia mbinu hii wahojiwa katika makundi yao huweza kubadilishana uzoefu kuhusu jambo hilo. Kwa hiyo, sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba tuliamini kuwa ni mbinu ambayo iliweza kutupatia data nyingi kwa muda mfupi.

Kwa kutumia mbinu ya mijadala ya vikundi, tuliwagawa walimu wa Fasihi ya Kiswahili katika makundi ya walimu watano kwa kila kundi. Kila mwanakikundi alipewa vivuli vya hadithi ambazo zimeshachapwa kwa ajili ya kuzipitia kwa kina ili hatimae kuweza kutoa mawazo ya kile kinachotafitiwa. Kundi la kwanza walipewa

hadithi namba moja (1) hadi hadithi namba nane (8) na kundi la pili lilipewa hadithi namba tisa (9) hadi hadithi namba kumi na tano (13). Watafitiwa hawa walipewa fursa ya kuzitalii hadithi teule kwa muda wa siku moja. Kufanya hivyo kulimuezesha kila mtafitiwa kupata uwelewa wa kina wa kile kinacho tafitiwa. Baadae mjadala wa makundi hayo ulifanyika kwa siku mbili ambapo kila siku kulikuwa na mjadala wa kundi moja ambalo lilifanya mjadala kwa muda wa saa moja na dakika thelathini. Katika majadiliano hayo mtafiti amepata maoni, mitazamo na mielekeo juu ya matumizi ya usihiri katika ngano za Zanzibar na namna mbinu hizo zinavyotumika kuibua dhamira.

### 3.6.3 Usomaji Makini Maktabani

Usomaji makini ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo humpatia mtafiti data baada ya yeye, ama msaidizi wake, kusoma matini iliyoteuliwa kwa kina. Kutokana na kusoma huko ndipo pale akutanapo na sehemu inayohusu lengo lake la utafiti hulidondoa (Kothari, 2008). Mbinu hii ilitumika katika kukusanya data za msingi na vilevile, data za upili. Katika ukusanyaji wa data za msingi, kwanza mtafiti alizipitia hadithi 40 ambazo alizikusanya uwandani na kuchagua hadithi kumi na nne (12) ambazo aliamini zina matumizi ya vipengele vya usihiri. Baadae mtafiti aliandaa shajara ambalo lilikuwa na vichwa/mada zinazohusiana na malengo ya utafiti ama kile kilichokusudiwa kukusanywa. Baada ya hapo, alianza kusoma ngano teule na kila alipoona sentensi au aya katika ngano hizo inayohusu malengo ya utafiti, aliinukuu katika shajara na baadae kuifanyia uchambuzi.

### 3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013) ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Katika utafiti huu data zimechambuliwa kwa njia ya kimaelezo. John (2007) anaeleza kwamba uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo humruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma taarifa, kisha kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo wake na kadhalika. Mbinu hii pia huhusisha uchambuzi wa lugha iliyotumika. Kwa kufanya hivyo, mbinu hii huruhusu utolewaji wa maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa na mtafiti kwa namna ambayo inawezesha kujibu maswali ya utafiti husika. Uchambuzi wa data za utafiti huu utafanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Ambapo uchambuzi ulifanywa kwanza kwa lengo la kwanza na kumalizia lengo la pili la utafiti huu. Pia, data za utafiti huu zilichambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo ili kurahisisha uchambuzi wake na kuziweka wazi zaidi ili ziweze kufahamika na wasomi watakaonuwia kupitia utafiti huu.

Aronson (1992) anaeleza kwamba mkabala wa kidhamira hutumika kuichambua kazi ya fasihi kwa kuzingatia hatua kuu nne. Hatua ya kwanza ni ya kukusanya data, hatua ya pili ni kuoanisha mada na data husika (kubainisha data zinazohusaina na mada ya utafiti). Hatua ya tatu ni kupangilia data kwa namna ya kuoanisha dhamira kuu na ndogondogo. Hatua ya nne ni kuandaa hoja au nyanja zitakazozingatiwa katika uchambuzi wa dhamira baada ya kusoma ama kupitia machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti husika. Uchambuzi wa data katika utafiti huu utafanywa kwa kuzingatia hatua zote nne za uchambuzi wa data kama zilivyoainishwa hapo juu.

### 3.8 Vifaa vya Utafiti

Mulokozi (1983) anaeleza kuwa vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti, aghlabu baadhi ya vifaa hivyo huwa ni pamoja na shajara kalamu na karatasi, tepurikoda, kamera, simu na ngamizi. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia vifaaa vifuatavyo;

#### 3.8.1 Shajara

Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2013) shajara ni kitabu cha kuwekea kumbukumbu za kila siku. Zana hii ilitumika kuhifadhi kumbukumbu za data zilizopatikana katika utafiti huu. Kwa kutumia zana hii, mtafiti aliandika katika shajara taarifa mbalimbali zilizopatikana wakati wa utafiti.

#### 3.8.2 Kompyuta

Kompyuta ni zana ambayo mtafiti ataitumia tangu mwanzo hadi mwisho wa utafiti wake. Kompyuta ni mashine ya kielektroniki inayotumika kuhifadhi na kusarifu taarifa zinazoingizwa ndani yake (TUKI, 2013). Mtafiti alitumia zana hii kuchapa kazi yake ya utafiti, kuhifadhi data, kutafuta machapisho na maandiko mbalimbali yanayohusu utafiti huu yanayopatikana katika tovuti na wavuti mbalimbali.

### 3.9 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti

#### 3.9.1 Usahihi wa Data

Usahihi wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika (Cohen na Wenzake, 2000). Usahihi wa data katika utafiti wetu unahakikishwa kwa kutumia mbinu tatu na zana mchanganyiko ambazo ni mbinu za maktaba, mahojiano ya vikundi na uchambuzi wa nyaraka. Katika

uchambuzi wa data, mkabala wa kidhamira na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ndizo zitazotumika katika kukusanyia data. Usahihi wa mbinu hizi unatokana na ukweli kwamba upungufu wa kila moja hukamilishwa na ubora wa mbinu nyingine.Vilevile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zitazotumika katika utafiti huu zitajadiliwa katika mjadala baina ya mtafiti na msimamizi wake.

### 3.9.2 Kuaminika kwa Data

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yaleyale ya utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zilezile (Kothari, 2008). Kuaminika kwa data hujitokeza pale ambapo kuna kuwa na uhusiano ama ulingano katika taarifa zilizotolewa na watu walewale kwa muda tofauti (Furlong na Lovelace, 2000). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kunahakikishwa kwa kutumia mbinu mchanganyiko za kukusanyia data na nadharia iliyotumika katika utafiti huu.

### 3.9.3 Maadili ya Utafiti

Miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa mtafiti kuvizingatia ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti pamoja na kutunza siri za watafitiwa. Hivyo, katika utafiti huu, maadili ya utafiti yatazingatiwa kabla na baada ya kukusanya data. Kwa kuwa utafiti wetu utakuwa ni wa uwandani na maktabani, tutahakikisha kuwa madondoo kutoka katika ngano na data kutoka kwa mijadala ya vikundi yanafanywa kwa usahihi na kuchambuliwa kifasihi kwa kuongozwa na Nadharia ya Uhalisiajabu.

## 3.10 Hitimisho

Sehemu hii imewasilisha mbinu za utafiti ambazo zitatumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti wetu. Mbinu hizo zinajumuisha zile za nyanjani na Maktabani. Mbinu za Maktaba zinahusisha ukusanyaji wa data kwa kusoma kwa makini kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti huu ili kupata data za kukamilishia data za msingi. Vilevile, data za msingi zilikusanywa kwa kupitia kwa makini ngano teule ili kupata data zinazoonesha usihiri na namna unavyoibua dhamira. Kwa upande mwingine, data za msingi zilikusanywa kwa kufanya majadiliano ya vikundi. Pia, sehemu hii imeeleza zana zilizotumika katika utafiti huu. Mwisho tumewasilisha vipengele vya usahihi wa data, kuaminika, maadili ya utafiti na hitimisho.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data. Katika sura hii, data zilizopatikana uwandani na maktabani, zimeelezwa zilifanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Ni katika sura hii ambapo vipengele vya usihiri na namna vinavyobeba dhamira katika ngano teule zimefanyiwa uchambuzi. Uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizomo kwenye tasnifu hii umezingatia mada, malengo na maswali ya utafiti huu.

## 4.1 Ngano Teule

Katika utafiti huu jumla ya ngano 12 zimeteuliwa kutoka katika ngano 40 ambazo mtafiti alizikusanya na baadae kuzichagua ngano zenye sifa za usihiri. Uchambuzi wa data zilizomo kwenye tasnifu hii umezingatia vipengele vya usihiri na namna vipengele hivyo vinavyotumika kuibua dhamira. Mtafiti aliziteua ngano hizi huku akiamini kwamba ngano teule zilifanikisha malengo ya utafiti huu na kujibu maswali ya utafiti. Majina ya ngano zilizoteuliwa ni pamoja na*Zimwi naMkia*, *Kijoka*, *Kilichomponza Nyoka Akakosa Maguu*, *Yamuimui*, *Kisiki*, *Mazimwi Wala Watu,Tatu na Saida, Miza, Babu Dii,Zena, Rajabu, Abanawasi na Sufuria, Tango* na *Mbwa Mahoka.*

## 4.2 Vipengele vya Usihiri katika Ngano za Zanzibar

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lililenga kutafiti matumizi ya vipengele vya usihiri kwa kadri vilivyojitokeza katika ngano za Zanzibar. Hivyo data

zimekusanywa katika ngano teule na zimeonesha kuwa ngano za Zanzibar zimekuwa zikitumia vipengele vya usihiri katika miktadha mbalimbali. Katika mijadala ya vikundi watafitiwa walivitaja vipengele hivyo ambavyo ni pamoja na matumizi ya wahusika wa kisihiri, kubadilika kutoka umbile moja na jengine, matukio ya kihalisiajabu, manuizo ya kisihiri, ndoto za kisihiri, vyakula vya kisihiri, mawasiliano ya kisihiri, safari za kisihiri na mandhari ya kisihiri. Vipengele hivyo vimefanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Matumizi ya Wahusika wa Kisihiri

#### 4.2.1.1 Wahusika wanyama

Matumizi ya wahusika wanyama ambao wanatenda matukio ya kisihiri ni aina ya wahusika wenye sifa za usihiri katika hadithi simulizi za Zanzibar. Wanyama hawa huwana sifa ya kutenda matendo ambayo huwa yanatendwa na binadamu na hata mara nyengine kumshinda binadamu katika matendo mbali mbali yanayohusu uwezo wa kukiuka ukawaida wa uhalisia. Katika hadithi namba tisa (9), hadithi inayoitwa *Yamuimui* tunaona namna watoto waliokuwa na wivu walivyomchukua Yamuimui na kwenda naye msituni ili kumuua kwa sababu ya wivu na choyo walichokuwanacho watoto hao. Mwisho Mzee mmoja pale kijijini alijigeuza mbwa na kumfuata mama yake Yamuimui huku akimwambia kuhusu habari ya kile kilichotokea dhidi ya Yamuimui. Mbwa huyo alikuwa akisema hivi:

> "Yamuimui….Yamuimui
> Kapachikwa panda ya mti kulee kulee
> Watu wende nami nende nikasikize kilio
> Yamuimui kauawa."

Katika tukio hilo tunaona namna kitendo cha mzee huyo cha kujigeuza mbwa kisivyokuwa cha kawaida. Tukio hili linaakisi mojakwamoja na nadharia ya

Uhalisiajabu. Uhalisiajabu umejitokeza wazi wazi katika tukio hili, pale mbwa alipozungumza na watu kwa lugha ya kibinadamu. Matukio haya ndiyo anayoyaeleza Wamitila (2013) kwamba matukio ya uhalisiajabu hukiuka matukio ya kihalisi katika kazi za fasihi. Tukio la kumchukua kijana na kumpeleka mwituni kwa lengo la kumuuwa limetumika kusawiri namna wivu na choyo unavyosababisha hata mauaji katika maisha ya kila siku ya wanajamii.

**Kisiki kuongea**

Katika hadithi namba 12, hadithi ya jini Kisiki. Katika hadithi hiyo kumetumiwa muhusika wa kisihiri ambapo kisiki alichokuwa amejikwaa Bi Asha kilikuwa ni jini amejigeuza kijiti hicho. Kutokana na hali hii kijiti kilikumbusha ahadi aliyoiweka Bi Asha ya kumpelekea mtoto iwapo atabahatika kujifungua mtoto. Hatimae kisiki hicho kinafunga ndoa na Salma, mtoto wa Bi. Asha. Kiujumla tukio hilo katika hali ya kawaida hali wezekani bali msanii alijaribu kutumia mbinu ya kiutunzi ya kuingiza usihiri ili kazi yake iwe na mvuto kwa wasikilizaji wake.

Katika hadithi namba tatu (3) iliyopewa jina la hadithi ya Rajabu pia kuna mhusika wa kisihiri. Tunaelezwa kuwa Rajabu alipopotea akiwa baharini alichukuliwa na mawimbi hadi kwenye jumba kubwa la kifahari huko baharini. Wakati Rajabu akiwa amekaa kwenye kiti alimuona ndege kwa mbali akielekea pale alipo. Alipokaribia alipo Rajabu ndege alijigeuza kiumbe kikubwa cha ajabu na cha kutisha. Baadae alijigeuza kuwa jini.

Katika hadithi namba kumi na tatu (13), ilyopewa jina la hadithi ya Kilichomponza Nyoka Kukosa Miguu tunaoneshwa wahusika wa kisihiri kutokana na jongoo

kuelezwa kuwa hakuwa na miguu, lakini kwa sababu ya wanyama wengine kukawia kuwasili katika kikao cha kugawanya miguu, jongoo aliichukuwa miguu yote iliyobakia na kujibandika nao yeye pake yake. Kwa sababu hiyo wanyama wengine akiwemo nyoka walikosa miguu. Hivyo usihiri unaojitoeza hapa ni ule wa jongoo kujibandika miguu mwenyewe, jambo ambalo katika hali ya kawaida haiwezekani kiumbe kujiongezea viungo mwenyewe.

Vile vile, katika hadithi ya 7 ya Tatu na Saida tunaona namna Saida alivyosawiriwa kama ni mhusika wa kisihiri. Tunalezwa kuwa Saida aligeuka ndege baada ya kutogwa sindano ambayo ilikuwa na usihiri. Tatu alimchoma Saida sindano na hatimae akageuka ndege papo hapo. Tukio hili mtafiti anasema kuwa ni la kisihiri kwa sababu linakiuka uhalisia wa kijamii na hivyo kuwa ni tukio la kinjozi.

Kwa ujumla tunaporejelea nadharia ya Uhalisiajabu tunaona kuwa wahusika ambao mtafiti amewajadili katika sehemu hii wanasifa za kiuhalisiajabu kutokana na kusawiriwa wakiwa wanaibua maajabu kwa msikilizaji na hatimae kuwa ni wahusika wa kisihiri ambao matendo yao yanashabihiana na uchawi. Maajabu haya yanabakia kuwa ya ushabihi kweli ambayo yanakiuka uhalisia wa maisha ya kibinadamu kutokana na kubeba kile baadhi ya watu wanachokiita nguvu za kiza. Katika jamii nyingi za Afrika imani za kisihiri zimekuwa zikiaminiwa na baadhi ya wanajamii. Watu wengine huenda kwa waganga na kuchukua dua ama vitu ambavyo huaminika kuwa na nguvu za kisihiri kama viungo vya wanadamu, wanyama na hata miti ili kufanikisha malengo yao kama vile ya kujipatia mali ama kuvunja kesi zilizowakabili huko mahakamani.

### 4.2.2 Kubadilika Kutoka Umbile Moja kwenda Jingine

Katika hadithi namba mbili (2), yenye jina la hadithi ya Zena tunaelezwa kuwa Zena alikuwa akiteswa na mama yake wa kambo. Siku moja alitakiwa na mama yake wa kambo akafuwe na kukosha vyombo katika mto ambao watu hawaendi huko kwa sababu ya kuhofia kuliwa na majini. Hata hivyo alilazimika kutii amri hiyo na aliamua kwenda. Alipofika katika mto huo alikutana na majini yaliyotamani kumla lakini alinusurika kwa kuonewa huruma na majini hao baada ya kueleza mkasa wa namna anavyotendewa uonevu na mama wa kambo. Tukio hili linasimuliwa hivi:

> "Chukua nguo na vyombo uende ukaoshe mtoni. Na mto ule ndio ambao tunaishi sisi. Kwa hivyo ukimaliza kufua nenda katikati ya mto uchukue maji ujimwagie mwili mzima na chochote ambacho utakiona usije ukashangaa ni sisi ambao tutafanya hivyo. Basi alivyomaliza akachukua maji na akajimwagia papo hapo akageuka na kuwa Mwarabu na kujiona yuko msafi tofauti na alivyokuwa."

Kutokana na hali hii tunaelezwa namna majini wanavyoibua tukio la kisihiri pale walipomuamuru Zena aende kwenye mto na ajimwagie maji na asijali kwa lile litakalotokea. Alipofanya hivyo Zena alibadilika rangi na kugeuka akawa Muarabu. Tukio hili ni la uhalisiajabu kwani kitendo cha kugeuka rangi si jambo la kawaida kwa mwanadamu. Tukio hili linauhusiano na nadharia ya uhalisiajabu ambapo moja ya msingi wa nadharia hii nikwamba matukio ya kiajabuajabu katika kazi za fasihi yanayoonekana ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya.

Hadithi nyengine iliyotumia usihiri kwa mbinu ya kujibadilisha rangi ni hadithi namba tatu (3) ijulikanayo kuwa ni hadithi ya Rajabu. Hadithi hii inasimulia maisha ya Shaaban na Rajabu na wazazi wao. Shaaban na Rajabu waliishi na wazazi wao hadi pale walipofariki wazazi wao wote wawili wakati huo Shaaban akiwa na umri wa miaka minane (8). Watoto walibaki pekeyao na sasa majukumu ya kuishghulikia

familia hiyo yalibakia mikononi mwa Rajabu. Rajabu alijishughulisha na kazi kadhaa ili aweze kuyakimu maisha.

Rajabu hatimae aliamua kufanya kazi ya uvuvi. Siku moja alitoka usiku peke yake. Wakati alipokuwa baharini upepo ulivuma kwa kasi na hatiame ukamchukua Rajabu hadi kwenye bahari kuu ambako alikuta nyumba kubwa ya kifahari yenye kila aina ya mali. Alipoingia ndani hakuona mtu ila alikuta pesa, dhahabu, vyakula vya kila aina, almasi na juu ya roshani palikuwa na kiti cha dhahabu ambacho alikwenda na kukikalia. Baadae kwa mbali aliona ndege mdogo anakuja na alipofika karibu na Rajabu alijigeuza umbile kubwa kuliko nyumba. Mara alijigeuza mtu mrefu sana asiekuwa na mwisho, baadae akajigeuza moto mkubwa unaowaka. Mwisho akajigeuza binadaamu na kuenda hadi alipo Rajabu na kumtolea salamu. Rajabu alipokea salamu bila hofu. Katika hadithi hii tunasimuliwa hivi:

> "…Baada ya muda si mrefu Rajabu alitupa jicho mbele akaona kwa mbali ndege mdogo anakuja. Akasema; "Ah! Ndege yule anatokea wapi usiku huu au amechelewa kurudi? Ndege akaja. Akaja. Akaja hata akafika karibu ya nyumba. Akajigeuza akawa kitu kikubwa kuliko nyumba. Rajabu alikaa kimya katulia juu ya kiti cha enzi anatazama miujiza tu, mara akajigeuza mtu mrefu sana asiyekuwa na mwisho, mara akajigeuza moto mkubwa unaowaka, hata mwisho akajigeuza umbo la binadamu akaingia ndani ya nyumba akamsogelea Rajabu kasha akamtolea salamu. Huyu ni jini. Rajabu alikuwa ametulia kabisa bila ya kupaparika moyo wake, akaitikia salamu kama ilivyo kawaida ya watu wanapokutana…"

Matukio yaliyooneshwa na ndege huyu ni matukio ya kisihiri kutokana na kuwa na uwezo wa kujibadilisha kutoka umbo moja na umbo jengine ambapo hatimae hutuibulia uhalisiajabu. Ndege huyu alikuwa ni jini aliyeakijigeuza kutoka hali moja na nyengine. Mutiso (2012), anasema kuwa viumbe wenye sifa ya kujigeuza ni aina ya mashetani, jini au pepo mbaya alae watu. Pepo huyu anaweza kumfanyia mtu

sihiri ama mazingaombwe na kawaida huwa ni mchawi wa kiume. Kwa kawaida majini ya namna hii huweza kuwa na maumbo mbali mbali ya wanyama, wanadamu na majitu. Viumbe hao hupenda kuishi makaburini na mahali mwengine kulikojitenga. Hula maiti au kitu chengine chochote wanachokutana nacho.

Katika hadithi namba moja (1), yenye jina la Hadithi ya Zimwi kuna matumizi ya usihiri unaojidhihirisha kutokana na mabadiliko ya maumbile ya mume wake Miza. Tunasimuliwa kwamba Miza alikuwa msichana aliyebahatika kuchumbiwa na wanaume wengi hata hivyo hakuwataka. Mwisho, alichumbiwa na zimwi bila kujua alikubali na wakafunga ndoa. Baada ya kufunga ndoa Miza na mume wake walikwenda kuhamia kwenye nyumba ambayo ilikuwa imejitenga msituni. Tunaelezwa kuwa Mboje ambaye ni mdogo wake Miza aligundua kwamba shemegi yake alikuwa ni zimwi mwenye mkia na anayejibadilisha kutoka umbile la zimwi hadi la binadamu kwa nia ya kuficha asitambuliwe kwamba ni zimwi. Mkia huo ulikuwa unawaka moto lakini wakati pale anapo hodisha kwa shemegi yake alikuwa akisema maneno haya "*muamu moto shima shima nimuitikie muamu*" papo hapo alikuwa anageuka kuwa umbile la kibinadamu. Tunasimuliwa hivi:

> "… Siku moja Miza aliamua kupeleka chakula mwenyewe ili kugunduwa mumewe ni zimwi au ndugu yake anasema uongo. Aliondoka na kwenda na alipofika alisita alipoona mumewe mkia unapiga piga na baadae akamuona mume wake akampa chakula na kuondoka. Alipofika nyumbani kwake alimwambia mdogo wake kwamba yale unayosema ni kweli."

Kutokana na matendo hayo tunaweza kusema kuwa matendo ya kisihiri yametumika kwa kiasi kikubwa katika baadhi ya ngano za Zanzibar.

Katika hadithi ya Mbwa Mahoka tunasimuliwa namna mkuu wa mazimwi anavyojigeuza moshi mrefu wakati alipozungukwa na mbwa. Kutokana na kujigeuza mazimwi wenzake walishangaa sana na kuduwaa. Kwa tukio hili Haji alipata nafasi ya kutoroka katika mikono ya mazimwi na hivyo kuokoa maisha yake.

Tunaporejelea nadharia ya Uhalisiajabu, mtafiti amebaini kuwa matendo ya wahusika kubadilika kutoka umbo moja na jengine yanalandana na nadharia ya Uhalisiajabu. Moja ya msingi wa nadharia hii ni ule unaoelezwa na Wanjiru (2013), kwamba katika kazi za Uhalisiajabu kunakuwa na matukio ya kiajabu ambayo huonekana kuwa ya kawaida pia huwa na hali za kushangaza na kuduwaza, kushangaza na kuogofya. Kwa mtazamo huu ngano za Zanzibar husimulia matukio ya kubadilika kwa wahusika kutoka umbo moja na jengine kama ujumi wa kawaida. Hata hivyo matukio haya huwa yanashangaza na hata kujenga hofu miongoni mwa hadhira hasa watoto wadogo.

### 4.2.3 Matukio ya Kihalisiajabu

Data zilizokusanywa katika hadithi simulizi teule za Zanzibar zinaonesha kwamba hadithi hizi zinasawiri matukio kadhaa yenye kubeba usihiri. Matukio hayo hukiuka kaida ya matukio halisi ya kiulimwengu. Mathalani, katika hadithi ya nne (4), yenye kichwa cha habari Hadithi ya Kijoka tunasimuliwa namna nyoka anavyodai afanyiwe tohara. Tunaelezwa kwamba nyoka huyo alikuwa akijigeuza kuwa binaadamu wakawaida, hivyo alifunga ndoa na binadamu jambo ambalo hutuibulia maswali mengi na hata kutoaminika katika uhalisia wa maisha ya kila siku.

Pia, nyoka huyo wakati akiwa mdogo anadai kufanyiwa tohara. Wakati alipokwenda mfanyaji tohara ghafla anajigeuza bianadam. Hatimae anafanyiwa tohara jambo ambalo linaibua maajabu kwa mnyama kufanyiwa tendo hili la mila na desturi. Tunavyojua binadamu ndio hufanyiwa tohara na si wanyama. Matukio kama haya yanasifa za kinjozi. Kama asemavyo Salim (2015), kwamba katika hadithi za kihalisiajabu wanyama hutenda matendo ambayo hufanywa na binadamu. Kwa mantiki hiyo, ni wazi kuwa matukio ya kisihiri au uhalisiajabu yamejitokeza katika ngano za  Zanzibar.

Vilevile, katika hadithi namba mbili (2) yenye kicha cha habari *Hadithi ya Zena*, kunaelezwa tukio la Zena kujimwagia maji na kubadilika kimaumbile. Katika hadithi hii maji yametumika yakiwa na nguvu za kisihiri ambapo yana uwezo wa kubadilisha mtu maumbile. Maji hayo yalimfanya Miza awe Muarabu. Tukio hili ni la kiuhalisiajabu usawiri wa maji kuwa na nguvu za kisihiri unashabihiana na ule anaoutumia Mbogo (2008), katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng`wanamalundi* ambapo Nyamiti anakuwa kizuu baada ya kujipaka mafuta yenye nguvu za kisihiri katika nywele zake pia kufufuliwa pial. Katika hadithi ya Zena tukio hili linasimuliwa hivi:

> "…mazimwi yakamsikiliza mtoto yule yale anayoyasema na wakamuonea huruma sana na wakamwambia "usiwe na hofu sisi tutakusaidia. Chukua vyombo na nguo uende ukaoshe mtoni na mto ule ndio amabao tunaishi sisi. Kwa hivyo ukimaliza kufua nenda kati kati yamto. Hapo tena chukua maji ujimwagie mwili mzima na chochote ambacho utakiona usijeukashangaa. Ni sisi ambao tutakufanya hivyo." Basi alipomaliza akachukua maji na akajimwagia, papo hapo akageuka na kuwa Mtu safi na kujiona yuko msafi tofauti na alivyokuwa halafu akenda zake. Alipofika kwao mama yake akamshangaa sana na Zainabu aliporudi Skuli akamuona Zena amebadilika akamwambia mama yake "nami nataka kwenda mtoni ili nami nikawe Mwarabu!" Mama yake akamwambia "sawa."

> Basi siku ilipofika Zainabu akaenda mtoni alipofika mazimwi hawakumuuliza bali walianza kumla na kumbakisha mifupa ndani ya maji…”.

Katika hadithi namba tatu (3), yenye kichwa cha hadithi ya Rajabu kuna matukio kadhaa ya kisihiri. Tunaelezwa tukio la Rajabu alivyoweza kumtisha jini katika nyumba kwa kumwambia kuwa yeye ni Ziraili aliyekuja kutoa roho yake. Kutokana na maneno haya jini alikubali kutoa fidia ili asiuawe. Rajabu anamuamuru jini huyo ahame, aache mali yote iliyomo katika nyumba yake na asithubutu kutoa siri hiyo. Mjadala huu ulikuwa hivi:

> “Mimi nipo hapa leo siku ya tatu nakusubiri urudi tu nifanye wajibu wangu. Sasa umeshafika kaa na utulie nitoe roho” Rajabu alijibu. Jini aliuliza “Bwana! Roho yangu haina sadaka badala yake? “Sadaka badala ya roho yako ipo je utaiweza?
>
> Jini alikubali “Naam nitaiweza bila ya wasiwasi!” Sadaka ya roho yako ni kuwa kwanza uihame nyumba hii kabisa wala usirudi tena maisha yako, pili habari hii usimwambie mtu katika uhai wako siku utakayomwambia mtu hapo hapo nitatokea na nitakutoa roho. Jini aliaga akakimbia”

Tukio hili ni la kisihiri kwa sababu maneno ya Rajabu yamekuwa na nguvu za kumshinda jini kutambua kuwa huo ulikuwa ni ujanja tu.

Katika hadithi namba (11) yenye kichwa cha habari *hadithi ya Tango* tunasimuliwa namna vijana walvyoiba tango ambalo lilikuwa tayari limetegwa kisihiri. Baada ya tango hilo kuliwa kila aliyelila alisikia sauti ya tango likizungumza likiwa ndani ya tumbo. Hali hii iliibua wasiwasi mkubwa miongoni mwa vijana hao. Tukio hili ni la maajabu ambalo linasadifu na kuakisi nadharia ya uhalisiajabu katika maisha ya kila siku.

Pia, katika hadithi hiyo hiyo namba tatu (3), kuna tukio la Rajabu ambalo linasawiriwa kisihiri. Rajabu anaonekana akiwa na nguvu za kisihiri zinazoibua uhalisiajabu kutokana na uwezo wa kuogopewa na majini na hatimae kupoteza maisha. Tunaelezwa kuwa Shaaban na Rajabu walikuwa kwenye mgogoro ambapo Shaaban alitaka kupelekwa ilikopatikana mali ili akachukue yake na hatimae asiwe tegemezi. Mwanzo Rajabu alikataa wazo hilo. Hata hivyo baada ya ubishani mkubwa kati ya Shaaban na Rajabu walikubaliana kwenda kwenye ile nyumba ya jini. Walipofika karibu ya ile nyumba walisikia sauti ambazo zilimfanya Shaaban kuogopa na hatimae alishauri warejee lakini Rajabu aliamua kuingia ndani ya ile nymba. Rajabu aligundua kwamba ndani mulikuwa na sherehe na tafrija kubwa ya majini. Rajabu alijificha. Hatimae Rajabu alimsikia jini akisimulia mkasa wote wa vitisho vilivyomtokea kwa Rajabu. Papo hapo Rajabu alijitokeza mbele ya majini na wote wakafariki. Tunaelezwa tukio hili hivi:

> "Ghafla Rajabu alijitokeza nyuma ya sinia akaenda mbele ya majini akasema "haya tayari mimi nimeshafika kukutoa roho kwa sababu miadi tuliyopeana hukuitimiza." Kwa hofu kubwa majini wote wakaanguka chini wakafa. Rajabu alipowaona wote wameshakufa akaanza tena kukusanya na kufunga fedha, dhahabu, almasi, Michele na nguo akateremka na mizigo yake mpaka chini. Wakati huu woga ulikwisha mpungua Shaaban wakasaidiana kupakia mali yao baadae wakatweka."

Tukio jengine la kisihiri linajitokeza katika hadithi ya kumi (10), yenye kichwa cha hadithi ya *Babu Dii.* Katika hadithi hiyo tunaelezwa namna Babu Dii, kijana kutoka katika familia ya kimaskini anavyolazimika kumramba tongo bibi kizee ili baadae aweze kumsaidia. Tukio hili linasimuliwa hivi:

> "…akasema lazima nifike kule kunakofuka moshi. Akenda, akenda, akenda hata hukoo akafika akaona kijibanda kidogo, mara kikatoka kibibi kikongwe, kikamuuliza "mjukuu wangu unakwenda wapi? Huku hakuji mtu ispokuwa awe na hisia miongoni mwetu." Babu Dii

> akamwambia “ nimekuja kutafuta kazi” akamwambia “kama unataka kazi njoo nikupe” Babu Dii akenda akachukuliwa hadi kibandani na yule bibi akamwambia kama unataka kazi kwanza nirambe tongo zangu zote mpaka zimalize, niweze kuona vizuri. Babu Dii akamramba tongo mpaka zikamaliza na bibi akawa anaona vizuri. Baada ya kumaliza Babu Dii alipewa pesa na mapande matatu ya dhahabu akayauze apate pesa zaidi ili aanze biashara yake mwenyewe..”

Katika hadithi hii kama tunavyoona hapo juu tunaoneshwa tukio la kisihiri la mtu kumramba tongo mtu mwengine ili hatimae aweze kuona. Tukio hili linasawiriwa kiuhalisiajabu katika jamii. Kama asemayo Njogu na Wafula (2007) kwamba matukio yasiyo ya kawaida katika kazi za uhalisiajabu hutumika ili yasawiriwe kiuhalisia. Katika tukio hili msanii anamtumia Bibi Kizee kuashiria nchi tajiri duniani na Babu Dii ni wananchi wa dunia ya tatu ambao wanaziendea nchi tajiri ili kupata misaada. Hata hivyo ili kupewa misaada hiyo nchi changa hulazimika kukubali mashariti ya nchi hizo. Mashrti ambayo hayana mustakabali mzuri na yanazidunisha nchi maskini.

Katika hadithi namba kumi na tatu (12), yenye kichwa cha hadithi ya *Kilichomponza Nyoka Akakosa Miguu* tunaelezwa tukio la kisihiri kutokana na kisa cha nyoka kukosa miguu. Tunaelezwa kuwa siku moja wanyama walitakiwa ifikapo saa mbili kamili wawe wamefika katika mkutano ili kugawana miguu. Siku ilipofika nyoka hakuamka mapema kutokana na uvivu aliokuwanao hivyo alichelewa hadi saa nne ambapo jongoo kutokana na kuamini kwamba kwa wakati huu hakuna mnyama mwengine atayetokea aliamua kujibandika yeye miguu yote iliyobakia. Baadae alipokwenda nyoka alikutia miguu hakuna tena hata mmoja kwa sababu hiyo alibakia akiwa hana miguu hadi leo.

Katika hadithi hii tunaona namna tunavyoibuliwa tukio la kisihiri la wanyama kujibandika miguu kama kisasili cha maumbile yao. Tukio hili lina misingi ya kisasili ambacho kinaibua maajabu. Kama asemavyo Wamitila (2013) kwamba uhalisiajabu unaibuliwa na matukio ambayo ni ya maajabu. Hivyo tukio la wanyama kugawanya miguu na jongoo kujibandika miguu yote ilyobakia ni usihiri. Katika hadithi hii tunasawiriwa namna uvivu na dharau unavyomfanya mtu akose maswala muhimu katika maisha yake ya kila siku.

### 4.2.4 Manuizo ya Kisihiri

Katika hadithi namba (7) inayozungumzia habari ya *Tatu na Saida*, tunasimuliwa kisa cha wasichana wawili wajulikanao kwa majina ya Tatu na Saida. Wasichana hawa walikuwa ni ndugu wa baba mmoja. Inaelezwa kwamba Saida alizaliwa kwa njia ya maajabu sana. Kwani alizaliwa kupitia kwenye goti. Baada tu ya kuzaliwa mama yake alifariki. Sasa akalelewa na mama yake wa kambo anayeitwa Mwajuma. Mwajuma alikuwa na mtoto wake aliyeitwa Tatu. Mwajuma alimpenda sana Tatu na alikuwa akimchukia Saida bila ya sababu ya msingi. Watoto hawa walikuwa wanalijua hilo. Ingawa hawakuwa na la kufanya. Siku moja mtoto wa Mfalme alitaka mke. Alipofika nyumbani kwa akina Mwajuma, bi Mwajuma aliamua kumficha Saida na kumdhihirishaTatu.Hata hivyo nyota ya kuolewa na mtoto wa mfalme haikumuangukia Tatu. Mtoto wa mfalme aliomba atolewe msichana mwengine aliomo ndani. Katika hatua za mwanzo Mwajuma aliendelea kuficha ukweli.Hata hivyo baadae Saida alitolewa na ndipo alipopata bahati ya kupendwa na mtoto wa mfalme. Hali hii Mwajuma hakuridhika nayo. Alipendelea mtoto wa mfalme amuowe mwanawe Tatu, lakini Waswahili husema “mapenzi ni majani huota

popote”. Hivyo mapenzi ya mtoto wa mfalme yaliangukia kwa Saida.Siku moja Mwajuma alienda kwa mganga na kutaka Saida aachwe na nafasi hiyo ichukuliwe na Tatu. Mganga alimpa Mwajuma sindano, na kumtaka amtoge nazo Saida mara saba kwenye kichwa chake huku akisema “ nuizo geuka ndege.” Tatu alikwenda kwa saida huku akiwa na furaha na kumtaka dada yake amsuke nywele. Saida alikubali hilo. Akaanza kumsuka na kumchoma sindano mara ya kwanza. Saida aliruka kwa maumivu. Hata hivyo, Tatu alimwambia “ulikuwa na mvi nimeung`oa.” Alifanya hivyo hadi mara ya saba papo hapo Saida aligeuka ndege na kuruka. Alipokuja muume wake Saida hakujua kuwa yule alikuwa si Saida. Hivyo aliendelea kuishi na Tatu.

Katika tukio hili tunaona namna Saida anavyoathiriwa na sindano baada ya sindano kuchomwa kwenye kichwa huku zikitumia manuizo. Tukirejelea nadharia ya Uhalisiajabu tunagundua kuwa msanii anajaribu kuakisi mazingaombwe kutokana na manuizo na sindano kuwa na uwezo wa maajabu ambayo hatimae yanamfanya Saida ageuke kuwa njiwa. Wakati akijadili kuhusu hirinzi ambayo pia hufanya kazi kama usihiri Muteso (2012), anasema kwamba maneno mengine ambayo huzungumzwa katika miktadha fulani huwa na sifa za usihiri.

Katika hadithi ya sita (6), yenye kichwa cha *Mbwa Mahoka* kunatukio la kisihiri ambalo linatumiwa na Mzee Haji ambaye anazungumza maneno yenye nguvu za kisihiri ambayo yalifika hadi waliko mbwa wake aliokuwa amewafungia. Maneno haya yalikuwa yakisema “*mbwa wangu mwaniacha nalia ni mazimwi.”* Maneno haya yaliwafanya mbwa wavunje banda walilokuwa wamefungwa na kukimbilia

msituni ambako alikuwa amezingirwa Mzee Haji na mazimwi. Kutokana na hali hiyo mbwa hao walifanikiwa kumuokoa Mzee Haji.

Katika hadithi ya kumi na mbili (12), yenye kichwa cha habari. *Hadithi ya Kisiki* tunasimuliwa namna muhusika jini anavyotumia maneno ya kisihiri. Maneno haya ya kisihiri yalidhihiri wakati Salma alipompa taarifa kwamba majirani wanataka waje wamuone. Suala hili halikumfurahisha hivyo basi anatamka maneno kwa kusema "…kuanzia hivi sasa ondoka katika nyumba yangu..." Maneno haya yalikuwa na nguvu za kisihiri ambazo zilimfanya papo hapo Salma ajikute ametoka katika nyumba hiyo na kupelekwa mbali kabisa na nyumba hiyo. Tukio hili tunasimuliwa hivi:

> "Bi Salma alipokuja muumewe akamwambia majirani wote wananambia kwamba wanataka wakuone hawakujuwi. Yule mwanamme akamwambia nilikwamba vipi? Kwa hiyo kuanzia hivi sasa ondoka katika nyumba yangu. Salma akajikuta amerejea pale pale kwenye kisiki…"

Katika hadithi hii ya Kisiki maneno yanayotamkwa na jini kumwambia Salma kama yanvyojitokeza katika dondoo la hapo juu yanasadifu moja kwa moja na Nadharia ya Uhalisiajabu kutokana na kuwa kwake na nguvu za kimiujiza. Kwa sababu ya manuizo haya ghafla Salma anajikuta ametolewa katika nyumba yake na hatimae anapelekwa kwenye kisiki ambapo alijikwaa mama yake Bi Aisha kabla ya kuchukuliwa ujauzito ambako aliweka ahadi ya kukipatia mtoto atakaejifungua.

### 4.2.5 Ndoto za Kisihiri

Katika hadithi namba nane (8), yenye kichwa cha habari hadithi ya *Mazimwi Wala Watu*, tunaelezwa namna katika jamii kulivyokuwa na mazimwi yaliyokuwa yakiishi

katika msitu wenye kiza kinene. Mazimwi hayo kila mwisho wa mwezi yalifanya sherehe kubwa. Katika sherehe hiyo walipika vyakula mbali mbali. Kitoeleo kilikuwa nyama ya mtu. Hivyo katika kila mwezi walikuwa wanakamatwa watu kijijini na kupelekwa msituni tayari kwa matayarisho ya shughuli ya sherehe. Siku moja Makame wa Makame alikamatwa na mazimwi na kwenda kuekwa katika msitu wa Mazimwi. Kwa bahati mzuri kulikuwa na zimwi mwanamke aliyemuhurumia sana na kumpa siri ya namna ya kufanikisha kutoroka. Zimwi yule alimwambia Makame wa Makame kwamba “mazimwi wanapokuwa hawajapata usingizi wanakua kimya na wanapokuwa wamelala huwa wanazungumza kwa sauti. Hivyo utaposikia mazimwi wakizungumza wakati wa usiku ujuwe wameshapata usingizi wanaota. Utatumia fursa hiyo kutoroka.” Siku ya pili yake wakati wa usiku Makame wa Makme aliposikia mazimwi yanapiga kelele alitoka katika msitu na kukimbia. Mazimwi walipoamka walimtafuta kila pembe lakini hawakufanikiwa kumuona Makame wa Makame. Hivyo walighadhibika sana.

Tukirejelea nadharia ya Uhalisiajabu tunaona kuwa ndoto zinazojadiliwa katika sehemu hii zinawiana na msingi wa nadharia ya Uhalisiajabu ambao unauona uhalisia na ndoto ni vitu viwili vinavyochanganyika. Katika hadithi hii ya *Mazimwi Wala Watu* tunaona kuna usihiri unaojitokeza kupitia ndoto za mazimwi. Tukio hili linaibua maajabu ambayo yanakiuka uhalisia. Kama asemavyo Vutagwa (2013), kwamba Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni. Katika jamii nyingi ndoto huchukuliwa kuwa na maana ya kiuhalisia katika maisha ya kila siku.

### 4.2.6 Vyakula vya Kisihiri

Katika hadithi ya nane (8) yenye kichwa cha habari Mazimwi Wala Watu tunasimuliwa kuwa mazimwi walikuwa wanakula nyama za watu. Mazimwi walikuwa na kawaida ya kufanya sherehe kila mwezi ambapo hupika vyakula mbali mbali na kuwakamata watu ambao huwatumia kama kitoeleo. Inaelezwa kuwa nyama za watu ndio huwapa nguvu za kuendelea na maisha yao. Jambo hili linaonesha usihiri kutokana na nyama za binadamu kupewa nguvu za kimaajabu.

Katika hadithi hii mtunzi ametuibulia uhalisiajabu kwa kuonesha ukengeushi wa uhalisia wa vyakula vinavyoweza kuliwa. Taswira kama hii ya uhalisiajabu unaohusiana na vyakula imetumiwa na Mbogo katika tamthililiya ya *Ngoma ya Ng`wanamalundi* ambapo msanii anaonesha vizuu walikuwa wakila vyakula ambavyo kimsingi haviwezi kuliwa na binadamu wakawaida. Tunaelezwa kuwa vizuu walikuwa wakila majongoo, mende, minyoo, panya na nzi. Vizuu ambao wamekuwa wakiwasiliana kwa lugha isiyoeleweka wakiwa wanasimamiwa na Mahube ambaye pia anatoka katika tabaka linalokandamizwa. Kwa kuzingatia hilo mtafiti amegundua katika ngano za Zanzibar pia wasanii wametumia vyakula vya kisihiri ambavyo katika maisha ya kawaida havitumiki.

### 4.2.7 Mawasiliano ya Kisihiri

Katika ngano namba nane (8), yenye kichwa cha habari hadithi ya *Tatu na Saida* kuna mawasiliano yanayofanywa na Saida baada ya kua ndege. Tunaelezwa katika hadithi hiyo kuwa ndege huyo alikuwa anakuja karibu na nyumba na kumuulza alipomuume wa Tatu. Anapoambiwa kuwa amekwenda msikitini husema `akija ni salimia.` Siku Tatu alipompa salamu hizi muume wa Saida papo hapo yule muume alijihisi hawezi

kujizuaia, lazima ampate huyo ndege. Hisia hizi hazikuweza kuzuilika hadi pale ndege huyo alipokuja.

Pia, katika hadithi namba sita(6), hadithi ya *Mbwa Mahoka* tunaelezwa namna mzee anayezungurukwa na mazimwi anavyowasiliana na mbwa wake kwa mtindo wa kisihiri. Tunaelezwa kuwa mzee huyo alikuwa mbali na walikokuwa mbwa wake. Hata hivyo sauti hiyo iliwafika mbwa hao na kuifuata hadi alikobwana wao na kumuokoa.

### 4.2.8 Safari za Kisihiri

Motifu za safari ni moja miongoni mwa matukio ya kisihiri katika hadithi simulizi za Zanzibar. Katika hadithi namba tatu (3),iliypewa kichwa cha habari *hadithi ya Rajabu* tunaona kuna safari za kisihiri kadhaa. Kwanza, tukio la Rajabu kupigwa na upepo akiwa baharini na hatimae kufika katika nyumba ya majini ni tukio la maajabu. Pili, jini akawa ndege na akawa anaruka kama ndege ni motifu ya safari ya kisihiri.

Mtafiti amebaini kwamba, tukio la jini kuruka na kuonekana na binadamu akiwa angani nitukio la kisihiri kwa sababu katika maisha ya kawaida huwa halitokei. Hivyo tukio hili limefumwa kiuhalisiajabu kama asemavyo Waliaula (2013), kwamba matukio ya uhalisiajabu huwa yanakiuka misingi ya ushabihi kweli. Yaani hufumwa yakiwa yamekiuka uhalisia wa kijamii.

### 4.2.9 Mandhari ya Kisihri

Mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina yoyote ya fasihi. Hadithi simulizi za Zanzibar zimechanganya mandhari ya kiuhalisia na ya kiuhalisiajabu hivi kwamba ni vigumu kuweka mipaka ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa ndoto.

Kwa kutumia maandishi ya kiajabu na yasiyozoeleka, hadithi hizo zinatumia mandhari ya baharini, misituni, kwenye mito na maziwa. Mtunzi ametumia mandhari haya yakiajabu ambayo yanasawiri sifa ya usihiri. Katika hadithi namba tatu (3), hadithi ya Rajabu tunaelezwa kwamba Rajabu alikuwa anakwenda kuvua na hatimae kukumbwa na dhoruba iliyompepeusha na kufika katika jumba kubwa la kifahari la kijini. Jumba hilo lilikuwa limejaa kila aina ya vitu vya thamani. Ni katika nyumba hii ambayo Rajabu anatishwa na jini lakini hakutishika hatimae Rajabu anamtisha jini mwenye nyumba hiyo kwa kumwambia kuwa amekuja kuondoa uhai wake Ili kumuachia huru akubali kuhama katika nyumba hiyo na kila kilichomo ndani yake na asithubutu kumsimulia mtu yoyote siri hiyo. Jini ana kubali na anahama. Rajabu anapata fursa ya kuchukua mali hiyo.

Matukio haya yanakwenda sambamba na nadharia ya uhalisiajabu ambapo moja kati ya msingi wa nadharia hii ni kutumia mandhari kama vile bahari. Katika tukio hili tunaona nyumba ikiwa kati kati ya bahari jambo ambalo linaweza kukubalika katika misingi ya usihiri na uhalisiajabu.

Mandhari nyengine yenye kusawiriwa kisihiri yamejitokeza katika hadithi namba mbili (2) yenye kichwa cha habari kisemacho , *hadithi ya Zena*. Katika hadithi hii Zena anatakiwa na mama yake aende akaoshe vyombo na kufua nguo kwenye mto ambao ni makazi ya majini. Kwa kawaida ilikuwa watu hawendi katika mto huo kwa sababu mtu yoyote anayefika katika mto huo alikwa analiwa na majini. Kutokana na kulazimishwa na mama yake wa kambo alilazimika kwenda. Alipofika alikamatwa na majini wakataka kumla. Hata hivyo baada ya kumsimulia yale anayotendewa na mama yake majini walimsameha na kumtaka aingie kwenye maji aoge. Zena

alikubali hilo na alipojirushia maji ghafla aligeuka Muarabu. Mandhari haya ya mto yamechorwa kisihiri kutokana na maji hayo kumbadilisha Zena.

Tunaporejela nadharia ya uhalisiajabu tunaona kuwa mandhari ya mto huu yamesawiriwa kisihiri. Maji ya mto huo yanauwezo wa nguvu za kisihiri kutokana na kuwa na uwezo wa kumbadilisha mtu kutoka umbo moja na jengine. Mutiso (2012), anasema kuwa hirinzi ambazo huwa na nguvu za kisihiri huweza kutumika katika maji ambapo huwa maji hayo yametiwa dawa fulani. Hivyo basi, yaelekea maji haya yanalinganishwa na nguvu hizo.

Katika hadithi namba nane (8), yenye kichwa cha habari hadithi ya Mazimwi Wala Watu kunatumika mandhari ya ndotoni. Mazimwi wanapokuwa wamelala ndio hufanya mawasilianao ya kinjozi. Wakati huo ndio huwa wamelala bila kujifahamu huzungumza mazungumzo. Tunaelezwa kuwa kutokana na mazimwi kulala Makame wa Makame alipata nafasi ya kuwatoroka mazimwi hao baada ya kupata siri hiyo kutoka kwa zimwi aliyemuhurumia Makame wa Makame.

Tukio hili ni la maajabu. Katika uhalisia wakati mtu ama kiumbe mwengine yoyote anapolala huwa hazungumzi ispokuwa maneno ya kuropoka ambayo kwa kawaida huhusiana na mambo ambayo huwa yamemkabili mtu katika maisha yake ya kila siku ama yamo katika jamii yake. Hivyo basi, mandhari haya yanafanana na msingi wa nadharia ya Uhalisiajabu ambapo Vutagwa (keshatajwa) anasema kuwa kazi za kihalisiajabu huwa hazitofautishi matukio ya kihalisi na matukio ya kwenye ndoto.

Katika sehemu hii tumefanya uchambuzi wa vipengele vya usihiri vilivyojitokeza katika ngano teuele za Zanzibar. Katika ucahmbuzi wetu tumebaini kuwa hadithi za

Zanzibar zimekuwa zikitumia vipengele kadhaa vya usihiri ambavyo hujikita katika usawiri wa wahusika, motifu za safari za kisihiri, matukio ya kisihiri, vyakula vinavyosawiriwa kisihiri, manuizi ya kisihiri na mandhari za kisihiri ambazo kwa ujumla wake huibua matukio ya uhalisiajabu. Hivyo basi, katika sehemu inayofuata tumefanya uchambuzi wa vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar na namna vipengele hivyo vinavyoibua dhamira.

## 4.3 Dhamira za Usihiri Zinazobainishwa katika Ngano za Zanzibar

Lengo mahusui la pili la utafiti huu lililenga kutafiti namna dhamira za usihiri zinavyobainishwa katika ngano za Zanzibar. Data zilizokusanywa na mtafiti zilionesha kuwa ngano za Zanzibar zimesawiri usihiri kama mbinu ambayo ndani yake kunajitokeza dhamira kadhaa zinazoihusu jamii lengwa. Miongoni mwa dhamira ambazo zinajidhihirisha ni kama vile ukoloni, ubaya wa mama wa kambo, ushujaa, ujasiri, wivu na choyo nakadhalika. Katika sehemu hii mtafiti amefanya uchambuzi na uwasilishaji wa namna vipengele vya usihiri vinavyoibua dhamira katika ngano teule.

### 4.3.1 Ujasiri

**Jadwali Na. 1 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Ujasiri**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Ujasiri | 1. Hadithi ya Rajabu (Na. 3) |

Ujasiri ni hali ambayo mtu anafanya maamuzi bila ya woga tena kwa kujiamini na kuwa na msimamo usioyumba (Mzee, 2015). Katika hadithi namba tatu (3), iliyoitwa

hadithi ya Rajabu, Rajabu anaibua usihiri wakati alipotishwa na jini. Rajabu hakuviogopa vitisho vya jini hata kidogo na hatimae Rajabu anamtisha kwa kutumia mbinu ya kumwambia kuwa "mimi ni malaika wa kutoa roho hivyo nimekuja kuchukua roho yako." Pia, Rajabu anapata ujasiri wa kuwatisha majini wakati wakiwa na sherehe katika jumba lao katika bahari na hatimae majini wote waliokuwepo pale walifariki.

Kupitia matukio haya ya kisihiri msanii anaibua dhamira ya ujasiri. Katika masimulizi haya mtunzi anatuonesha kuwa ujasiri ni suala muhimu kabisa. Ujasiri kwa mtu ili kujiokoa na matatizo yaliyomkabili. Ili kuyashinda masaibu mbali mbali ambayo huwakuta watu lazima watu wawe na ujasiri. Ujasiri aliokuwa nao Rajabu ndio uliomuokoa na hatari iliyomkabili dhidi ya jini. Ujasiri huu ndio uliowapelekea kujinasua na hali ngumu ya maisha. Nadharia ya uhalisiaajabu imempa dira mtafiti kupitia muhimili wake unaosema "mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa.Ibara hii ina maana kwamba wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja". Kupitia mwongozo huo na data alizozikusanya mtafiti tumebaini namna Rajab alivyoIbua swala la ujasiri katika mazingira ya bahari ambapo alifanikiwa kuwahamisha majini na kumuwezesha kupata utajiri. Kwa mantiki hiyo Nadharia ya Uhalisiaajabu imewazindua wanajamii ya kwamba katika harakati za kutafuta ukombozi wa aina yoyote ule swala la mapambano linahitajika ili jamii ifikie malengo waliyo yakusudia.

### 4.3.2 Malezi

**Jadwali Na. 2 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Malezi**

| Dhamira | Hadithi |
|---|---|
| Dhamira ya Malezi | 1. Hadithi ya Tatu na Saida (Na.7)<br>2. Hadithi ya Zena (Na.2) |

Malezi ni tabia ya wazazi kukaa pamoja na watoto wao, kwa ajili ya kuwapahuduma zote za msingi na kuwaongoza katika tabia njema huku wakizingatia mila na dasturi katika jamii zao. Dhamira ya malezi pia inasawiriwa katika hadithi teule kupitia mbinu za kisihiri. Katika hadithi ya *Tatu na Saida* iliyopewa jina hadithi namba (7).Katika hadithi hii kunajadiliwa namna Mwajuma anavyotumia usihiri ili kuonesha upendo kwa upande wa Tatu na kuonesha chuki kwa upande wa Saida. Mwajuma anampa Tatu sindano ya usihiri ili kumdhuru Saida na hatimae anafanikisha kumgeuza ndege.

Tukio hili la usihiri linaibua dhamira ya malezi. Tunaoneshwa namna baadhi ya wazazi walivyo na tabia ya kuwapenda baadhi ya watoto wao na kuwachukia wengine. Kutokana na tabia kama hii waliyonanyo wazazi wanajikutia wakisababisha migogoro isiyo ya lazima ndani ya familia na hata mara nyengine kusababisha madhara makubwa ikiwa ni pamoja na baadhi ya watoto kuchukua maamuzi yasiyofaa baada ya kutambua kwamba baadhi ya ndugu wanapendwa zaidi katika familia.

Katika hadithi ya *Zena* tunaoneshwa malezi yanayofanywa na mama wa kambo kuwa hayafai. Tunaelezwa kwamba mama yake Zena alimlazimisha kwenda kufua

nguo na kuosha vyombo katika mto ambao ulikuwa na hatari. Huko anakamatwa na majini ambao wanakaribia kumla lakini wanamsamehe baada ya kueleza namna alivyojieleza kuhus ukatili wa mama yake wa kambo. Ili kuonesha jambo lisilo la kawaida majini wanamuamuru Zena akaoge katika mto na papo hapo akapta utajiri. Kupitia tukio hili la usihiri tunasawiriwa malezi ya mama wa kambo kwamba kila siku huwasukuma watoto wa kambo katika matukio na matendo ambayo hatima yake ni kuwaingiza katika majanga makubwa. Hata hivyo, watoto hao huwa wanapata msaada kwa watu wegine na hatimae kuibuka kuwa watoto waliobora. Wazo hili linathibitika kupitia utafiti alioufanya Bwanga (2016), alipochunguza usawiri wa mama wa kambo katika hadithi simulizi za Zanzibar aligundua kuwa hakuna hata hadithi moja kati ya alizozikusanya ambayo imemchora mama wa kambo akioneshwa akiwa na matendo mema dhidi ya watoto wa kambo.

Uzoefu wa mtafiti unaonesha kuwa mama wa kambo wamekuwa wakiishi na watoto wa kambo kwa aina fulani ya uadui. Watoto hawa hawapewi fursa sawa na mara nyingi huwa wanalaumiwa kwa yale wanayoyatenda. Mawazo haya pia yalithibitishwa na mjadala wa wavikundi ambapo wao walisema kuwa malezi ya mama wa kambo dhidi ya watoto wa kambo ni ya chuki tu. Bwanga (2017), alifanya utafiti akichunguza usawiri wa mama wakambo katika malezi ya watoto kama nafasi hii inavyosawiriwa katika ngano za Zanzibar. Katika utafiti huo mtafiti aligundua kwamba hakuna hata ngano moja iliyomchora mama wa kambo akiwa mwema dhidi ya watoto wa kambo. Mama hao wamechorwa wakiwa ni wakatili katika kuwalea watoto wa kambo. Kupitia nadharia ya uhalisia ajabu ambayo mtafiti aliichagu katika kuchmbulia data za utafiti imepinga vikali swala la malezi mabaya kupitia muhimili

aliosema Wanjiru (2013) yakwamba "Uhalisiaajabu unapinga uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya watu kiutengano" kwa minajili hiyo nadharia ya uhalisiajabu imeona chanagamoto zilizoikumba jamii ya Zanzibar na kuitaka jamii hiyo iwachane na maswala ambayo hayana nafasi katika maendeleo ya jamii na hatiama yake huzalisha chuki, uhasama miongoni mwa wanajamii na hudumanza maendeleo endelevu katika Taifa letu.

### 4.3.3 Ushujaa

**Jadwali Na. 3 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Ushujaa**

| Dhamira | Hadithi Ushujaa |
|---|---|
| Dhamira ya Ushujaa | 1. Hadithi ya Miza (Na.1)<br>2. Hadithi ya Rajabu (Na. 3) |

Mzee (2015), anasema kwamba ushujaa ni hali ya kutenda jambo kubwa ambalo katika hali ya kawaida huwa linawashinda watu wengi. Pia, shujaa huweza kutazamwa kwa mtu kufikwa na jambo na akaweza kulivumilia ili aweze kulipatia utatuzi na wakati huohuo anawakinga wengine wasipatwe na athari. Dhamira ya ushujaa imejitokeza katika hadithi namba (1) yenye kichwa cha *hadithi ya Zimwi* kupitia mhusika Miza pale alipomuona shemegi yake akiwa na tabia na vitendo visivyo vya kawaida (zimwi). Tunaelezwa shemegi huyo alikuwa na mkia uliokuwa ukiwaka moto. Hata hivyo hakuogopa hadi pale alipomshuhudisha dada yake. Kutokana na tukio hilo Miza na dada yake pale pale waliamua kurudi kwao bila ya kusita au kuwa na hofu.

Pia, dhamira ya ushujaa inajitokeza katika hadithi ya Rajabu hadithi iliyopewa namba (3) kupitia mhusika Rajabu. Katika hadithi hii tunasimuliwa tukio la kisihiri analolitenda Rajabu wa kuwashituwa majini waliokuwa kwenye sherehe na hatimae wote wanakufa. Huu ulikuwa ni ushujaa ambao ulimpasa kuwa nao Rajabu ili kuokoa maisha yake. Kupitia tukio hili tunaoneshwa namna tabaka la chini linavyotakiwa kuwa na ushujaa ili kupambana na ukandamizaji unaoendelea katika jamii.

Katika jamii ya Zanzibar kulifanikisha mapinduzi ya kuung’oa utawala wa Mwarabu kutokana na ushujaa wa wananchi wa Zanzibar wakisaidiwa na Waafrika wengine kutoka nchi jirani kama vile John Okello (Mbogo, 2015). Wakati wa mjadala wa vikundi watafitiwa walieleza kuwa ushujaa ni mbinu muhimu sana katika harakati za kujenga jamii mpya endelevu. Ilielezwa kwamba kutokana na kukosekana kwa ushujaa miogoni mwa wanajamii kumepelekea kuendelea ukandamizaji na unyonyaji dhidi ya tabaka la chini.

Nadharia ya uhalisiaajabu pia haikuliwacha nyuma suala la ushujaa katika kupigania haki kupitia muhimili unaosema mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, miti, misitu, majini, mazimwi binadamu hurejelewa ili kuonesha ushujaa katika maeneo yaliyozungukwa na jamii. Hivyo basi mtafiti kupitia data alizokusanya amebaini kwamba suala lolote la ukombozi haliwezi kufanikiwa bila ya kuwepo matendo ya kishujaa katika jamii yetu ya Kizanzibar.

### 4.3.4 Uongozi Mbaya

**Jadwali Na. 4 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uongozi Mbaya**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Uongozi Mbaya | 1. Hadithi ya Mazimwi Wala Watu (Na.8) |

Uongozi mbaya ni uongozi ambao haujali maslahi ya wanaongozwa. Mara nyingi, kiongozi mbaya huwa na tabia zisizoendana na jamii anayoiongoza. Kiongozi huyo anakuwa hakubaliki katika jamii yake na wakati mwengine hata katika jamii nyengine (Mzee, 2015). Katika hadithi namba 8 yenye kichwa cha habari hadithi ya Mazimwi Wala Watu kunatumika usihiri wa kindoto ambapo mazimwi wanapokuwa wanazungumza usiku huwa wamelala. Mazimwi hayo tunalezwa kuwa walikuwa na tabia ya kinyama ya kula nyama za watu. Kupitia tukio hili msanii anaibua dhamira ya uongozi mbaya ambao umekuwa ukiendeleza ukatili, dhulma na ukiukaj wa haki za binadamu katika jamii. Kula nyama za binadamu inaashiria ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu unaofanywa na watu wa tabaka la juu.

Tatizo la ukiukaji wa haki za walalahoi ulimwenguni limekuwa la kihistoria. Tatizo hili limekuwa likifanywa na wakoloni katika nchi za dunia ya tatu na hata baada ya nchi hizi kupata uhuru wa bendera hali hii imekuwa ikiendelea. Matokeo yake ni kudhoofisha ustawi na mustakabali mzuri wa maisha ya watu wa tabaka la chini. Kwa mfano, Mulokozi (2012) alipokuwa akifanya uchambuzi wa riwaya ya Makuadi wa Soko Huria (2002) anausawiri uongozi wa kikoloni ambao uliunda pembe tatu; yaani mabepari wenyeji, mabepari wa kigeni na viongozi wa serikali ambao kwa pamoja walishirikiana kupora raslimali za nchi za Afrika na hivyo viongozi

kujigeuza kuwa mafisadi na mawakala wa nchi za kigeni.Kwa ujumla tunasema kwamba hadithi simulizi za Zanzibar zimesadifu sifa za viongozi waliokuwepo wakati wa ukoloni na baadhi ya wale wanaoendelea kutawala nchi za Afrika baada ya ukoloni. Nadharia ya uhalisiajabu imetoa mwamko mkubwa kwa kutumia wahusika mazimwi kiishara kuashiria baadhi ya viongzi wasio waadilifukwa wananchi wao. Wanabadilka mara tu baada ya kuchaguliwa na kuingia katika uwongozi. Wanakuwa hawana tena habari ya wapiga kura na hatimae hutumia kodi za wanyonge kujitajirisha na familia zao.

### 4.3.5 Utu

**Jadwali Na. 5 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Utu**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Utu | 1. Hadithi ya Mazimwi Wala Watu (Na. 8) |

Utu ni tabia na matendo mema ya binadamu. Mtu iwapo hana matendo mema hubakia kuwa mtu asie na utu. Kama asemavyo Sengo (2009), kwamba utu wa mtu hupimwa kwa matendo yake mema. Katika hadithi teule tumebaini vipengele kadhaa vya usihiri ambavyo vimetumika kwa minajili ya kujadili dhamira ya utu katika jamii. Kwa mfano, katika hadithi namba 8 yenye kichwa cha habari hadithi ya Mazimwi Wala Watu tunaona msichana zimwi alivyofichua siri kwa Makame wa Makame ili aokoe maisha yake. Alimueleza kuwa wakati anaposikia mazimwi yanazungumza wakati wa usiku ajue wamelala hivyo atumie fursa hiyo kutoroka. Makame wa Makame anafuata maelekezo hayo na anafanikiwa kutoroka na kuokoa maisha yake.

Katika usihiri huu tunaibuwa dhamira ya utu. Tunaona kwamba utu ni sifa ya pekee ambayo huwa nayo kiumbe. Kutokana na utu matatizo kadhaa huweza kuepukika. Pia, sifa ya utu humfanya kiumbe awe na huruma na kuweza kumsaidia kiumbe mwengine wakati shida inapomkabili. Sifa hii ndio inayomfanya msichana wa kizimwi amsaidie Makame wa Makame kuokoa maisha yake bila ya kujali hatari ambayo ingeweza kumkabili iwapo mazimwi wenzake wangegundua hilo.

Matukio haya yanaakisi mawazo ya Njogu na Wafula (2007), wanaposema kwamba fasihi huwasilishwa na kumchochea msomaji kujitafutia na kujigundulia mengi kwa kumfumbia ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi. Hivyo basi, utalii ulioufanywa na mtafiti katika hadithi ya Makame wa Makame ulituonesha namna baadhi ya Wazanzibar walivyo na utu na kwa sababu ya utu huwasaidia wengine wanapokuwa na shida. Watafitiwa katika mijadala ya kikundi walieleza kuwa kihistoria jamii ya Wazanzibar imekuwa ikikumbukwa kwa sifa ya ukarimu, upendo na ubinadamu bila ya kujali ukabila, dini na utabaka. Matendo haya ndiyo yanayotuonesha utu wa wkaazi wa visisiwa vya Zanzibar.

Sambamba na hayo, Nadharia ya Uhalisiaajabu sio tu huangazia matendo maovu yanayoebuliwa na mtafiti katika dhamira za usihiri bali pia husawiri matendo mema yanayotendwa katika jamii ya Kizanzibari, ili kuyaweka wazi maisha ya Wazanzibar yalivyo na namna yanavyoiathiri jamii hiyo.

#### 4.3.6 Uchoyo

**Jadwali Na. 6 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uchoyo**

| **Dhamoira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Uchoyo | 1. Hadithi ya Tatu na Saida (Na. 7) |

Dhamira ya uchoyo imeelezwa katika hadithi namba (7), yenye kichwa cha habari Tatu na Saida. Tukio la Tatu kutumia manuizi ya kisihiri linamfanya Saida ageuke ndege kutokana na choyo alichokuwanacho Tatu na mama yake dhidi ya Saida. Katika hadithi hiyo tunaoneshwa namna uchoyo unavyosababisha watu kuwaathiri watu wengine. Mtu mwenye uchoyo huweza kumfanyia uchoyo hata mtu wake wa karibu kama mama, baba, mtoto, mke nakadhalika bila kujali athari zinazoweza kujitokeza. Hivyo basi, kupitia tukio hili la usihiri mtafiti ameibua dhamira ya uchoyo. Tunatanabahishwa kuwa athari za choyo huweza kumrejea yule anayefanya uchoyo huo. Kwa mfano, katika hadithi hii tunaona namna Tatu na Mwajuma wanavyoadhirika baada ya ukweli kubainika na Saida kurejea katika umbile lake la binadamu wa kawaida. Kuhusiana na ubaya wa uchoyo Salim (2015), anaonesha namna Sapa anavyopata upofu katika riwaya ya *Kusadikika* kutokanana uchoyo aliomfanyia Salihi wa kutaka kugawana kila kitu ambacho atakiomba kwa Mungu.

Watu wengi ni wachoyo na hawaridhiki na kile wanachokipata. Kutokana na choyo walichonacho hujikuta wakitumbukia katika matatizo. Baadhi ya watu hujiingiza katika imani za kishirikina ili kupata mali kama walivyo watu wengine. Matukio ya mauaji ya vikongwe, walemavu na hata watu wengine ambayo hutokea mara kwa

mara huendana na matokeo ya choyo yanayowasukuma watu kutaka mali kwa haraka na hatimae kujiingiza katika vitendo vya kishirikina na hata wizi na ujambazi.

Nadharia ya uhalisiajabu, ni miongoni mwa nyenzo muhimu katika kupambana na suala la uchoyo katika jamii na ndio maana yale matendo yasiokubalika katika jamii yakadhihirishwa ili yaweze kukemewa. Pia mtafiti wakati alipochambu data za utafiti amebaini kuwa uchoyo unapokithiri katika jamii husababisha hasadi, chuki, migogoro na migongano na wakati mwengine hupelekea vifo. Mtafiti ameshauri kuwa jamii ya Zanzibar iwachane na suala hilo kwani ni aduwi wa maendeleo.

### 4.3.7 Kiburi

**Jadwali Na. 7 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Kiburi**

| **Dhamoira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Kiburi | 1. Hadithi ya Zena (Na. 2)<br>2. Hadithi ya Rajabu (Na. 3) |

Katika hadithi ya Zena ambayo ni hadithi namba (2), kuna tukio la kisihiri lililojitokeza kwenyemjadala kati ya Zena na majini. Tukio hilo lilitokea wakati Zena alipokwenda mtoni ambako hakwendi watu. Zena alikuwa hayuko tayari kwenda katika mto huo kwa sababu ya kuhofia usalama wake dhidi ya majini. Lakini kutokana na kiburi alichokuwa nacho mama yake wa kambo alimlazimisha Zena aende kufua nguo na kuosha vyombo katika mto huo hatari bila ya kujali usalama wa Zena.

Kupitia tukio hili la kisihiri msanii anaibua dhamira ya kiburi kwa mama wa kambo. Mama wengi wa kambo huwaingiza watoto wao wa kambo katika mateso ambayo huweza kuhatarisha afya na hata maisha yao. Ni kutokana na sifa hii ya kiburi mama huyu anamlazimisha Zena kwenda katika mto wenye majini hatari.

Usawiri huu wa mama wa kambo umesadifu matendo yanayotendwa na mama wa kambo wengi katika jamii ya Zanzibar. Mama wakambo mara kadhaa wamekuwa wakilalamikiwa na familia kwamba hawatendi matendo mazuri kwa watoto wao wa kambo. Wakati wa majadiliano ya vikundi ilielezwa kwamba baadhi ya watoto huamua kuhama katika familia zao kwa sababu ya matendo mabaya ya unyanyasaji wanayotendewa na mama wa kambo. Ubaya wa mama wa kambo dhidi ya watoto wa kambo pia umewahi kugunduliwa na Ali (2015) na Mbwanga (2017), ambapo anasema kwamba mama wa kambo wamekuwa ni wabaya na hawawalei vizuri watoto wa kambo katika jamii za Uswahilini. Tabia hii imeondoa imani ya mama hao kwa jamii. Ili kurudisha imani njema kwa jamii dhidi ya mama wa kambo baadhi ya nyimbo za Uswahilini kama vile “Mama wa Kambo” zimekuwa zikishadidia kuwa mama wa kambo naye ni mama.

Dhamira ya kiburi pia inasawiriwa katika hadithi namba tatu (3), hadithi ya Rajabu. Katika hadithi hii kuna usihiri unaooneshwa na jini anayejigeuza maumbo tofauti tofauti wakati alipokuwa mbele ya Rajabu. Kitendo cha jini huyu kujigeuza kilikuwa na nia ya kuonesha kiburi mbele ya Rajabu. Jini huyo alitaka kujionesha kwamba yeye ana uwezo wa kila kitu. Kujigeuza kunakofanywa na jini ni ishara ya kiburi kinachofanywa na wakoloni. Wakoloni waliitawala Afrika kwa mbinu ya ukoloni

mkongwe, baadae  ukoloni mamboleo na sasa wanaendelea kulitawala bara hili kwa sera ya utandawazi hasa katika suala la ubinafsishaji na soko huria.

Mulokozi (2012), anasema kwamba uhuria ni zao la utandawazi na unakuja na sura mbali mbali. Kuna sura ya uchumi ubinafsishaji na uwekezaji wa kigeni. Wananchi wananyanganywa ardhi na maeneo yao wanapewa waekezaji kutoka nje. Kuna utalii wa mbuga za wanyama kutoka magharibi na kuna udini (makanisa ya kilokole bila shaka kutokea Marekani). Haya yote yanawezekana kwa sababu wapo watu wenyeji, wafanya biashara na wanasiasa ambao wako tayari kununuliwa na wageni. Hivyo Rajabu ni ishara ya wenyeji wachache wenye ujasiri na wanaopinga kununuliwa na wageni.

Tukirejelea nadharia ya uhalisiajabu, inaamini kuwa wakati na mahali inauhusiano wa kiduara badala ya kistari inamaanisha kwamba jambo linaweza kujirudia kwa sura nyingine mahali pengine. Hivyo basi mtafiti alipochambua data za utafiti amebaini kuwa kiburi walichokuwanacho wakoloni wa Kiarabu hapa Zanzibar kimerudi katika sura nyengine mpya. Kiburi hicho kimerudi kupitia watawala wazalendo wanwadhofisha na kuwanyanyasa Wazanzibar mithili ya ukoloni mkongwe. Mtafiti anashauri wale viongozi wa Zanzibar wanaotumia nguvu za ziada kwa watu watabaka la chini waachane na swala hilo ili wazalendo wafurahie uhuru wao na waweze kutoa ushirikiano katika kuijenga Zanzibar.

### 4.3.8 Uvivu

**Jadueli NA.4. 1 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uvivu**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Uvivu | 1. Hdithi ya Kilicomponza Nyoka Akakosa Maguu (Na. 12) |

Bidii katika kazi ndio msingi wa maisha katika jamii zote. Katika hadithi namba kumi na tatu (12),iitwayo hadithi ya Kilichomponza Nyoka Akakosa Maguu inatumia uhalisiajabu wa wanyama kugawiana miguu wakiwa mkutanononi. Miguu inayobakia yote anajibandika jongoo hatimae nyoka kutokana na uvivu alionao alichelewa kwenda kuchukua miguu hiyo kwa wakati jambo amabalo lilipelekea nyoka kukosa miguu.

Kupitia tukio hili la kihalisiajabu tunaibuliwa dhamira ya uvivu. Uvivu umeoneshwa ukiwa na athari kubwa kwa watu katika jamii. Baadhi ya watu wamekuwa wakikosa hata mahitaji ya kila siku kutokana na uvivu. Kwa kuukemea uvivu Shaaban Robert (1967), katika riwaya ya *Kufikirika* anajadili kuhusu uvivu na anaeleza kuwa mvivu katika nchi ya Kufikrika alistahili kulaumiwa kwa sababu ya kukosa kufanya kazi.

Nadharia ya uhalisiajabu, imefungamana na sanaajadi kama vile visasili yaani hadithi zinazoelezea asili ya watu na matukio fulani. Nadharia hii imekemea vikali swala la uvivu katika jamii ya Zanzibar. Hii nikutokana na kwamba mtu anaweza kukosa haki zake za msingi ambazo zinaweza kumuathiri katika maisha yake ya kila siku. Mtafiti anaishauri jamii yake ya kwamba katika maisha ya mwanadamu uvivivu hauna nafasi na hata vitabu vya dini vimethibitisha hilo.

#### 4.3.9 Ukarimu

**Jadueli NA.4. 2Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Ukarimu**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Ukarimu | 1. Hadithi ya Mazimwi Wala Watu (Na. 08) |

Hadithi ya Mazimwi Wala Watu, hadithi namba (8) inatumia usihiri unaowafanya mazimwi kupiga kelele bila ya kujitambua wakati wanapopata usingizi. Katika usingizi huo wanapiga kelele. Hivyo siri ya kwamba wakati huo mazimwi wanakuwa usingizini inatolewa na zimwi mwanamke kumpa Makame wa Makame.

Hivyo, usihiri huu unaibua dhamira ya ukarimu. Zimwi aliyempa siri hii anaonesha ukarimu kwa Makame wa Makame. Kutokana na ukarimu huo Makame wa Makame anaokoa maisha yake. Maisha yake yangekuwa hatarini lakini zimwi huyu bila kujali kile ambacho kingeweza kumkabili iwapo wenzake wangebaini kwamba ametoa siri kwa Makame wa Makame na hatimae kutoraoka. Kutokana na miktadha hii mtafitianabaini kwamba ukarimu unaokuwepo miongoni mwa watu hupelekea jamii kusaidiana kwa hali na mali na hata katika mazingira ya hatari.

Nadharia ya uhalisiajabu, inashadadia uwepo wa swala la ukarimu katika jamii ya Kizanzibar kwani hiyo ndio mila na desturi ya wakaazi wa maeneo hayo. Mtafiti wakati wakuchambua data alibaini kuwa licha ya swala la kuingiliana kwa watu kutoka jamii moja na nyengine lkuwa kubwa ila hadi sasa wapo watu wenye matendo ya ukarimu na ubinadamu katika visiwa vya Unguja na Pemba.Kwa mantiki hiyo mtafitianashauri kuwa matendo hayo yanapaswa kuendelezwa ili kulinda heshima ya Wazanzibar.

#### 4.3.10 Nafasi ya Mwanamke

**Jedwali NA.4. 3 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Nafasi ya Mwanamke**

| **Dhamira** | **Hadithi Nafasi ya Mwanamke** |
|---|---|
| Dhamira ya Nafasi ya Mwanamke | 1. Hadithi ya Kijoka (Na. 4 )<br>2. Hadithi ya Tatu na Saida ( Na. 07)<br>3. Hadithi ya Zena (Na. 02) |

Data za utafiti zilizokusanywa katika hadithi simulizi za Zanzibar zimeonesha kuwa hadithi zilizotajwa kwenye jedwali 4.4 hapo juuzimemsawiri mwanamke kupitia vipengele vya usihiri. Katika hadithi namba nne (4), iitwayo hadithi ya Kijoka tunaona kwambakuna usihiri unajitokeza pale msichana anapoozeshwa kijoka ili familia ipate mali. Kupitia tukio hili tunaibuwa mjadala kuhusiana na nafasi ya mwanamke katika masuala ya ndoa. Tunachokibaini hapa ni kwamba wazazi humtumia mwanamke kama chanzo cha mapato au kupata mahari mengi ambayo yatawafaidisha wanafamilia. Kutokana na tamaa ya mali wanawake wengi katika jamii za Afrika wanabakia hawana maamuzi kuhusu ndoa zao binafsi.

Wasichana hujikuta wakilazimishwa kufunga ndoa na wanaume ambao si chaguo lao lakini kwa sababu hawana la kufanya wanabakia kuridhia na kukubali maisha hayo. Hili linasawiriwa pia na Mbia (1961 ), katika tamthiliya ya *Three Suitors: One Husband* ambapo anamuonesha Julieta, msichana wa shule ya sekondari anapokelewa mahari na babu yake (Abessolo) na baba yake (Atangana) bila hata yeye kushauriwa. Mathalani, anapodai kuwa ipo haja ya kupata fursa ya kutoa ushauri wake Abessolo anadai kuwa katika jamii ya Mvoettosi mwanamke hawezi

kushauriwa kuhusiana na suala la ndoa. Pia, Abessolo anasisitiza kuwa iwapo Jullieta atapewa fursa ya kuchagua mchumba anayemtaka ataleta mwanamme ambaye hana nyumba, hana gari, hana nguo ni maskini kama nzi. Kauli hii inatuonesha namna suala la ndoa linavyogubikwa na tamaa ya kupata mali katika jamii.

Katika hadithi namba 7 iitwayo hadithi ya hadithi ya Tatu na Saida tunaoneshwa namna mwanamke alivyo na uchoyo kwa watoto wa kambo. Mwanamke amekuwa akiwatendea watoto wa kambo matukio ambayo huweza kuwaangamiza. Kwa mfano, Mwajuma anashirikiana na Tatu ili kumtendea usihiri Saida. Hatimae inapobainika kwamba walimfanyia uadui Saida wanajikuta katika fazaa kubwa. Dhamira hii pia inajitokeza katika hadithi ya Zena, msichana anaelelewa na mama wa kambo na analazimishwa na mama yake wa kambo kwenda kufua nguo na kuosha vyombo katika mto wenye kuaminika kuwa kuna majini wanakula watu. Anapofika katika mto huo Zena anakamatwa na majini. Mwisho baada ya kusimulia mikasa ya mama wa kambo wanamuamuru akaoge mtoni na atageuka rangi. Tabia hii ilijadiliwa na watafitiwa katika kikundi na kuonesha kuwa mama wa kambo vyovyote viwavyo hawako wasafi katika kuwalea watoto wa kambo.

Nadharia ya uhalisia ajabu, imetusaidia sana  kudhihirisha uhalisia au tabia za wanawake katika maisha yetu ya kila siku na kupitia jamii zetu. Mtafiti  kupitia nadharia husika anawataka wanawake wasiotambua nafasi zao na mchango walionao katika jamii na kwa taifa kwa ujumla wabadilike kwa kuwa kigezo kizuri cha kupima michango yao na kushirikiana na wenzao ili kuleta mabadiliko ya wanawake Zanzibar na jamii  kwa ujumla.

### 4.3.11 Uhalifu

**Jadueli NA.4. 412 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uhalifu**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Uhalifu | 1. Hadithi ya Yamuimui ( Na. 9 )<br>2. Mazimwi Wala Watu (Na. 08)<br>3. Hadithi ya Miza ( Na. 14 ) |

**Chanzo: Data kotuku kwenye Utafiti**

Uhalifu ni kitendo cha kutekeleza matendo yanayopingana na kanuni na sharia za jamii ambayo husababisha kumuathiri mtu kiafya na hata mara nyengine kumpotezea maisha yake. Data zilizokusanywa na mtafiti zilionesha kwamba kuna usihiri umekuwa ukitumiwa na wahusika kama vile majini, mazimwi na hata binadamu ili kutekeleza uhalifu. Hadithi namba (9) yenye kichwa cha habari hadithi ya *Yamuimui* tunaelezwa namna Mzee anavyojigeuza mbwa ili kufichua mauaji yaliyofanywa na vijana baada ya kumuua Yamuimui.

Katika hadithi namba (8) yenye kicha cha habari Mazimwi wala Watu tunaelezwa namna mazimwi hao walivyokuwa na kawaida ya kukamata mtu kila mwezi ili kumtumia kama kitoeleo katika sherehe zao. Makame wa Makame anafanikiwa kutoroka na kuepuka uhalifu huu baada ya kupewa siri na zimwi mwaname kwamba unaposikia mazimwi wanazungumza wakati wa usiku ujue ndio tayari wamelala. Baada ya kutambua hilo alifanya kama alivyoelekezwa. Kutokana na tukio hili watu wanatakiwa wawe majasiri na wenye kufanya maamuzi mazito ili kupambana na uhalifu unaotendeka.

Matendo ya uhalifu pia yamesawiriwa kupitia malezi ya watoto wa kambo. Katika hadithi ya kwanza (1) hadithi ya Miza tunaelezwa namna Miza alivyolazimishwa kwenda kwenye mto amabao una majini wanaokula watu. Kutokana na Miza kulazmishwa na mama wa kambo analazimika kwenda kwenye mto huo. Hata hivyo anapokwenda anatuibulia usihiri pale anapoambiwa aoge maji ya mto huo na anapooga anabadilika kutoka rangi yake aliyokuwanayo.

Wakati wa majadiliano ya vikundi ilielezwa kuwa suala la uhalifu limekuwa ni tatizo kubwa katika jamii nyingi za Tanzania na Afrika kwa jumla. Kutokana na tatizo la uhalifu baadhi ya watu wamekuwa wakihujumiwa, kupotea na hata wengine kufariki na baadae kutupwa bila ya kutambulika yule anayefanya hujuma hizo. Kwa mantiki hii tunasema kuwa masuala ya uhalifu yanayojadiliwa katika ngano za Zanzibar ndiyo tunayoyashuhudia hapa Tanzania. Kutokana na uhalifu huo serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia vikosi vya ulinzi na usalama imeapa kupambana na hujma hizo huku ikiwataka wale wanaotekeleza uhalifu huo kuacha mara moja.

Nadharia ya uhalisiaajabu imemsaidia mtafiti kudhihirisha uhalisia au tabia za baadhi ya watu tunaoishi nao katika harakati za maisha ya kila siku kwani baadhi ya matendo ya usihiri hupelekea uvunjifu wa amani katika jamii. Mtafiti kupitia nadharia hiyo anaiasa jamii kuchukuwa hadhari na sio tu kumuamini kila mtu kwani Waswahili wanasema “ Mbaya hana alama na mwema hajuilikani” hii ina maana kwamba mtu yule unaemuamini anaweza kukudhuru.

### 4.3.12 Ukoloni

**Jedwali NA.4. 5 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Ukoloni**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Ukoloni | 1. Hadithi ya Rajabu (Na. 03)<br>2. Hadithi ya Miza ( (Na. 14)<br>3. Hadithi ya Yamuimui (Na. 09)<br>4. Hadithi ya Babu Dii (Na. 10)<br>5. Hadithi ya Kisiki ( Na. 12) |

Suala la ukoloni limeshughulikiwa na kazi za fasihi andishi na zile za fasihi simulizi. Wakati wa utawala wa wakoloni katika bara la Afrika suala la ukoloni lilisawiriwa kupitia fasihi kwa mbinu ambazo ziliwafanya Wazungu kutogundua mafumbo ya kile kinachoendelea. Lengo kuu likiwa ni kuepuka mkono mrefu wa utawala wa kikoloni. Moja kati ya mtindo wa kibunilizi ambao ulitumiwa na watunzi wa fasihi wa wakati huo ulikuwa ni ule wa usihiri ama uhalisiajabu.

Katika hadithi ya Rajabu kunatumiwa mhusika jini ambaye anatumia usihiri kutokana na kujigeuza kutoka umbo tafauti tafauti. Jini huyu ametumika ili kuibua dhamira ya ukoloni. Wakoloni walitumia mbinu kadhaa za kuwatisha Waafrika ili kusudiwajengehofu na hatimae kuwatumia Waafrika kama ngazi ya kujilimbikizia mali. Tunaelezwa kuwa jini huyo alikuwa amejenga nyumba kubwa ya kifahari na ndani ya nyumba hii mulikuwa na mali nyingi. Hadithi hii inasawiri umwinyi uliokuwa ukifanywa na watawala wa kikoloni katika bara la Afrika, Zanzibr ikiwemo. Kitendo cha Rajabu kuwatisha majini na hatimae kufa wote kinasawiri

mapinduzi ya Zanzibar ambayo yaliwaondoa wakoloni wa Kiarabu katika visiwa vya Zanzibar. Tunaelezwa kuwa jini huyo aliacha nyumba hiyo ya kifahari na mali kadhaa. Suala hili linatiliwa mkazo  na Husseina (1971) katika utangulizi wa tamthiliya ya *Masheitani* ambapo anaeleza kuwa mapinduzi ya Zanzibar yaliwafanya watu kukimbilia Tanganyika na wengine kukimbilia sehemu nyengine za bara huku wakiacha mali zao.

Katika hadithi ya *Mazimwi Wala Watu* na hadithi ya *Miza* tunaoneshwa namna mazimwi na majini walivyokuwa na kawaida ya kula watu na kujenga woga miongoni mwa wanajamii. Kitendo hiki cha kisihiri pia kinasawiri ukoloni na matendo ya wakoloni katika jamii. Majini na mazimwi wanaashiria wakoloni na kitendo cha kula watu kinasawiri namna wakoloni walivyokuwa wakiwakandamiza na kuwanyonya Waafrika bila ya kujali utu. Kutokna na hali hii watu waliwaogopa wakoloni.

Katika hadithi ya kumi (10), iliyopewa kichwa cha habari hadithi ya Babu Dii tunasimuliwa namna tukio la kisihiri la kumramba tongo Bibi Kizee ili aone vizuri na hatimae kumsaidia Babu Dii linavyosawiri dhamira ya ukoloni mamboleo hasa katika zama hizi za utandawazi. Bikizee anawakilisha mataifa tajiri ambayo huzisaidia nchi changa baada ya kutekelezewa masharti magumu ya nchi hizo. Na pindi nchi changa zinapokataa masharti hayo hunyimwa misaada hiyo. Hivyo ili kupata misaada hiyo viongozi wengi wa bara la Afrika hugeuka kuwa makuadi wa wakoloni. Kama asemavyo Mulokozi (2012), kwamba viongozi wengi wamegeuka kuwa makuadi wa uhuria jambo ambalo huamua kushirikiana na wakoloni katika kulikandamiza na kulinyonya bara la Afrika.

Dhamira ya ukoloni pia inasawiriwa katika hadithi namba kumi na mbili (12), iitwayo hadithi ya Kisiki. Katika hadithi hiyo kama tulivyoona hapo kabla Bi Asha anakawia kupata ujauzito. Siku moja anapojikwaa kwa kisiki anaweka ahadi kwamba iwapo atafanikiwa kupata mtoto atampeleka mtoto huyo kwa kile kisiki. Siku zinapokwenda Bi Asha anapata mtoto. Anamlea mtoto yule hadi siku moja kile kisiki kinamkumbusha Bi Asha kuhusu ahadi yake ya kupeleka mtoto. Hatimae Bi Asha anampeleka Salma kama ni ahadi ya kutekeleza ahadi aliyoiweka.

Kupitia tukio hili la kisihiri tunaoneshwa namna wakoloni walivyo na tabia ya kuweka masharti magumu katika nchi maskini hasa pale zinapokuwa na shida. Kutokana na kutokuwa na nguvu nchi hizo nazo hujikuta zikitekeleza masharti wanayoikiwa na pindi wakivunja masharti hayo hujikuta wakiingia katika migogoro na nchi hizo. Katika hadithi ya Kisiki tunaona namna Salma anavyoekewa masharti na muume wake (jini) kutotoa siri yoyote na anapokubali majirani kuja kumtembelea muume wake anaonekana amevunja masharti na anaamua kumrudisha kwenye kisiki.

Tukio hili linamsawiri Bi Asha kama kuwadi wa wakoloni. Tunasema ni kuwadi kwa sababu anakubali masharti ya wakoloni na kuamua kumpeleka Salma. Chambilicho Mulokozi (2012), alipokuwa akifanya uchambuzi wa riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* ambapo anaona kuwa makuadi wa soko huria ni wale wanaosimamia uhuria ambao hufanya biashara ya kuuza watu kwa mabepari wa kigeni.

Nchi changa zimekuwa zikiathirika katika masuala ya kisiasa, kiuchumi na hata kiutamaduni. Mathalani nchi hizi zimekuwa zikipangiwa masharti mengi ambayo hayana manufaa kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi zao. Aidha, uchumi wa nchi

changa umehodhiwa pamoja na kudidimizwa na nchi tajiri ulimwenguni. Zanzibar imeshuhudia vipindi kadhaa vya unyonyaji na ukandamizaji wa kikoloni. Hadi pale Zanzibar ilipoamua kufanya Mapinduzi ili kuuondoa utawala wa kikoloni. Jesse (2017), anasema kuwa Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964 yalikuwa ya lazima kutokana na wananchi kunyimwa nafasi ya kuchagua mfumo wa kiuchumi ambao ungeweza kuwafaa.

Kwa upande wa nadharia ya uhalisiajabu, inapinga vikali sualazima la mtu mmoja au kundi fulani kuwatawala wengine kiuchumi kisiasa na hata kijamii kwa misingi ya unyonyaji na ukandamizaji. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha kuwa bado ukoloni katika jamii zetu upo ingawaje umekuja kwa sura nyengine kama vile utandawazi biashara huria, mikopo na nyenginezo.

### 4.3.13 Umasikini

**Jedwali NA.4. 6 Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Umaskini**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Umaskini | 1. Hadithi ya Babu Dii ( Na. 10)<br>2. Hadithi ya Ramadhani (Na. 03 ) |

Umaskini ni hali ya mwanadamu kushindwa kupata mahitaji muhimu ya msingi kama vile chakula, mavazi, makaazi na matibabu katika hali ya kawaida katika maisha yake. Akifafanua maana ya umaskini Ali (2017), anasema kuwa umaskini ni hali ya mtu, jamii au taifa kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za mahitaji ya maisha yake ya kila siku ikiwemo kumiliki chakula, malazi, mavazi, huduma za afya na elimu.Umaskini ni tatizo ambalo limekuwa likiikabili jamii za Afrika kwa miaka

mingi na serikali zimefanya jitihada kubwa ya kuhakikisha kuwa jamii zinaondokana na umaskini.

Katika hadithi namba kumi (10), hadithi ya Babu Dii tunaoneshwa tukio la kisihiri ambapo Babu Dii anamramba Bibi Kizee tongo ili aweze kuona na hatimae apate kazi. Tukio hili linatuibulia dhamira ya umaskini miongoni mwa mataifa ya bara la Afrika. Tunaona kutokana na umaskini mataifa machanga hayana budi ila kukubali kupangiwa masharti kadhaa ili kupata misaada kutoka mataifa tajiri ulimwenguni.

Aidha, tumegundua kuwa hadithi ya Ramadhani inasawiri hali ya umaskini wa kiwango cha hali ya juu kupitia familia ya Rajabu. Hata hivyo katika hadithi hii msanii anaonesha mbinu kadhaa za kuondokana na hali hii ya umaskni ambapo anawataka watu wafanye kazi kwa bidii. Mtunzi anamtumia Rajabu ambaye anaamua kujiingiza katika shughuli za uvuvi ili kupambana na ukali wa maisha. Vile vile msanii katika hadithi hii anapendekeza tupige vita ukoloni ili kujenga jamii mpya endelevu. Tunaoneshwa namna Rajabu alivyosimama huku akiwa na ujasiri wa kupambana na jini (mkoloni) na hatimae anapata mafanikio makubwa.

Hapa Tanzania tatizo la umaskini limekuwa sugu na la kihistoria ambalo limeshuhudiwa kwa miongo kadhaa. Tanzania imekumbwa na tatizo la umaskni tangu wakati wa ukoloni, wakati wa uhuru, kipindi cha Azimio la Arusha na hata sasa katika kipindi hiki cha mfumo wa vyama vingi.  Pamoja na juhudi kubwa zinazofanyika bado hakujapatikana utatuzi wa kupunguza hali ya ukali wa maisha hasa kwa watu wa tabaka la chini.

Ali (2017) anajadili suala la umaskini nchini Tanzania na kueleza kwamba Serikali ya Tanzania imekuwa ikiunda sera zenye kutilia mkazo na kuhimiza wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kukabiliana na umaskini. Baadhi ya kauli mbiu hizo ni "kilimo ni uti wa mgongo wa taifa," "kilimo cha kufa na kupona," na "siasa ni kilimo." Kauli mbiu hizi zilitolewa na viongozi wa serikali ya awamu ya kwanza wakiongozwa na baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere (Nyerere, 1977).

Madhumuni ya kauli mbiu hizo ni kuihamasisha jamii ifanye kazi kwa bidii ili kujenga jamiii mpya endelevu. Kwa mfano, serikali ya awamu ya tatu chini ya utawala wa mheshimiwa rais Benjamin William Mkapa ilikuja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania. Mkakati huu ulilenga kukuza sekta ya kilimo, mifugo, elimu, afya, huduma za maji safi na salama, umeme vijijini na viwanda. Mkakati huu ulisaidia sana katika kukuza sekta ya elimu ambapo mpaka hivi sasa karibu kata zote Tanzania zina shule za sekondari. Hata hivyo, sekondari hizo bado zinakabiliwa na upungufu wa walimu, vitabu, madawati, nyumba za walimu, mabweni, miundo mbinu ya maji, umeme na maabara. Jambo ambalo serikali inaendelea kukabiliana nalo ni kuhakikisha kuwa shule zote zinapata mahitaji yote muhimu ili zitowe elimu bora kwa wananchi.

Kupitia utafiti huumtafiti ameona kwamba umaskini katika jamii ya Kizanzibari bado ipo licha ya jitihada nyingi zinazochukuliwa na Serikali. Mtafiti kupitia mijadala ya vikundi alibaini kuwa baadhi ya Wazanzibari hawataki kujishughulisha na kazi zao binafsi huitegemea serikali kuwapatia ajira na hatimae kugubikwa na umaskini mkubwa na wale ambao wanajaribu kujiajiri wenyewe hujipatia mahitaji

yao ya msingi, hivyo basi mtafiti anashauri vijana wachape kazi ili waweze kujikomboa kiuchumi nasio tu kubakia vijiweni kushadadia maovu.

#### 4.3.14 Uchawi na Ushirikina

**Jadueli NA.4. 7 Hadithi nambari15: Hadithi Zinazoibua Dhamira ya Uchawi na Ushirikiana**

| **Dhamira** | **Hadithi** |
|---|---|
| Dhamira ya Uchawi na Ushirikina | 1. Hadithi ya Tango (Na 11)<br>2. Hadithi ya Mbwa Mahoka( Na.6 )<br>3. Hadithi ya Tatu na Saida (Na. 7) |

Mbonde (2005), anasema kwamba miongoni mwa tishio kubwa lililoikumba Afrika ni suala la uchawi na ushirikina. Dhamira hii imesawairiwa pia katika ngano za Zanzibar. Kwa mfano, katika hadithi ya Tango; hadithi namba (11), tunasimuliwa namna vijana waliochuma tango bila idhini ya mwenyewe walivyojikutia katika matatizo mara baada ya kulila. Tango lilipofika matumboni tu lilianza kuzungumza. Huu ni usihiri wa kile baadhi ya watu wanachokiita tego. Katika hadithi ya Mbwa Mahoka tunaelezwa namna Mzee Haji anavyowatumia mbwa anaowafuga nyumbani kwake kwa njia za kichawi. Wakati alipokamatwa na mazimwi alizungumza nao kwa njia ya kimanuizi hatimae mbwa hao aliweza kupata taarifa na kuvunja banda na kwenda kumuokoa.

Pia, katika hadithi ya Tatu na Saida hadithi namba (7) tunasimuliwa namna Mwajuma anavyokwenda kwa mganga na kupewa sindano yenye nguvu za usihiri.

Sindano hiyo alipotogwa nayo Saida kwenye kichwa aligeuka ndege. Mbonde (2005), anasema kwamba waganga wengi wa kienyeji katika jamii wamekuwa wakitumia mbinu hii ya uchawi na ushirikina kama mradi wao wa kuchumia mali.

Katika mjadala wa vikundi uliofanyika ilielezwa kuwa suala la uchawi na ushirikina lipo katika jamii na limekuwa na athari kubwa. Kutokana na imani za kishirikina baadhi ya watu hutengwa, husalitiwa na hata kuingia katika migogoro. Pia, ilielezwa kwamba baadhi ya watu hujikuta wakipoteza maisha kwa sababu za imani za kichawi na kishirikina. Matukio haya ya kisihiri hayatafautiani na mawazo ya Njogu na Wafula (2007), ambao wanaona kwamba matukio ya uhalisiajabu hukiuka uhalisia.

Kwa Hivyo mtafiti anashawishikakusema kwamba, pamoja na ukiukaji wa uhalisi katikamatukio haya ya kisihiri hata hivyoyamebeba dhamira muhimu sana zinazoihusu jamii.Kwa mfano hapa Tanzania mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) yanaendelea kufanyika kwa sababu ya imani za ushirikiana, Albino wamekuwa wakikatwa baadhi ya viungo vya mwili na hata mara nyengine kuuawa kwa sababu ya imani za kichawi na ushirikina. Hivyo basi, wakati umefika wa kuondokana na hali kama hii. Nadharia ya uhalisiaajabu imethibitisha kuwa matokeao ya Kiajabu yanaonekana ya kawaida pia huwa na hali ya kushangaza, kuduwaza na kuogofya. Kwa ujumla mtafiti anakubali kuwa nadharia hii imeliangazia kwa kina swala la uchawi ambalo limeshamiri katika jamii ya Zanzibar na baadhi ya wakati linaonekana la kawaida ndani ya jamii hizo, hivyo basi mtafiti anapendekeza kuwa swala la uchawi na ushirikina lisipewe nafasi tena katika jamii

kwani linasababisha chuki, uhasama na hata vifo na hatimae hukwamiza maendeleo katika nchi.

### 4.4 Hitimisho

Katika sehemu hii tumefanya uchambuzi wa dhamira za usihiri zinazobainishwa katika ngano za Zanzibar, Tumegundua kwamba baadhi ya hadithi simulizi za Zanzibar zimefumwa kisanii kwa matukio ya kisihiri. Matukio hayo ndiyo yanayosukuma msuko wa hadithi hizo na sio tu wasimuliaji walizitamba hadithi zao kwa lengo la kujiburudisha na kupumzika baada ya machofu makubwa walipo maliza kufanya kazi bali walikusudia kuebua mambo mbali mbali yaliyosawiri katika jamii za washahili wa Zanzibar yaliyomo ndani ya maisha yao kila siku kisiasa, kiuchumi na hata yale ya kijamii na namna yanavyoathiri jamii hiyo, ili yale yote yanayopaswa kuendelezwa yaendelezwe na yanayostahiki kuepukwa yakemewe. Hivyo basi, katika sehemu inayofuata iltafafanua muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafitiamewasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii ina sehemu tatu ambazo ni muhtasari wa utafiti uliofanywa. Sehemu ya pili inahusu matokeo ya utafiti kupitia malengo mahususi ya utafiti yaliyowekwa na sehemu ya tatu imetoa mapendekezoya utafiti.

### 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ilijikita katika kuchunguza matumizi ya usihiri katika hadithi simulizi za Zanzibar na namna vipengele vya usihiri vinavyoibua dhamira katika hadithi simulizi za Zanzibar. Hadithi zilizohusika ni zile zilizotambwa na wanafunzi ambazo baadae mtafiti alizitalii na kuzichagua zile zenye matumizi ya vipengele vya uhalisiajabu. Jumla ya hadithi kumi na tatu ziliteuliwa kama samapuli ya utafiti huu.

Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili mahususi ambapo lengo la kwanza lilikuwa ni Kubainisha vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo ni vipengele vipi vya usihiri vimejitokeza katika ngano za Zanzibar?

Katika Utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa  ngano hizo teule zimesheheni vipengele mbaimbali vya usihiri kama vile matumizi ya wahusika wa kisihiri, mandhari ya kisihiri, vyakula vya kisihiri na vingi vyenginevyo.

Lengo mahususi la pili lilikuwa ni; Kubainisha dhamira zinazoebuliwa na vipengele vya usihiri  katika ngano za Zanzibar. Lengo hili nalo liliongozwa na swali la utafiti

lisemalo; Ni dhamira zipi zinazoebuliwa na vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar?

Utafiti huu ulibaini kuwa, dhamira mbali mbalii zimeebuliwa na vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar zinaakisi maswala mbalimbali yanayojitokeza katika jamii zetu kama vile, imani za kishirikina, umaskini, uchoyo, ukoloni na nyingi nyenginezo. Kwa mantiki hiyo, ngano kama kipera cha fasihi simulizi ni vyema kuhifadhiwa na kuendelezwa kwa manufaa ya kizazi kilichopo kinacho kuja na taifa kwa ujumla.

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza ni sura ya utangulizi ambayo inaeleza mambo ya msingi ya utafiti huu. Katika sura hii mtafiti amejikita katika kufafanua usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu na malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa utafiti huu.

Sura ya Pili inahusu mapitio ya maandiko ambayo mtafiti aliyapitia kabla na wakati wa kuandika tasnifu hii. Sura hii inasehemu tangulizi, aina za hadithi simulizi, vipengele vya usihiri na mapitio ya tafiti mbali mbali kuhusu ngano. Sura hii pia imeeleza dhana ya dhamira na pengo la utafiti. Mwisho sura imewasilisha na kujadili nadharia zilizoongoza utafiti huu ambazo ni nadharia ya Uhalisiajabu na mwisho sura imeweka hitimisho la sura.

Katika Sura ya Tatu utafiti unaeleza mbinu zilizotumika kukusanya data hadi utafiti huu kukamilika. Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii ni eneo la utafiti,

walengwa wa utafiti, sampuli na usampulishaji, kuaminka na kuthibitika kwa data za utafiti. Mwisho sura hii imemalizia kwa kutoa hitimisho.

Sura ya nne, inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Sura hii imeongozwa na maswali mawili ambayo yameigawanya katika sehemu mbili, ambapo sehemu ya kwanza imefanya uchambuzi wa vipengele vya usihiri vinavyojitokeza katika hadithi simulizi za Zanzibar. Uchambuzi wa sehemu hii ya kwanza umeongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu. Sehemu ya pili imewasilishwa na kufanya uchambuzi wa vipengele vya usihiri katika hadithi teule za Zanzibar na namna vipengele hivyo vilivyotumika kuibua dhamira. Kiujumla sehemu zote mbili zimeongozwa na nadharia ya uhalisiaajabu.Mwisho, sura hii imetoa hitimisho.

Katika Sura ya Tano tunapata hitimisho la tasnifu hii. Sura hii imejumuisha vipengele kama vile muhtasari wa tasnifu yote, matokeo ya utafiti na mapendekezo. Ni katika sura hii ambapo matokeo ya utafiti huu yanaonekana na muhtasari wa tasnifu hii umewasilishwa kwa kubainishwa sura ya kwanza hadi ya tano.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Baada ya kuzifanyia uchambuzi data za utafiti huu tumeona namna ngano za Zanzibar zinavyosawiri matukio mbali mbali ya kijamii kwa mbinu ya usihiri. Vipengele kadhaa vya usihiri vianavyohusiana na mbinu za kifani vimetumika ili kujenga hadithi hizo na kuendeleza masimulizi na hatimae kuibua dhamira za hadithi hizo. Hivyo basi, maswali ya utafiti huu yaliweza kujibika kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la Utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha vipengele vya usihiri vinavyojitokeza katika ngano za Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti la kwanza lisemalo: Ni vipngele vipi vya usihiri vimejitokeza katika ngano za Zanzibar?

Katika utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa ngano za Zanzibar zimetumia vipengele kadhaa vya usihiri kama mbinu ya mtindo. Vipengele hivyo vya usihiri ni pamoja na wahusika wa kisihiri, mandhari za kisihiri, motifu za safari za kisihiri, matukio ya kisihiri, manuizo, ndoto za kisihiri na vyakula vya kisihiri. Kwa mfano katika hadithi namba 12 hadithi ya Kisiki kuna jini ambaye amejigeuza kisiki na hatimae jini huyo anamuoa Salma. Katika hadithi ya Tatu na Saida, Mwajuma na Tatu wanatumia sindano ambayo baada ya kunuilia na kumtoga Saida anageuka kuwa ndege. Pia, katika hadithi ya Majni wala watu tunaona namna majini wanavyofanya sherehe na kutayarisha vyakula mbalimbali ambavyo kitoeleo chake ni nyama ya binadamu. Kiujumla matendo hayo sio ya kawaida kutendeka katika jamii bali ni matendo ya kisihiri.

### 5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti wetu lilikuwa ni: lisemalo: Kubainisha namna vipengele vya usihiri vilivyoibua dhamira katika ngano za Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo; Ni dhamira zipi zinazoebuliwa na vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar?

Utafiti huu ulibaini kuwa, ngano za Zanzibar zimebeba dhamira tofauti za usihiri kama vile; ujasiri, ushujaa, uongozi mbaya, ukoloni, uvivu, wivu na choyo, ndoa na mapenzi, rushwa na uhalifu. Kwa mfano, katika hadithi namba 12 hadithi ya Kisiki tunaona namna Bi Asha anavyolazimika kumtoa Salma ili afunge ndoa na jini kama ni rushwa ya kile alichoahidi pindi akipata mtoto. Katika hadithi ya Kilichomfanya Nyoka Kukosa Miguu tunaibuwa dhamira ya uvivu kutokana na nyoka kuchelewa hadi miguu yote inapochukuliwa na jongoo akajibandike yeye. Katika hadithi ya Rajabu imesawiri dhamira ya ukoloni mamboleo pale tunasimuliwa tukio la jini anayejigeuza ndege, umbo jengine la kutisha na hatimae jini ili kumtisha Rajabu. Katika hadithi hii pia tunaona namna tunavyoibuliwa dhamira ya ushujaa kutokana na kitendo cha usihiri ambapo Rajabu anawashitua majini waliokuwepo kwenye sherehe hiyo na wote wanakufa.

Hivyo utafiti huu umefanikiwa kuziba pengo lililokuwepo linalohusu matumizi ya usihiri na namna yanavyoibua dhamira katika ngano za Zanzibar. Ni matumaini ya mtafiti kwamba utafiti huu utakua kichcheo kwa watafiti wengine kutathmini matumizi ya vipengele vya usihiri katika tanzu nyengine za fasihi ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na fasihi andishi na fasihi simulizi.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya vipengele vya usihiri katika ngano za Zanzibar. Katika utafiti huu tumebaini kuwa vipengele vya usihiri vimekuwa vikitumiwa na watunzi wa ngano za Zanzibar ili kusawiri dhamira kadhaa za kijamii. Ujumi wa kutumia vipengele vya usihiri katika ngano Zanzibar umekuwa na athari kubwa katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Kwa ujumla usihiri katika ngano za

Zanzibar haukusawiriwa tu kama sehemu ya uchawi na ushirikina bali ni mbinu inayotumika kusawiri dhamira kadhaa za kijamii kama vile; uchawi na ushirikina, ujasiri, malezi, ushujaa, uongozi mbaya, utu, kiburi, uvivu, ukarimu, ujanja, uhalifu, umaskini na nafasi ya mwanamke katika maisha ya kila siku. Hivyo basi, tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa ngano za Zanzibar ni bohari ya uhalisia wa jamii ya Wazanzibar katika miongo kadhaa ambayo jamii ya visiwa hivi imepitia.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu unahitimisha kuwa ngano za Zanzibar zimetumia vipengele vya kisihiri ambavyo huibua dhamira Hivyo basi, utafiti huu unapendekeza mambo yafuatayo:

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine

Utafiti huu ulijikita kuvichunguza vipengele vya usihiri na namna vinavyoibua dhamira. Hivyo ni wazi kwamba bado ipo nafasi ya kufanya tafiti nyengine katika ngano za Zanzibar katika vipengele vyengine vya fani na maudhui.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Watunga Sera

Utafiti unapendekeza kwamba ipo haja kwa watunga sera kuchukua mawazo yanayojadiliwa katika tafiti mbalimbali katika jamii ili kutatua matatizo kadhaa yanayoikabili jamii. Kwa kufanya hivyo tutaweza kujenga mustakabali mzuri wa maisha ya jamii.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Taifa

Kwa upande wa Serikali kupitia asasi za kielimu inapaswa kuhamasisha wasomi juu ya swala zima la kufanya tafiti za kitaaluma ikiwemo eneo maalum la fasihi pamoja

na  fasihi simulizi ambayo inaonekana kufifia,ili kuweza kuimarisha taaluma hiyo katika maendeleo ya elimu nchini Tanzania na dunia kwa ujumla. Juhudi hizo zitasaidia kuongeza kasi mpya ya wanajamii ikiwemo wasomi kuweza kuisaidia serikali kuongeza wataalamu waliobobea katika tasnia ya fasihi.

**Mapendekezo kwa Jamii**

Jamii ina wajibu mkubwa wa kujifunza taaluma mbalimbali ikiwemo taaluma ya fasihi, Mtafiti anapendekeza kuwa wanajamii wawe na utamaduni wa kusimulia hadithi simulizi ikiwemo ngano ili kutanua maaarifa na kuwawezesha kufanya matendo mema na kuepuka maovu yanayo chorwa katika ngano hizo na kuakisi katika jamii. Mbali na hayo,jamii inapaswa kuwa na tabia ya usomaji wa vitabu kama vile riwaya tamthilia na hata tasnifu ili kutanua wigo wa maaria kwa mtu binafsi na kwa taifa kwa ujumla.

Jambo jengine kama mchango wa utafiti huu wanajamii wasilipuuze swala la ngano na kuona kuwa ni utanzu ambao umepitwa na wakati na hauna haja tena bali unafaa kuhifadhiwa na kuendelezwa kwani umuhimu wake ni mkubwa sana katika kuakisi matendo yanayotendka katika jamii.  Vile vile kwa upande wa Serekali ni vyema kuchukuwa jitihada za maksudi kuzihifadhi ngano za Zanzibar na kuwaendeleleza wale ambao wanauwezo mkubwa wa kuhifadhi hadithi simulizi kwani kufanya hivyo ni kutunza historia ya Zanzibar kupitia sanaa ya hadithi simulizi katika kipera cha ngano. Hii ni kutokana na kwamba ngano kwa kiasi kikubwa zilihifadhiwa kwa kutumia akilini mwa wanadamu jambo ambalo limeleta pengo kubwa kwani wengi wao waliozihifadhi wamefariki dunia.

**MAREJELEO**

Al- Farsy, A. B. (1993). *Qurani Takatifu: Chapa Mpya Iliyopitiwa Upya na Kuwekewa Tangulizi za Sura. Nairobi: Islamic Foundation*

Ali, H. A. (2015). *Kutathmini Usawiri wa Mhusika Mwanamke katika Hadithi Simulizi za Wapemba.* Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Bwanga, M. M. (2016). Kuchunguza Usawiri wa Mama wa Kambo Ndani ya Ngano (Hadithi) za Kiswahili za Zanzibar. Tasnifu ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Chaligha, E. N. (2013). *Vigezo vya Ruth Finnegan katika Utendi wa Lianja.* Katika Mulika Na. 32. Uk. 90.

Haji, A. I. (1983). *Fasihi Simulizi Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Creswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative and Methods Approches*. Los Angeles: SAGE publications.

Chanady, A. B. (1985). *Magical Realism and the Fantastic*. New York: Garland Publishing, Inc

Cohen, L. et al. (2000). *Research Methods in Education* (5th edition), London. Longman Ltd.

Mbatia, M. (2002). *Kamusi ya Fasihi* Nairobi Standard Text book

Mbode, J. P. (2005). Gabriel Ruhumbika: Janga Sugu la Wazawa (2002). Uchambuzi na Uhakiki katika Jarida la *Swahili Forum*, Toleo Na 12, ku. 81-93.

Morrison, K. (2000). *Research Method in Education* (5th ed.). London: Rontledge Press

Cooper, B. (1998) *Margical realism in West Africa*, Routledge: New York.

Enon, J.C (1998). *Educational Reseach: Statistics and Measurement 2nd Ed*. Kampala.Depatment of Distance Education Makerere University. Kampala.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford at the Clarendo press

Furlong, N. et al. (2003) *Research Methods and Statistics: An Integrated Approach*. Harcourt College Publishers: New York.

Gibbe, A. G. na Mvungi, T. A. (1987). *Fasihi Simulizi Sekondari na Vyuo.* Standard Publishing Dar es Salam: Company Limited

Jilala, H (2008), "The Artist Uses of Metaphors in constructing meaning in new generation songs in Tanzania" M.A Linguistic Desertation, University of Dar es Salaam.

John, L. (2007). *Critical Reading: A Guide*. In, http://www.Brocku.Ca/ English/jige/criticle Reading cited on 30th October 2017.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: Kenya: Paulines publicatios Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Reseach Methodogy: Methods and Techiniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Maeda, T. S. (2016). *Fasihi Simulizi.* Imepakuliwa 27/11/2017 kutoka https"// sw.m.wikipedia.org/wiki/ saa 10.20 alasiri

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale.* Dar es Salaam: TUKI.

Mutiso, K. (2012). *Motifu ya Hirizi katika Ushairi wa Kiislamu wa Kiswahili.* Katika Mulika Na. 31 uk. 115-133.

Mzee, M. M. (2015). *Kuchambua Maudhui yanayopatikana katika Hadithi za Watoto Katika Jamii ya Wapemba.* Tasnifu ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Ndumbaro, E. (2013). *Hadhi na Nafasi ya Fasihi Andishi ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa*.katika, chombozi blogspot. Com/imepakuliwa 15/11/2017 saa 11.00 jioni.

Njogu, K. na Chimerah C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*: Nairobi Jomo  Kenyata Foundation.

Nyamsenda, J. C. (2012). *Usawiri wa Taswira za Wahusika Wanyama Katika Ngano za Waikizu.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dar -es Salaam.

Nyamsenda, J. C. (2015). *Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Safari na Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari.* Tasnifu ya Uzamivu wa Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Hajji, H.O. (2013). *Nafasi ya Hadithi Simulizi katika Kufunza Maadili Mema Shule za Sekondari, Visiwani Zanzibar.* Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Oyoyo, J. O. (2013). *Uhakiki wa Fani katika Ngano za Kiswahili*. (Tasnifu ya M.A Kiswahili) Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapwa). Imepakuliwa leo 10-10-201 kutoka erepository.uonbi.ac.ke/bit

Rio, F. (1999). *Margical Realism Definitions.* Found on internet (Unpublished).

Robson, C. (2007). *How to do a research project: A guide for Undergraduate Students*. Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Sengo, T.S.Y.M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA

Senkoro, F. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre

_______ (1987) *Fasihi na Jamii*, Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

_______ (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salam:Dar es Salaa Universty Press.

_______ (1997) ‘‘The Significance of the Journey in FolkTales from Zanzibar’’, Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

________ (2006). *Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.* Katika *Kioo cha Lugha*, Juzuu 4. 22-38, Dar eS Salaam.

________ (2011). *Fasihi Andishi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Shemweta, G. (2015). *Itikadi katika Tamthilia za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ngwanamalundi na Fumoliongo.* Tasnifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Spata, A. V. (2003). *Research Methods: Science and Diversity*. USA: John Willey & Sons Inc.

Strecher, M. C (1999). *Magical Realism and the Search for Identity in the Fiction of Murakami Haruki.* Journala of Japanese Studies, Volume 25.

TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salam: Oxford Universty Press.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press

Vutagwa, F. L. (2013). Sifa za Kiuhalisiajabu na Umuhimu wake katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Waliaula, K. W. (2010). *Uhalisia na Uhalisia Mazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* Katika Swahili Forum, 17 (2010), ku. 143-157. Wamitila, K.W. (2002). Uhakiki waFasihi na Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: Phonix Publishers Ltd.

________ (2003). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoeni Publishers.

________ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Vide – muwa, Nairobi.

________(2013). *Mikakati ya Uhalisiajabu Katika Riwaya ya Kiswahili. Katika* Mulika Na. 32, uk, 1-12

Yin, R. K. (1994), *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Zamora, P. L na Faris, B.W. (1995). *Margical Realism Theory: History Community*, London.

## VIAMBATANISHO

**KIAMBATANISHO NA. 1 Hadithi ya Zimwi na Mkia**

**MTAMBAJI: Paukwa.**

**MTAMBAJI:** Hapo zamani za kale palikuwapo mama na watoto wake wanawake wawili , mmoja mkubwa na mmoja mdogo, watoto hawa walikuwa wakiitwa, Mize na Mboje ambapo Mize ni mkubwa na Mboje ni mdogo.

Siku zote Mboje alikuwa amezoea wanapokuja waume kwao kumtaka yeye alikuwa hayuko yayari mpaka wakafikia wanaume sita . Hata siku hiyo alipokuja mwanamme wa saba ambae ni zimwi walikubaliana nae bila ya kujua lolote kutokana na mwanamme huyo. Ikafanyika harusi na wakafanya maandalizi ya wakaondoka kuelekea nyumbani kwao kwa ajili ya kuanza maisha ya Mke na Mume, kabla ya kuondoka ndugu yake Mboje alimwambia kwamba atakapoondoka amchukue na yeye dada yake alikataa sana mpaka mama yao akaingilia kati akamwambia amchukue akakubali kumchukua wakaondoka pamoja . Mboje alipotaka kuondoka alipewa dawa na Mama yake katika vichupa vinne ambapo katika kichupa kimoja kilikuwa na vijiti, kimoja kilikuwa na vibenza , kimoja kilikuwa na bahari na kimoja kilikuwa na moto. Ilipofika siku ya safari waliondoka na walichukuwa muda mrefu kufika kwa sababu alikuwa amejenga nyumba mwituni. Mume wake Mboje alikuwa na tabia ya kuondoka nyumbani asubuhi kurudi usiku, hivyo alihitaji kupelekewa chakula na alikuwa anapelekewa na shemegi yake Mboje.

Mboje alikuwa anamwita shemegi yake ili aje achukue chakula lakini alipokuwa anamwita alikuwa anaona mkia unampiga usoni na anamuona shemegi yake

ameshafika anampa chakula na kuondoka . Kila siku zilivyokua zinakwenda mbele aliona hali ni ile ile aliamua kumwambia dada yake kwamba shemegi yake ni Zimwi lakini alipomwambia dada yake alipinga na akamwambia ndio maana nilikataa kukuchukua lakini ulifanya ukaidi.

Siku moja Mize aliamua kwenda kupeleka chakula mwenyewe ili kubaini kama mume wake ni zimwi au anasema uongo tu. Aliondoka na kwenda alipofika nyumbani kwake alimwambia ndugu yake kwamba yale anayosema ni kweli, kwa hiyo waandae safari ya kundoka na kurudi kwao.Zena Mize na ndugu yake wakiwa wanapanga njama za kwenda kuwala ambapo mumewake ndie aliekuwa muongozaji wa kundi hilo. Asubuhi mapema waliamka na kuanza kukunja ili kujitaarisha na safari na mazimwi nao walikuwa wapo njiani wanakuja . Mize na ndugu yake walikunja vitu vyote na kuingiza kwenye kikapu na wenyewe na wenyewe wakaingia na kuanza kuimba kwa ajili ya kuondoka " kikapu pa ! pa ! pa! na kikapu kikaanza kupaaa juu na kuondoka.

Baada ya kuondoka mazimwi walitokea lakini walipoingia ndani hawakuona chochote wakaanza kuangalia juu wakaona kikapu kinapaa wakaanza kukifuata ili kitakapotuwa wawapate. Baada ya kuona hivyo Mboje alianza kumwaga kichupa cha ujiti wakawa wanachomwa na vijiti huku wanaendelea na safari baadae akamwaga kichupa cha vibenza wakawa wanachomwa na vibenza lakini hawakusimama waliendelea na safari na mwisho akamwaga kichupa cha moto wakaungua wote wale Mize na Mboje wakaenda zao mpaka kwao walipofika walimuhadithia mama yao yote yaliyo wafika na akasema Mboje ndie aliemsaidia.

**KIAMBATANISHO NA. 2 Hadithi ya Zena**

MTAMBAJI: Hadithi hadithi

HADHIRA: Hadithi njoo utamu kolea.

MTAMBAJI: Hapo zamani za kale alikuwepo Zena na Zainabu ambao walikuwa na baba mmoja na mama kila mtu wake Zena mama yake akafariki akaenda kukaa na mama wa kambo na kwa bahati mbaya mama yake akawa hampendi na akawa anatafuta njama za kumuuwa mtoto huyo. Kadri ya siku zilivyoendelea siku moja mama akamkusanyia nguo na vyombo ili akafue mtoni ambako hakuendi watu, mtoto akamwambia mama yake kule hakwendi watu na mtu akienda analiwa na mazimwi mama yake akamwambia utakwenda hivyo hivyo nataka wende ukanioshee . Siku ya pili mtoto akachukuwa nguo na vyombo akaenda mtoni alipofika njiani karibu na ule mto akaanza kusikia sauti za mazimwi ya kimwambia Zena, Zena Zena huku hakuna watu na wala hakuji watu na wakija hawarudi . Zena akasema mimi ni mtoto ambae na kaa na mama wa kambo nilimwambia kama huku hakuji watu na wakija hwarudi lakini akanambia nije hivyo hivyo kwa sababu anataka nife huku nisirudi tena kwake yale mazimwi yakamsikiliza mtoto Yule yale anayoyasema na wakamuonea huruma sana na wakamwambia usiwe na khofu sisi tutakusaidia . Chukuwa nguo na vyombo wende ukafue mtoni na mto ule ndio ambao tunaishi sisi kwa hivyo ukimaliza kufua nenda kati kati ya mto chukuwa maji ujimwagie mwili mzima na chochote ambacho utakiona usije ukashangaa ni sisi ambao tutafanya hivyo. Alipo maliza akachukuwa maji na akajimwagia papo hapo akageuka na kuwa muarabu na kujiona yuko msafi tofauti na alivyokuwa baadae akaenda zake alipofika kwao mama yake akamshangaa sana na zainab aliporudi Skuli akamuona zena

amebadilika  akamwambia mama yake mimi nataka kwenda mtoni nami nikawe muarabu mama yake akamwambia sawa. Siku ilipofika Zainabu akaenda mtoni alipofika mazimwi hawakummuuuliza kitu bali walianza kumla na kumbakisha mifupa ndani ya maji.  Baada ya muda kupita mama yake akaingiwa na khofu kubwa mtoto wake hakurudi mtoni na akatoka akaenda kumfuata alipofika akaona mifupa ndani ya maji  inaelea na akasema bila shaka mwanangu ameshaliwa na muda si mrefu nay eye akaliwa na Zena akaishi na baba yake vizuri na akapata mama mwengine ambae anamthamini na maisha yake yakawa raha mustarehe na hadithi ikamalizia hapo.

**KIAMBATANISHO NA.  3  Hadithi ya Raajabu**

Hapo zamani za kale alikuwepo masikini akijuilikana kwa jina la bwana Makame , ambaye alikuwa na mke na watoto wawili, Rajab na Shaaban. Bwana Makame  na Mke wake waliwalea watoto wao vyema . Waliwafundisha tabia na adabu nzuri. Rajabu alipofika umri wa miaka kumi mama yake akafa akabakia  Bwana Makame peke yake akaendelea kuwalea watoto wake . Shaaban alipofikia umri wa miaka minane baba yake nae akafa watoto wakabakia peke nyao  maskini  Rajab ulezi ulimuandama wa kumlea mdogo wake. Rajab hakujua kazi ya kufanya ila kwenda majumbani kufanya kazi ya  kuosha vyombo, kufyagia na kufuo nguo ili apate pesa za ktumia, wakati wa jioni husuka makuti na kuyauza  pesa alizopata akitumia kununua chakula chao, maisha hya yaliendelea muda mrefu  siku moja Rajabu alimuaga ndugu yake akaondoka nyumbani alfajiri akaenda pwani kutafuta ngarawa mbovu na isiyotakiwa tena akafanikiwa kuipata  na akaitengeneza  wakati ngalawa

iko katika matengenezo aliomba nafasi kwa wavuvi ili apate uzoefu akapewa na kuanza kuvua mara ngalawa ilipo malizika akwaomba radhi wale wavuvi na akaanza kuvua katika ngalawa yake katika harakati zake za uvuvi baadhi ya siku alikuwa anapata samaki siku nyengine hakubahatika . Siku moja aliondoka usiku kama ilivyokawaida yake na kwa bahati mbaya ulivuma upepo mkubwa wavuvi wote wakapoteana Rajab alijiona peke yake anakwenda upepo unamchukuwa mbele yake kwa mbali sana akaona nyumba kubwa yenye kung'ara mataa tokea chini mpaka juu akaufuata mwangaza huo mpaka akafika karibu na ile nyumba akatupa nanga akashuka bila kuogopa chochote , alisogea karibu na nyumba akaona milango yote iko wazi lakini hakuona mtu wala sauti hakuisikia alinyemelea akaingia ndani akapanda ngazi mpaka juu, alipofika juu alipanda ngazi na kuingia vyumbani akaona pesa zimejaa tele, dhahabu, almasi, Michele, nguo na viatu na alipo toka nje ya nyumba akaona kiti cha dhahabu kipo kwenye roshani , hakusita alikwenda kukikalia huku akiangalia mandhar ya bahari. Baada ya muda akatokea ndege akafika karibu ya nyumba na akajigeuza kuliko nyumba Rajab akatulia katika kiti cha enzi anatizama miujiza mara akajigeuza mtu mrefu sana asiye kuwa na mwisho mara akajigeuza moto unaowaka na mwisho akajigeuza umbo la binadamu akaingia ndani ya nyumba akamsogelea Rajab akamtolea salaam huyu ni jinni, wakasalmiana baadae ji ni akamuuliza Rajabu wewe ni nani umekuja kufanya nini katika nyumba hii Rajab akamjibu mimi ni Ziraili nimekuja kukutoa roho ! jini kusikia sauti hiyo alitetemeka akalia huku akisema Bwana Ziraili tafadhali usinitoe roho yangu haina sadaka badala yake? Sadaka badala ya roho yako ipo jee utaiweza ? Jini alikubali naam nitaiweza bila yawasiwasi, sadaka ya roho yako ni kuwa uihame nyumba hii na wala usirudi tena maisha yako yote pia habari hii usimwambie mtu yeyote katika

maisha yako utaposema nitakutokea nikutoe roho Jini aliaga na akakunja kila kitu akaondoka Rajabu alipoona jinni ameondoka akaingia ndani akakusanya fedha, dhahabu, almasi, Michele, na nguo akiviteremsha chini vitu vyote akapakia akang'oa nanga akarejea kwao. Kuanzia hapo Rajabu na ndugu yake wakaishi maisha ya kifahari., baada ya muda kupita Shaabani alitamani kupelekwa ulipopatikana utajiri Rajab akampeleka walipofika kwenye hile nyumba wakisikia kelele na zogo jingi wala watu hawaonekani kutokana na hali hiyo Shaabani akamwambia kakayake warudi lakini Rajabu i alikataa akaingia ndani akaona sinia kubwa limeegemezwa ukuta hapo ukumbini Rajabu akajificha nyuma ya sinia akakaa kimya akasikiliza majini wakistarehe katika karamu yao. Baada ya kumaliza kula mwenyeji wao alieleza mkasa ulio mpata katika nyumba hile pale alipo kuja kurudi kwao na kumuona binadamu akajigeuza ndege mkubwa kuliko nyumba hii hakuogopa tena nikajifanya mrefu bila ya kiasi pia hakuogopa mwisho nikajigeuza moto hata hivyo hakuogopa alikaa kimya nilipojigeuza binadamu nikamsalimia akaniitikia nikamuuliza wewe ni nani akajibu mimi ni Ziraili nimetumwa nikutoe roho akaeleza kama walivyokubaliana mara akajitokeza na akamwambia miadi yetu imeshafika kwani hukutekeleza tulivyokubaliana nimeshafika ni kutoe roho kwa hofu kubwa majini wote wakaanguka chini wakafa. Rajabu alipoona wameshakufa akaanza tena kukusanya mali na kuipakia na kurudi tena kwao wakiwa na ongezeko kubwa la utajiri. Mwisho wa hadithi.

***KIAMBATANISHO* NA. 4 Hadithi ya Kijoka**

MTAMBAJI: PAUKWA

HADHIRA: PAKAWA

MTAMBAJI: Hapo zamani za kale alikuwepo mama mmoja ambae alikuwa hajapata mtoto, siku moja mama huyu alikwenda kutafuta kuni, akaona gogo akalichanga mara akatoka nyoka, mama akasema heee ! angalau na mimi mungu angenijaalia ni kazaa mtoto japo kama hiki kijoka. Yule mama aliendelea kukaa kwa siku nyingi mpaka akasahau kuwa aliomba mtoto, kwa bahati mama akabeba ujauzito na akazaa kijoka cha kiume, kutokana na hamu yake ya kutaka mtoto yule mama alifurahi sana kwa kupata mtoto huyo, akamlea mpaka akafikia umri wa miaka saba msiku moja akamtuma mtumishi wake anaemshughulikia akamuimbia wimbo:

Kanu wangu Kanu wangu, Kanu

Nenda kamwambie mama, Kanu

Kuwa kijoka ataka tohara, Kanu

Aliposikia hivyo Kanu akaenda kumwambia mama yake kijoka kuwa mwanawe anataka kutahiriwa, kwa vile mama alikuwa na uwezo mkubwa na mali nyingi akampa yaya kinu na nchi wa dhahabu.

Ilikuwa kila anapopita watu wanamkejeli kwa kusema kwamba sitafuti kujatafunwa na nyoka, baada ya kuzunguka sana alitokea bwana mmoja mzee wa makamo kidogo akasema mimi nitakwenda kumtahiri na akaenda kumtahiri akapewa kinu na nchi . Walikaa baada ya muda Kijoka akamwambia Kanu

Kanu wangu Kanu wangu, Kanu

Nenda kamwambie mama,  Kanu

Kuwa Kijoka ataka mke, Kanu

Kanu akaenda kwa mama yake Kijoka akamwambia kuwa  Kijoka ataka mke mama akasema sawa, akamwita yaya akamwambia  apige mbiyu ya mgambo atangaze kuwa atakaekubali kuolewa na kijoka atapewa pesa nyingi na nyumba kubwa ya kifahari . Mbiu ilianza lakini kila mtu aliesikia alisema aaaa!  Nimpe mwanangu Kijoka amtafune, sifanyi kosa hilo , baadae mwisho wa mji akatokea mwari mmoja akasema mimi namtaka hata kama ni kijoka, akamwambia mama yake achukuwe zile mali ili watokane na umskini  mkubwa walionao na yeye akaolewe na kijoka.

Kwa hivyo wazee wa Yule mwari wakenda wakamuozesha kijoka mtoto wao lakini walikuwa na hofu ya mtoto wao kutafunwa na nyoka  lakini kutokana na umaskini wao wakaona wamombe Mungu tu. Kumbe Yule Kijoka alikuwa sinyoka bali alikuwa ni mvulana mzuri sana wa Kiarabu, kwa hivyo mke wake akagunduwa kuwa mumewake alikuwa ni mtu kamili na mumewake akataka asimwambie mtu kuwa yeye si nyoka .

Waliishi siku nyingi sikumoja akamwita Kanu akamwambia ;
Knu wangu Kanu wangu , Kanu
Nenda kamwambie mama Kanu
Kijoka atoka nje, walimwengu wamuone.
Aeee! Kanu walimwengu wamuone.

Kanu akaenda kwa mama yake kijoka akamwambia kuwa Kijoka anatka kutoka nje, mama yake akaona sasa huu mtihani, mwanangu hatauliwa akaona bora amkataze asitoke lakini kijoka akasema bora nitoke. Huko nje watu wakaambiwa wakaona

wajilinde  wakakaa na mapanga, mashoka na marungu wanataka kumuuwa Kijoka. Mara Kijoka akatoka na mke wake wakiwa wamependeza  na watu wakamuona kuwa sio nyoka  bali ni mtu mzuri, watu wakashangaa na zile silahazao zote wakazitupa chini na wakabaki wanalalamika kuwa walidanganywa kumbe si nyoka ni mtu nzuri tena mwenye mali , na hadithi ikaishia hapo.

**KIAMBATANISHO NA.  5  Hadithi ya Abanawasi na Sufuria**

MTAMBAJI: Paukwa.

HADHIRA: Pakawa.

MTAMBAJI: Sikumoja punda wa Abanawas alikuwa na kiu. Chombo cha kumtilia maji apate kunywa hana. Akaenda kwa jirani yake, akamwambia niazime sufuria nimnyweshee punda wangu maji. Akampa sufuria, akaenda zake. Akakaa nayo siku tatu siku ya nne, akatwaa ile sufuria, akatia na kisufuria kidogo ndani, akampelekea mwenyewe. Akamwambia sufuria yako hii. Akaitwaa, akaona ndani kisufuria kidogo, akauliza "hiki kisufuria kidogo ni cha ani?". Abanawasi akasema, "mimi sio mwizi siwezi kuiba mali ya watu; sufuria yako imezaa kwangu na huyu mtoto wake. Nina mwiko wangu nikikorogea sufuria hupata mtoto." Yule mwenye sufuria akafurahi sana, akanena nyumba ya Abanawasi inabaraka sana, inazaa hata sufuria. Hivyo akamwambia Abanawasi aichuke ile sufuria ili akakae nayo tena mpaka izae. Abanawasi akakubali hilo.

Abanawasi alipofika nyumbani aliitafutia mtu akaiuza ile sufuria. Huku Yule mwenyewe akitarajia kupata sufuria nyengine itakayozaliwa. Akakaa kwa muda

mrefu bila kumuuliza hadi mwaka na nusu ulipopita. Siku moja Yule mtu akamwendea Abanawasi akamwambia nipatie sufuria yangu na hizo zilizozaliwa. Abanawasi akamjibu kwamba sufuria yako ilikufa wakati wa harakati za kujifungua na hata mtoto aliyekuwa anataka kuzaliwa alikufa tumboni na nilizizika tokea mwaka jana. Kusikia hivyo Yule mtu hakuwa na lakusema. Na hadithi ikamalizia hapo.

**KIAMBATANISHO NA. 6 Hadithi ya Mbwa Mahoka.**

MTAMBAJI: Paukwa.
PAKAWA: Pakawa.

MTAMBAJI: Hapo zamani za kale alikuwepo mzee mmoja na mbwa wake saba. Mzee huyo aliwajengea mbwa wake banda zuri na alikuwa na mazoea ya kutoka nao kila siku katika shughuli zake za msituni. Mbwa wale walijenga mapenzi makubwa na bwana wao. Wanapokuwa safarini mbwa wale walikuwa na tabia ya kumzunguruka kwa miliao na minung`uniko inayompa faraja mzee huyo. Kazi yeke ilikuwa ni kupiga paa kwa kutumia mkuki unaosadikiwa kuwa ulikuwa si bure bali una ucahwi.

Siku moja katika matembezi yake kwenye viunga vya mji alipata ashiki ya kwenda mawindoni bila ya kufuatana na mbwa wake waliomzoea. Alipokuwa katikati ya msituni katika harakati za mawindo alijikuta amezunguukwa na mazimwi wala watu pande zote na kwanza hakujua la kufanya. Katika kutapatapa ili kujiokoa na mazimwi yale alijikuta akiimba hivi:

“Mbwa wangu mahoka
Mbwa wangu mahoka
Mwaniacha naliwa ni mazimwi
Mbwa wangu mahoka”

Mbwa mmoja alisema kuwambia wenzake sikilizeni, nimesikia sauti ya bwana wetu akiwa katika mashaka anaomba msaada wetu. Mbwa mkubwa akajibu “muongo wee mimi mwenye masikio saba sijasikia, usikie weye mwenye sikio moja!”

Yule mzee akaimba tena mara ya pili kama hivi:
“Mbwa wangu mahoka
Mbwa wangu mahoka
Mwaniacha naliwa ni mazimwi
Mbwa wangu mahoka”

Mbwa mwengine akasema kuwa “nami sasa nimesikia sauti ya bwana wetu ikiomba msaada tufanyeni shauri tukamuokoe” Mbwa mkubwa akasema “nawe sasa umekuwa mzushi itakuwaje usikie weye mwenye masikio mawili kuliko miye mwenye masikio saba?”

Mzee akaendelea kuimba mara ya tatu, ya nne, ya tano na ya sita. Akiwa amekaribia kukata tamaa akaimba tena mara ya sita kwa majonzi na kutoa sauti iliyomfikia mbwa mkubwa mwenye masikio saba. Hapo mbwa waliamua kuusukuma mlango na kufuata sauti ilikokuwa inatokea ili kutoa msaada. Huku nao wakiimba hivi:

“Bwana wetu mwema

Sisi tuko nyuma yako

Kwa juhudi na maarifa

Kulinda maisha yako”

Mbwa walipofika mbele ya bwana wao waliyakuta mazimwi yanahaha kudai roho ya mzee huyo. Nao hawakupoteza muda walilirukia lile zimwi kubwa lenye mikia saba na ndimi saba na kulivamia. Zimwi lilitapatapa kwa utungu mkubwa wa mauti hadi lilikata roho. Baada ya kukata roho liligeuka moshi mkubwa uliowatisha mazimwi wote msituni. Katika harakati za kushangaa mazimwi yale, Yule mzee alipata fursa ya kuwatoroka na akawa salama wa salimini. Na hadithi ikamalizia hapo.

**KIAMBATANISHO NA. 7 Hadithi ya Tatu na Saida**

MTAMBAJI: Paukwa.

HADHIRA: Pakawa.

MTAMBAJI: Hapo zamani, zama za mababu palitokea mzee mmoja aliyepata mtoto wa kike aliyeitwa Saida. Saida alipozaliwa kupitia kwenye goti, kwani haikuwezekana kutoka katika njia ya kawaida kutokana na ugonjwa mkubwa wa mama yake- mama huyo alifariki na kumuacha Saida katika dunia akiwa na siku moja tu toka kuzaliwa.

Baba yake alimpenda sana Saida na kumtafutia mtu wa kumnyonyesha, ila ilishindikana kwa sababu watu walihofia maajabu ya kuzaliwa kwake. Baba yake alimlea na kumtunza sana na siku zote hakumruhusu kutoka nje kwa kuhofia watoto wa jirani walioelekezwa na wazazi wao kwamba Saida si binadamu kwa sababu alizaliwa kupitia kwenye goti.

Baada ya miaka sita tokea kuzaliwa kwa Saida baba yake alioa mke mwengine na alipata mtoto wa kike pia, ambaye alimwita Tatu. Saida na tatu ni baba mmoja ila

Saida akaangukia mikononi mwa mama wa kambo. Mama huyo alimchukia sana Saida.

Saida kila siku akiwa usingizini alikuwa akisomeshwa na marehemu mama yake hadi alipohitimu na kuwa maarifa mazuri. Walipokuwa vigori ilitokea nong`ono mwana wa Mfalme alikuwa akitafuta mchumba wa kuoa. Alitembea nyumba zote za kiamboni na katika aila yao kutafuta mchumba lakini hakupata aliyemridhisha. Siku ya saba akafika nyumbani kwao Tatu, kusikia taarifa hiyo mama akamtoa mwanae, Tatu mbele ya mtoto wa Mfalme lakini hakuridhika nae.

Mwana wa Mfalme aliuliza “Je humu ndani hamna msichana mwengine?” Mama yake Tatu alijibu kwa kitetemeshi kwamba hamuna.” Mwana wa Mfalme akasema “ikibainika muna mtu humu ndani mumemficha azabu yenu ni kifo.” Kusikia hivyo Tatu akasema “yumo ila ni kijakazi, mweusi na mchafu. Mwanamflme akasema “nileteeni.”

Alipoletwa Sada alimuona mzuri aliyetimiza kila sifa ya kuwa mwana wa Mfalme. Harusi ikaandaliwa na siku ilipofika akaolewa na kuanza maisha mapya katika jumba la kifalme.

Tatu na mama yake walichukia sana na wakaamua kutaka kumuangamiza. Ili kutimiza hilo, Mganga akampa sindano ambayo alimuelekeza amchome mara saba Saida kichwani na atageuka kuwa ndege wakati huo iwpo atanuia kwa kusema “kuwa ndege.” Atakapofanya hivyo Tatu atakuwa mke wa mtoto wa Mfalme bila jambo hilo kujuilikana na yoyote. Hapo sasa Tatu akafundishwa ususi na mama yake hadi alipofahamu vema.

Siku moja Tatu alikwenda kumtembelea dada yake na kumwambia amsuke. Wakati akimsuka alifuata maagizo ya mganga, akamdunga Saida sindano kichwani huku akimwambia kuwa ilikuwa anamng`oa mvi. Baada ya kumdunga sindano mara saba Saida aligeuka ndege na kuruka kupitia dirishani. Sasa Tatu akawa ndie mke wa mtoto wa Mfalme. Siku ya pili baada ya tukio hilo mtoto wa Mfalme alipotoka kuelekea msikitini Yule ndege alitua kwenye bustani karibu na dirish la Tatu na kuimba hivi:

Ndege: Kibaraka kibaraka

Tatu: Labee bibi labee

Ndege: Kibaraka kibaraka

Tatu: Labee bibi labee

Ndege: Mume wako kenda wapi?

Tatu: Kenda msikitini kusali na kuadhini.

Ndege: Akija nisalimie!

Ndege baada ya kumaliza kusema hayo akaruka na kuondoka.

Siku ya pili mtoto wa Mfalme alipoenda msikitini ndege akaja na nyimbo ile ile hadi siku ya saba ambapo Tatu aliamua kumsimulia muumewe. Muume kusikia hayo aliamua kujitega ili kumnasa ndege Yule. Kamakawaida yake siku ya nane ulipofika muda alitua kama kawaida yake ndipo alipojikuta akitua ,mikononi mwa mwana wa Mflame.

Mtoto wa Mfalme aliajabia sana ndege yule mzuri ambaye hajapata kumuona katika maisha yake yote. Wakati akimgusa kichwani alihisi kunakitu kigumu. Alipokitoa kilikuwa sindano! Baada ya kuitoa ile sindano papo hapo ndege Yule alageuka na

kuwa sura ya Saida mke wake wa mwanzo. Baada ya hapo nyumba ilijaa nuru kama mwanzo. Baadae Saida alisimulia mkasa wote huku Tatu na mama yake wakibakia kuona aibu kwa walivyotenda. Tangu siku hiyo Saida akaishi na muume wake kwa raha mustarehe.

**KIAMBATANISHO NA. 8 Hadithi ya Mazimwi Wala Watu**

MTAMBAJI: Paukwa

HADHIRA: Pakawa

MTAMBAJI: Hapo zamani za kale walikuwa wakiishi watu karibu na msitu. Katika msitu huo inaaminika kwamba kulikuwa na mazimwi ambao walikuwa wanafanya sherehe kila mwisho wa mwezi. Katika sherehe hizo walikuwa wakipika vyakula vya namna mbalimbali. Hata hivyo cha kushangaza ni kwamba mazimwi hao walikuwa kitoeleo chao ni nyama za watu.

Watu walijenga hofu sana kutokana na tabia ya mazimwi hao. Mazimwi walikuwa hawachaguwi mkubwa wala mdogo. Siku moja mazimwi walimkamata Makame wa Makme na kumfunga kwa kamba huku wakiwa wanasubiri usiku wamchinje kwa ajili ya kitoeleo. Makame wa Makame alipiga kelele sana ili kujinusuru lakini ilikuwa ni kazi bure. Kelele zake zilikuwa kama gita ambalo lilikuwa likiwaburudisha mazimwi.

Katika mazimwi hao kulikuwa na zimwi msichana ambaye alikwenda hadi aple alipokuwa Makame wa Makame na kumpa siri kwamba mazimwi wanapokuwa wamelala usiku utasikia wanapiga kelele na wakiwa bado hawajalala huwa wako

kimya. Hivyo alimtaka atumie fursa hiyo ili kutoroka. Lakini alimtaka awe makini sana.

Makame wa Makame alipofika usiku alisibiri hadi aliposikia mazimwi wanaweka kelele akajua kwamba tayari mazimwi wameshalala. Hivyo haraka haraka alifungua zile kamba ambazo alikuwa amefungawa nazo na akatafuta njia akakimbia. Walipoamka mazimwi hawakumuona Makame wa Makame. Walimtafuta sana lakini ilikuwa ni kazi bure. Makame wa Makame alikwishafika kijijini na kusimulia yote yaliyomkuta. Tangu siku hiyo akawa makini sana kwenda katika msitu huo. Baade wanakijiji waiamua kuuvamia msitu na kuwafukuza mazimwi hao. Kuanzia hapo watu waliishi raha mustarehe.

**KIAMBATANISHO NA. 9 Hadithi ya Yamuimui**

MTAMBAJI: Paukwa

HADHIRA: Pakawa

MTAMBAJI: Hapo zamani za kale walikuwepo wanakijiji, mwanakijiji mmoja alizaa mtoto mzuri sana, mtotot huyuo alikuwa akiitwa Yamuimui , pale kijijini kila mtu alikuwa akimsifu Yamuimui kwa uzuri wake , jambo ambalo watoto wenzake walichukizwa nalo sana, siku moja watoto walipanga kumuuwa Yamumuimui, walikwenda hadi kwa mama yake wakamuomba ili amruhusu wende wakacheze na kuvua kombe bwachini kwa bahati mama yake Yamuimui alikubali wakaondoka nae wakaenda nae mwituni , kisha wakamwambia sisi hatunaraha mtaani kwa sababu yako eti kwa kuwa umzuri sana , sasa leo tunataka tukuuwe ili balaa lituondokee angalau na sisi mtaani tupumzike kudharauliwa kwa sura zetu mbaya , wakafanikiwa

kumuuwa walipomaliza kumuuwa wakampachika juu ya panda la mti  na wao wakarudi majumbani kwao. Mama yake Yamuimui alipoona muda umezidi kuwa mkubwa akaona bora akawaulize watoto wenzake Yamuimui yukom wapi mbona hajarudi nyumbani? Watoto wakamjibu sisi hatujui kwani tumerudi nae zamani na tumemuacha anakwenda nymbani kwao. Mara mama baada ya kuondoka tu alifuatwa na mbwa na akawa anabweka sana na baadae mbwa akaimba;

Yamuimui…Yamuimui
Kapachikwa kwenye mti kulee kulee
Watu wende nami nende nikasikilize kilio
Yamuimui kauwawa.

Baadhi ya watu wakasema, jamani tumfuateni huyu mbwa huenda ikawa ameona jambo, kwa hivyo baadhi ya watu wakamfuata mbwa na mbwa akenda mpaka iliko maiti ya Yamuimuin na hapo watu wakabaini kuwa Yamuimui kauwawa, akachukuliwa akenda akazikwa na hadithi yangu iakaishia hapo.

**KIAMBATANISHO NA. 10 Hadithi ya Babu Dii**

MTAMBAJI: Hadithi… hadithi

HADHIRA: Hadithi njoo…utamkolea

MTAMBAJI: Hapo zamani za kale alikuwepo Babu Dii na mke wake na watoto wao saba, watu hawa walikuwa maskini sana hata chakula chao kilikuwa cha tabu , siku moja babu dii aliwaza sana kuhusu kupata kazi ili apate pesa akanunuwe chakula, aakaona ni bora aende nje ya kijiji chao akatafute kazi , akaenda mpaka ukoo akaona msitu mkubwa kwa mbali akaona sehemu inafuka moshi , akasema lazima nifike kule kunako fuka moshi akaenda akaenda akaenda hata hukoo akafika, akaona kijibanda kidogo, mara kikatoka kibibi kikongwe , kikamuuliza mjukuu wangu unakwenda wapi huku hakuji mtu ispokuwa awe na hisa miongoni mwetu, babu Dii akamwambia nimekuja kutafuta kazi , akamwambia kama unataka kazi njoo nikupe Babu Dii akachukuliwa mpaka kibandani bibi alipofika bibi akamwambia kama unataka kazi kwanza nirambe tongo zangu zote mpaka zimalize ili niweze kuona vizuri . Babu dii akamramba tongo Yule bibi mpaka zikamaliza ikawa anaona vizuri . Baada ya kumaliza babu dii alipewa pesa na mapande matatu ya dhahabu akayauze apate pesa zaidi ili aanze biashara yake mwenyewe, Babu Dii akaondoka, akarudi kwake na mali zake na hadithi ikamalizia hapo.

**KIAMBATANISHO NA. 11 Hadithi ya Tango**

MTAMBAJI: Paukwa.

HADHIRA: Pakawa.

MTAMBAJI: Hapo zamni za kale alitokea mzee mmoja akapanda mtango kando ya nyumba yake. Mtango ukazaa matango mawili makubwa, mzee Yule baaoa ya matngo kuzaliwa aliyatia dawa na kuyanuilia kusudi atakayeyaiba pindipo akiyala avimbe tubo na tumbo lipite likisema hivi;

Nataka tango langu, nataka tango langu.

Nataka tango langu, nataka tango langu.

Kufika siku ya saba yule kijana aliyeiba tago alivimba tumo mithili ya mjamzito na siku ya kumi na moja alfajiri sana alijisikia kichefuchefu na kulitapika lile tango likiwa zima, baada ya siku tatu lile tango lililotapikwa lilikuwa kubwa sana na likapelekwa nyumbani kwa yule mzee aliyepanda mtango kama malipo ya tango lake lililoibiwa.Mke wake alilipokea wakati mume wake akiwa shambani kwake. Mara baada ya kukipokea alichukua kisu, maji na sufuria kwa ajili ya kulimenya, kulikata aliona ajabu kubwa lile tango lilikuwa na nywele! Aliliacha hadi alipokuja muume wake akamsimulia mkasa mzima uliotokea. Tangu siku hiyo kilimo cha mzee huyu hakikuharibiwa tena na vijana. Kwa hali hiyo akawa anaendeleza kilimo chake kwa raha mustarehe.

**KIAMBATANISHO NA. 12 Hadithi ya Jini Kisiki**

MTAMBAJI: Hadithi… hadithi

HADHIRA: Hadithi njoo…utamkolea

MTAMBAJI: Hapozamani za kale alikuwepo mama na mume wake . Bi Ashsa na Mzee Ali . Mama huyu alikuwa na kawaida ya kwenda kondeni kila asubuhi ilipofika na alikuwa kwa bahati mbaya hajapata mtoto. Baada ya muda Bi Asha kabeba ujuzito na ikawa bado safari zake za kwenda kondeni zinaendelea . Siku moja alipofika njiani kuelekea bondeni alijikwaa kwa kisiki na akasema “kisiki weye mtoto nitakaye mzaa kama ni mwanamke nitakupa wewe “ baada ya siku kupita Bi Asha alijifunguwa mtoto wa kike na akamwita Salma, Salma aliendelea kukuwa mpaka akawa mkubwa akaanza kumfuata mama yake bondeni mpaka akazoea ikawa anakwenda bondeni peke yake . Siku moja alikuwa anapita pale penye kisiki akakisikia kisiki kinasema “Mwambie mama yako ile ahadi yangu bado . Yule Salma alipofika akamwambia mama yake akasema sawa. Salma akamuuliza mama yake ni ahadi gani, mama yake akamwambia nikupeleke wewe, ilipofika siku Bi Asha alimchukuwa mwanawe Salma na kumpeleka kwenye kisiki lakini kile kisiki kilikuwa ni jini , akajenga nyumba akaishi na mkewe Bi. Salma . Bi. Salma akaishi vizuri na majirani wakawa wanakuja kuchota maji na kuzungumza nae lakini kila walipo kuwa wanakwenda walikuwa hawamuoni mume wake alikuwa anakwenda kwake usiku na kuondoka alfajiri kwa hivyo majirani wakamuuliza mbona mume wako hatumuoni kila siku yuko wapi? Bi. Salma alipokuja mume wake wakamwambia majirani wote wananambia kwamba wanataka wakuone hawakujui kila siku wanapokuja hawakuoni, Yule mwanamme akamwambia Bi. Salma

nilikwambia vipi? Kwa hiyo kuanzia hivi sasa ondoka katika nyumba yangu Yule nyoka akaondoka na Salma akajikuta amerejea pale pale kwenye kisiki , majirani wote wakawa wanaendelea kumdharau Bi. Salma akaondoka na kurudi kwa mama yake alipofika kwa mama yake akaambiwa na mama yake akamtafute mumewe popote alipo . Bi.Salma akatoka akenda kumtafuta akaandaa mikate saba , akiwa njiani kuelekea aliko mume wake alikuwa anakutana na watu wanamwambia huku hakwendi watu na kama unataka wende acha mkate mmoja halafu upite akenda hivyo hivyo alipofika mtu wa saba akamuuliza kuhusu mume wake kuwa anamjuwa na ni mkuu wa majini na leo anaharusi akamwambia kamwite, alipokuja akamuona akamwambia nimekuja kukutafuta wewe akasema kama ni hivyo itabidi ni kuuwe wewe na Yule mwengine niachane nae , akamchukuwa akenda nae kwenye harusi lakini walipokuwa wanapita njiani watu walikuwa wanajikata mikono kwa kumtazama yeye alipofika harusini akamuoa na akakaanae pale pale.

**KIAMBATANISHO NA. 13 Hadithi ya Kilichomponza Nyoka Akakosa Maguu**

MTAMBAJI: Hadithi… hadithi

HADHIRA: Hadithi njoo…utamkolea

MTAMBAJI: Hapo zamani za kale walipanga wanyama wote wakusanyike kwa ajili ya mgawanyo wa miguu ili waweze kutembea hata kwa masafa ya mbali pasi na usumbufu wowote . Kwa hivyo viongozi wa wanyama wakapanga wakusanyike kwa muda wa siku tatu muda wa wanyama wote kuhudhuria ni saambili kamili asubuhi .

Kufika saa mbili kamili asubuhi wanyama wote walikuwa wameshafika, kwa ajili ya kuanza kuchukuwa miguu yao ispokuwa nyoka ilikuwa bado hajawasili. Nyoka kwa uvivu wake alichelewa kuamka, mara baada ya kuamka akajishughulisha huku na huku, alipofika kwenye mgawanyo wa miguu walikuwa wanyama wote wameshatawanyika na kila mmoja ameshapata mgawanyo wake , Jongoo ambaye alikuwa ndiye aliyekuwa akigawanya miguu, kwa hivyo jongoo baada ya kuona hadi saa nne hakuna mnyama aliyetokea akaamuwa miguu yote iliyobakia ajibandike yeye, hata alipo wasili nyoka wanyama wote wameshatawanyika na kila mmoja ameshapata mgawanyo wake . Nyoka kuona hali hii alisikitika sana lakini masikitiko yake hayakusaidia kitu chochote , kwa hiyo hadi leo nyoka amekosa mi

**Kiambatanisho Na. 14**

**MWONGOZO WA MASWALI YA MIJADALA YA VIKUNDI KWA AJILI YA WALIMU WA FASIHI WA SHULE ZA SEKONDARI**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Usihiri katika Ngano za Zanzibar.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usihiri katika ngano za Zanzibar  na kuona ni jinsi gani usihiri unavyotumika kuibua dhamira. Kumbuka taarifa zote zilizotolewa zimehifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mshiriki na pia zimetumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

1. Unafikiri ngano zinaweza kutumia mbinu za usihiri katika kuzisanii?
2. Unadhani  kuna matumizi ya usihiri katika ngano za Zanzibar?
3. Taja vipengele vya usihiri vilivyotumika katika ngano za Zanzibar.
4. Je, ni vipengele vipi vya usihiri vimeibua dhamira?
5. Bainisha dhamira zinazojidhihirisha katika vipengele vya usihiri katika ngano teule za Zanzibar .

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**Kiambatanisho Na. 15**

**Picha ya Mtafiti Akiwa na Mtafitiwa**



Mtafiti (kulia) akiwa na mtafitiwa akitambiwa ngano.

**Kiambatanisho Na. 16**

**Picha ya mtafiti akitambiwa Ngano**



**Picha ya mtafiti (aliye kamata simu) akitambiwa ngano na mtafitiwa.**

**Kiambatanisho Na. 17 Mtafiti akishiriki katika mijadala ya vikundi ya Walimu waskuli ya Chwaka Tumbe Sekondri kuhusu ngano.**



**Kiambatanisho Na. 18 Mtafiti akishiriki katika mijadala ya vikundi ya walimu waskuli ya Chwaka Tumbe Sekondri kuhusu ngano.**



**Kiambatanisho Na. 19 Mtafiti Akitambiwa Ngano na Mtafitiwa**

